

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 18 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na kikao chetu cha thelathini na mbili.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ningependa kutoa Taarifa inayohusiana na kukamilika kwa Mkutano wa Nne wa Bunge la Afrika Mashariki uliofanyika hapa kwetu tarehe 8 hadi 27 Aprili, 2018.

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia tarehe 8 hadi 27 Aprili, 2018 Bunge la Afrika Mashariki (*East Africa Legislative Assembly*) lilikuwa na Mkutano wake wa Nne ambao kwa mwaka huu ulifanyika hapa Tanzania na kipekee katika Ukumbi wa Msekwa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kuwa mkuutano wa kwanza kufanyika kwenye viwanja vyetu vya Bunge hapa Dodoma na wa kwanza kufanyika Tanzania chini ya Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 55(1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mikutano ya Bunge hili hufanyika kwa mzunguko mionganoni mwa nchi wanachama kila baada ya miaka miwili na nusu. Lengo la kufanyika mikutano hii kwa mzunguko ni kukuza ushirikiano na mawasiliano baina ya Bunge hilo na Mabunge ya nchi wanachama.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia taratibu za uendeshaji wa Bunge hilo wa kutoa fursa maalum kwa Rais wa Nchi mwenyeji kuhutubia kwenye mkutano husika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alihutubia Mkutano wa Bunge hili tarehe 24 Aprili, 2018 ambapo baadhi ya Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Bunge walihudhuria kwa niaba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano huo wa Nne wa Bunge la Afrika Mashariki shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwa ni pamoja:-

(i) Shughuli za Kamati za Bunge la Afrika Mashariki zilifanyika;

(ii) Kamati Ndogo ya Tume ya Utumishi wa Bunge la Afrika Mashariki ilikutana;

(iii) Miswada miwili ya Sheria ilijadiliwa na kuwasilishwa;

(iv) Mkutano wa kubadilishana uzoefu baina ya Kamati za Bunge la Afrika Mashariki na Kamati za Kudumu za Bunge letu ilifanyika;

(v) Palikuwa na kushiriki kwenye zoezi la upandaji miti 1,000 ambalo ilifanyika katika eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*);

(vi) Wabunge wa Afrika Mashariki waliweza kushiriki kwenye sherehe za miaka 54 ya Muungano wa Tanganyika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na Zanzibar zilizofanyika tarehe 26 Aprili, 2018 katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma; na

(vii) Pia walishiriki kwenye michezo ya kirafiki ya mpira wa miguu kati ya timu ya Bunge la Afrika Mashariki na timu yetu ya *Bunge Sports Club*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wabunge wote, kumshukuru Katibu wa Bunge na watumishi walioko chini yake wote na wadau wengine wote kwa namna tulivyoweza kushiriki kwa pamoja kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha mkutano huu.

Aidha, napenda kuwataarifu kwamba Spika wa Bunge la Afrika Mashariki ameniandikia barua kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Bunge kwa maandalizi mazuri yaliyofanyika na ofisi yetu ili kufanikisha mkutano huo. (*Makofi*)

Maandalizi hayo yaliyofanywa na Bunge letu yaliwezesha mkutano huo kufanyika kwa ufanisi na kumalizika kwa mafanikio makubwa. Ahsanteni. (*Makofi*)

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza litaulizwa kuelekea Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na litaulizwa na Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Khadija tafadhali.

Na. 266

Kuwawezesha Wanawake na Vijana Kiuchumi

MHE. KHADIJA NASSIR ALI aliuliza:-

Miongoni mwa matakwa ya Serikali ni kuwawezesha vijana na wanawake kiuchumi.

Je, Serikali inatekelezaje suala hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutungwa kwa Sera ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 pamoja na sheria mbalimbali zinazohusu uwezesaji wananchi kiuchumi, Serikali inatekeleza Mpango wa Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kama ifuatavyo:-

Moja, ni kutambua umuhimu wa mafunzo ili kuwawezesha wanawake na vijana kukuza shughuli zao za kiuchumi na kujikwamua kimaisha.

Pili, ni kuhamasisha vijana na wanawake kijiungu na vikundi vyakuchumi vyavyama vyakuweka Akiba na Kukopa (*SACCOS*) ili kujipatia kwa urahisi mitaji ya kuanzisha na kuendelez amiradi ya kibashara.

Tatu, ni kuwekeza katika Sekta ya Ufundisti ili vijana wanaohitimu waweze kuwa na ujuzi wa kuweza kujiajiri.

Nne, kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ni chanzo cha ajira kwa wanawake na vijana.

Tano, ni kuanzisha Benki ya Wanawake kwa lengo la kutoa mikopo kwa wajasiriamali wanawake na pia uwepo wa mifuko maalum ya uvezeshaji wa akina mama (*WDF*) na vijana (*YDF*).

SPIKA: Mheshimiwa Khadija, swali la nyongeza nimekuona.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nielezee masikitiko yangu juu ya majibu ya Serikali ambayo amenipatia.

Mheshimiwa Spika, majibu ambayo Serikali imeleta yako kisera zaidi, nilitegemea yaje majibu ambayo kidogo yangeleta taswira na mwanga kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelezea malalamiko yangu kwa vile tuko kwenye Mwezi Mtukufu wa Ramadhani lakini kwa kweli nimesikitishwa sana na majibu. Baada ya kusema hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali imepanua fursa ya elimu kwa kuongeza Vyuo Vikuu vyayeli na Elimu ya Kati. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendana basi na mahitaji yaliyopo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kiasi gani Mfuko wa Vijana umeweza kuwagusa walengwa ukizingatia na hali halisi iliyopo? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo likianzwa na kutoridhishwa kabisa na Mheshimiwa kwa majibu ya awali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali ya kuwawezesha vijana na akina mama na msingi mkubwa wa uwezeshaji huo unatokana na sera. Kwa hiyo, nimuondoe tu hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba majibu haya kwa sababu ya uwezeshaji na sera inatuelekeza hivyo ndiyo maana yalijikita hapo.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika swali lake la kwanza la kujua kuhusu ongezeko la idadi ya wahitimu wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Ufundi ikilinganishwa na nafasi za ajira. Kama Serikali na kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2014 ya *Integrated Labour Force Survey* ambayo imeeleza kinaga ubaga juu ya nafasi za ajira zinazotengenezwa kila mwaka lakini na watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka husika kwamba idadi imekuwa ni kubwa tofauti na nafasi za ajira ambazo zinatengenezwa.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali tuliona njia nyingine mbadala ni kuanza sasa kuwabadili mitazamo vijana wetu hasa wahitimu wa vyuo vikuu na kuamini kwamba bado wanaweza wakafanya shughuli zingine za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufunjaji na biashara na sisi kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuweza kuwawezesha ili kuweza kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu tafsiri kwa mujibu wa Sera ya Ajira ya mwaka 2008, ajira ni shughuli yoyote halali inayomuingizia mtu kipato. Kwa hiyo, tumeanza sasa kuwabadili mitazamo vijana wetu waanze kuamini kwamba si wote ambao wanaweza kwenda kukaa ofisini, lakini pia tunaandaa mazingira mazuri waweze kufanya kazi za kujajiri.

Mheshimiwa Spika, la pili ameuliza kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; ni kweli, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Sheria Na. 21 ya mwaka 1961, kifungu namba 21(1)

kilianzisha Mfuko wa Maendeleo wa Vijana ambao lengo lake ni kuhakikisha tunawagusa vijana wengi zaidi kwa kuwasaidia kupata mikopo na mitaji na mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninavyozungumza hivi sasa, tayari tumeshafikia vikundi vyta vijana 397 ambao tumeshatoa kiasi cha shilingi zaidi ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuwawezesha vijana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Khatib, swali tafadhali.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015, wakati tukienda kwenye uchaguzi mkuu, kila chama kiliuba sera zake kwa Watanzania. Chama cha Mapinduzi kilitangaza sera kuwapatia wananchi wa Tanzania kila kijiji shilingi milioni 50 sera ambayo iliwavutia sana Watanzania. Je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kutekeleza ahadi yake iliyoweka kwa Watanzania? Kama haijashindwa, ni lini pesa hizi zitapelekwa kwa vijiji vyote vya Tanzania? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, ni kweli katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020 tulieleza bayana ya kwamba moja katika ya mkakati mkubwa wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ilikuwa pia ni pamoja na utengwaji wa shilingi milioni 50 kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, narejea majibu yangu ya awali kwamba utaratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi huwa unakwenda sambamba na utayarishaji wa miundombinu rafiki ya kufanya mpango huu uweze kuwafikia wananchi kwa wakati. Tulijifunza katika mipango iliyopita ikiwa mabilioni ya JK na hivi sasa tunaendelea na mkakati wa kuona namna

bora ya miundombinu ambayo itawekwa ili fedha hizi pindi tutakapoanza utoaji wake, ziwafikie walengwa kwa uhakika na pia iende kufanya kazi ambayo itakuwa imekusudiwa.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa kwamba ni mpango wa Serikali na bado upo katika mchakato wa kuona namna bora ya kuweza kuandaa miundombinu hiyo.

SPIKA: Tunaendelea, bado tupo Wizara hii hii Waheshimiwa.Swali linalofuata la Mheshimiwa Zainab Katimba tafadhali.

Na. 267

Serikali Kutunga Sera ya Mafunzo kwa Vitendo Kazini

MHE. ZAINAB A. KATIMBA aliuliza:-

Vijana wengi wanakosa sifa za kuajiriwa kwa kukosa uzoefu kazini.

Je, Serikali haioni haja ya kutungwa kwa Sera ya Mafunzo kwa Vitendo Kazini kwa wahitimu wa elimu ya juu na vyuo vya ufundi (*Internship Policy for Higher Learning Institutions and Technical Colleges Graduates*) ili vijana waweze kupata ujuzi utakaoendana na mahitaji ya soko la ajira?

SPIKA: Majibu ya swali la vijana kutoka kwa Mbunge kijana tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha pengo la ujuzi (*skills mismatch*) kati ya ujuzi walinao wahitimu na ule

unaohitajika katika soko la ajira unazibwa. Ni kweli Serikali imeona kuna haja ya kuwa na miongozo ya kisera kama alivyoshauri Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba ambapo kupidia ofisi yangu tumeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu (*National Internship Guidelines*). Mwongozo huu unasaidia wadau kuandaa, kutekeleza, kusimamia na kuratibu mafunzo ya uzoefu kazini kwa wahitimu. Mwongozo huu ulizinduliwa mwezi Septemba, 2017 na kuanza kutumika rasmi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 zaidi ya nafasi 750 zimetolea na waajiri mbalimbali kuwezesha wahitimu kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 ili kuendana na mahitaji ya sasa. Sera mpya pamoja na mkakati wa utekelezaji wake ipo katika hatua za mwisho ambapo inatarajiwaa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2018. Mlongoni mwa matamko mahsusii ya sera hii ni pamoja na kusitiza kuwepo kwa mafunzo kwa vitendo kazini kwa wahitimu wa vyuo. Baada ya kupitishwa sera hii, suala la mafunzo ya vitendo kazini kwa wahitimu litawekwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa waajiri wote nchini kuendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa programu ya mafunzo kazini kwa wahitimu kwa kutoa fursa kwa vijana wahitimu kujifunza katika maeneo yao ya kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab Katimba.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, pia nashukuru kwa kuchukua mapendekezo haya na kuona umuhimu wa kutunga sera hii ya mafunzo kwa vitendo kazini kwa wahitimu.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza, sisi tunafahamu kwamba ili kijana/mhitimu awe na uzoefu, uzoefu hujengwa kwa kuanza. Sasa pamoja na kwamba Serikali itatunga sera hii kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo

kazini kwa wahitimu, lakini haioni haja kwamba kuna kazi zingine ambazo hazihitaji kuwa na *experience*, kwa sababu ukiangalia leo hii ajira zilizotolewa utakuta kuna kigezo, *two years experience, three years experience, five years experience*. Sasa hawa vijana wanaohitimu, wataanza lini kupata huo uzoefu kama kila kazi inayotolewa inahitaji wawe na uzoefu?

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na kwamba Serikali itatunga sera hii ambayo itaweza kusaidia kuondoa hilo umbwe kati ya elimu waliyopata wahitimu pamoja na mahitaji ya soko la ajira lakini Serikali haioni haja kwamba kuna kazi zingine ambazo hazihitaji huo uzoefu na vijana wawewe kupata fursa ya kuajiriwa ili na wenyewe wawewe kujikwamua na changamoto ya kukosa ajira? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri, ukizingatia *gallery* hizi zimejaa vijana wa vyuo vikuu wanaotegemea sana majibu yako mara wakihitimu masomo yao. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Zainab Katimba kwa namna ambavyo anawapigania vijana wa Taifa hili la Tanzania na vile alivyokuwa mstari wa mbele kuhakikisha maslahi ya vijana yanalindwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na changamoto kubwa katika masuala ya uhitaji wa uzoefu katika nafasi za kazi ambazo zimeombwa na kama itakumbukwa, wakati wa kampeni mwaka 2015 Mheshimiwa Rais pia aliwahi kulisema hili juu ya kigezo hiki cha uzoefu. Sisi kama Wizara tukaona kwa sababu asilimia kubwa ya vijana wanaotoka katika Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu wamekuwa wakipata taabu sana kwenda kujifunza kivitendo na wengi wao ni mashahidi huwa wanatembea na ile barua ya *to whom it may concern* na wengine mpaka kumaliza soli za viatu bila kupata eneo la kwenda kufanya kazi. Kama Serikali tukaona sehemu ya kwanza ya kuanzia ni

kuhakikisha tunatengeneza mwongozo huu na mwongozo huu tumefanya kati ya Serikali, waajiri na Vyama vya Wafanyakazi ili tutoe nafasi kwa vijana wale wahitimu wa Vyuo Vikuu wakimaliza masomo yao na tumeshazungumza na haya makampuni yatoa nafasi, tunawapeleka moja kwa moja katika makampuni na taasisi mbalimbali kwenda kujifunza kuanzia miezi sita mpaka mwaka mmoja. Lengo letu ni kuondokana na kikwazo cha kigezo cha *experience* ili akitoka pale akienda sehemu awe ana *reference*.

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo la kwanza ambalo tumelianzia, naamini kabisa kupitia mpango huu utawasaidia sana vijana wasomi wa nchi yetu ambao wamekuwa wakipata tabu na kikwazo cha uzoefu. Kwa hiyo, hivi sasa atapata nafasi ya kujifunza katika kampuni kwa muda huo wa mwaka mmoja na baadaye tutampatia cheti cha kumtambua ili iwe kama *reference* yake katika sehemu inayofuata. Tunafahamu ni tatizo kubwa, ni changamoto kubwa lakini kama Serikali tumeona tuanzie hapa kwenda mbele na jinsi Waheshimiwa Wabunge watakavyotushauri tutaona namna nzuri ya kuboresha mpango huu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ALEMAVU: Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza majibu machache katika swali hili na hasa nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo amekwisha kuyasema.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuona tatizo hilo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema tumeshatengeneza hiyo miongozo. Tunafikiri sasa kazi yetu kubwa ambayo tumeanza kuifanya ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuji-link sisi Ofisi ya Waziri Mkuu na miongozo tuliyonayo na wenzetu wa Wizara ya Elimu, lakini kupitia vyuo vikuu vyote kuhakikisha kwamba tunatambua mahitaji na tunawasaidia hawa vijana kuwaandaa vizuri, ili awingie kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana pia ndani ya Serikali na ndio maana mmeona hata ajira na matangazo ya ajira yanayotolewa sasa hivi, ajira hizo zinazotolewa sasahivi kwa kweli, kimsingi wengi wanaoajiriwa kwenye ajira hizi ni wale ambao ni *fresh* kutoka kwenye vyuo vyetu vikuu na taasisi nyingine ambazo zinatengeneza ujuzi. Wakati mwingine tunaweza kuwa tunataka ajira katika *position* fulani ambazo zina matakwa rasmi. Kwa mfano, Mkurugenzi labda wa kitu fulani kwa matakwa fulani kwa hiyo, huko ni lazima tuone sasa wale walioenda *internship*, lakini vilevile wale ambao wana uzoefu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie vijana wetu kwa kweli, baada ya kuona hiyo *gap* ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumeifanyia kazi vizuri sana, sasa hivi waajiri na Serikali kwa pamoja na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi tumeanza kulifanyia kazi vizuri sana eneo hilo. Na tunawaondoa hofu vijana wetu kwa kweli sasa tunataka kuwapa *assurance* ya ajira bila kupata vikwazo vyovyote katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Nchi kwa majibu ya nyongeza, vijana wasomi ziko kazi nyingine hazihitaji uzoefu, mnagombea Udiwani, mnagombea Ubunge. Nawatangazia vita Waheshimiwa hapa. (*Kicheko*)

Tunahamia TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini tafadhali.

Na. 268

Kujenga kwa Lami Barabara ya Urefu wa Kilometra 10

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL aliuliza:-

Mheshimiwa Rais katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 aliahidi kujenga kilometra 10 za barabara ya lami katika Manispaa ya Moshi.

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kusaidia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kujenga mitaro katika barabara zake za lami ili kuzifanya zidumu muda mrefu?

SPIKA: Majibu ya Serikali, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napensa kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, barabara zenyе urefu wa kilometa 16.57 zimejengwa katika Manispaa ya Moshi kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2018 ambapo kati ya hizo kilometa 6.06 zimejengwa kupitia fedha za Mfuko wa Barabara kwa gharama ya shilingi 2,076,497,094 na kilometa 10.51 zimejengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kuimarisha Miji 18 (*ULGSP*) kwa gharama ya shilingi 8,384,872,640.87. Vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri inaendelea na ujenzi wa barabara zenyе urefu wa kilometa 2.79 kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara unaotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi 1,178,201,860.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa Kuimarisha Miji 18 (*ULGSP*) katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2018 Serikali imejenga mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 11.57 kwa gharama ya shilingi 1,833,520,330. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kujenga mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 9.47 na mradi huu utagharimu jumla ya shilingi 1,612,952,130 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, ujenzi huu upo katika hatua za awali.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini swali la nyongeza.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuititia fedha ya Mfuko wa Barabara na fedha ya Benki ya Dunia mtandao wa barabara ya lami katika Manispaa ya Moshi unaridhisha kwa kiwango fulani, lakini kwa kuwa fedha hizi hazina mahusiano ya moja kwa moja na ahadi ya Rais ya kilometra 10 aliyoitoa siku tano kabla ya kufunga kampeni zake mwaka 2015. Je, Waziri haoni kwamba, kuna sababu ya kumkumbusha Rais huenda akawa na nafasi ya kukumbuka ile ahadi yake ya kilometra 10 katika Manispaa ya Moshi?

Mheshimiwa Spika, Iakini la pili, tangu *TARURA* imeanza kazi Manispaa ya Moshi *speed* yake ya uwajibikaji haijaenda kwenye kasi ile ambayo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilikuwa inafanya wakati inasimamia barabara zake.

Je, Waziri haoni kwamba, kuna haja ya kuisukuma *TARURA* ili iweze kuongeza kasi ili kuhakikisha kwamba, barabara ambazo zimeharibiwa sana na mvua kipindi hiki cha mvua zinakarabatiwa, ili ziwe katika hali nzuri kama ilivyokuwa wakati Halmashauri ya Manispaa ya Moshi inasimamia yenye?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Josephat Kandege tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza anasema kwamba utekelezaji wa hizi barabara hauna uhusiano wa moja kwa moja na ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tu akatambua kwamba fedha zote ambazo zimefanya kazi ya ujenzi wa barabara katika Mji wa Moshi ni utekelezaji na mwenye fedha ni Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe. Najua ana kiu,

angependa barabara nyingi zaidi zijengwe, lakini haiondoi ukweli kwamba tumefanya kazi kubwa sana katika ujenzi wa barabara katika Manispaa ya Moshi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swalii lake la pili, anasema haridhishwi na kasi ya chombo hiki ambacho tumeanzisha, *TARURA*, ukilinganisha na hapo awali jinsi ambavyo wao halmashauri walikuwa wakifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie, chombo hiki ni baada ya kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengi ambaao tulikuwa tunapenda barabara zetu zichukuliwe na *TANROADS, TARURA* katika maeneo mengi inafanya kazi vizuri na Moshi naamini nao watafanya kazi vizuri. Hebu tukilee na tuhakikishe kwamba tunakisukuma tunakipa nguvu kifanye kazi iliyotarajiwa. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Lubeleje, swalii la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Halmashauri tano za Mkoa wa Dodoma zilipata fedha za kujenga barabara za mijini, lakini halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa hatukupata na nimezungumza na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kongwa kwamba Mpwapwa na Kongwa hatukupata barabara za kujenga mijini na ilikuwa ni ahadi ya Waziri wa TAMISEMI, tarehe 30 Desemba, Mheshimiwa Jafo.

Naomba maelezo ya Waziri kwa nini, Kongwa na Mpwapwa hatukupata hizi hela katika hiyo bajeti? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, swalii hili unatakiwa ulijibu vizuri. Kana kwamba haitoshi hata bajeti ya mwaka huu Kongwa na Mpwapwa hazina hata robo kilometra ya lami, mnamuonea kweli Spika ninyi. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakkisha kwamba maeneo yale yote na hasa kwa sababu na ye ye amesema kwamba ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimhakikishie dhamira ya dhati ipo, lakini ni ukweli usiopingika kwamba miji mingine yote kwa Mkoa wa Dodoma imepata. Maana yake katika hatua inayofuata lazima tuhakikishe kwamba na maeneo hayo mawili ikiwepo eneo la kwako Mheshimiwa Spika yanatiliwa mkazo, ili barabara zijengwe kwa kiwango cha lami na kwa Mheshimiwa Lubeleje. Naomba nilichukue kwa mikono miwili kwa dhati kabisa kuhakkisha kwamba, na hasa kwa kuanzia kwa Mheshimiwa Spika hatukusahau hata kidogo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, swali lako tafadhalli uliza. Bado tuko TAMISEMI

Na. 269

Tume ya Huduma kwa Walimu

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Serikali imeanzisha Tume ya Huduma kwa Walimu (*TSC*) kwa lengo la kutatua matatizo ya walimu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha Tume hiyo ili ifanye kazi kikamilifu kama ilivyokusudiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*) imeanzishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Walimu Namba 25

ya mwaka 2015 na kuanza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 1Julai, 2016 kupitia Ofisi za Tume zilizopo katika Wilaya 139 za kiutawala ambazo zinasimamiwa na Makatibu Wasaidizi wa Wilaya. Majukumu ya tume yameainishwa katika kifungu cha 5 cha Sheria hiyo ambayo ni pamoja na kusimamia mikataba ya ajira za walimu, kuwapandisha madaraja na kuchukua hatua za kinidhamu, ikiwemo kusikiliza rufaa kutoka ngazi za chini, kuwatambua na kutunza kumbukumbu za walimu wa shule za msingi na sekondari, kusimamia mafunzo ya walimu walio kazini, kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu utumishi wa walimu na kutathmini hali ya utumishi wa walimu na kusimamia maadili ya utumishi wa walimu.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa pili tu wa uhai wa Tume hiyo ambayo bado ni changa. Mikakati mahususi ya Serikali ili kuimarisha zaidi Tume hiyo ni ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuipatia fedha ili iweze kutimiza majukumu yake ipasavyo. Mfano katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bunge limeiidhinishia Tume ya Utumishi wa Walimu shilingi 12,515,260,520 kati ya hizo shilingi 7,893,115,025 ni za mshahara na shilingi 4,622,145,495 ni za matumizi mengineyo, ili Tume ipate vitendea kazi kama magari, samani za ofisi na pia kugharamia vikao vya mashauri ya nidhamu na vifaa.

(ii) Kuipatia ofisi na watumishi wa kudumu, mfano, hadi sasa inao Makatibu Wasaidizi wa Wilaya 138 ambao wameshajengewa uwezo na mwaka ujao 2018/2019 wataajiriwa watumishi 45 wapya na wengine 145 watahamishiwa kwenye Tume kama uhamisho wa kawaida. Uimarishaji wa Tume hiyo utaendelea kufanyika ndani ya wigo wa sheria iliyoanzisha Tume hiyo.

SPIKA: Mama Margaret Sitta, swali la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuimarisha Tume ya Huduma kwa Walimu (TSC), kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili walimu na matatizo mengi.

Swali la kwanza, ni kwamba, je, Serikali iko tayari kuwatuma wataalam kwa mfano Kenya kwenda kujifunza jinsi ambavyo wenzetu wameweza kuimarisha chombo kama hiki cha *TSC* ili kifanikishe katika utoaji wa huduma kwa walimu kwa kuwa nao Kenya walikuja kujifunza kutoka kwetu, wao wakaenda wakaimarisha wakafanikisha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali iko tayari baada ya kuwatuma wataalam Kenya kujifunza jinsi ambavyo wamefanikisha wenzetu, kurudi huku na wahakikishe kwamba, wanachukua hatua za kuimarisha, ili kifanikishe katika kutoa huduma kwa walimu?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Kakunda tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nieleze kidogo kuhusu Mheshimiwa Mama Margaret Sitta. Mheshimiwa Sitta ni hazina kubwa ya kumbukumbu na uzoefu katika sekta ya elimu nchini kama Mwalimu, Afisa Elimu, Kiongozi wa Chama cha Walimu, Waziri na Mbunge. Kwa hiyo, kwa kweli, amekuwa msaada mkubwa sana kwetu Serikali katika kutoa mawazo ya kuboresha zaidi sekta ya elimu na sisi tutaendelea kufaidika nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo, kwa pamoja:-

Mheshimiwa Spika, kwamba ushauri wake wa kwenda kujifunza katika nchi ya Kenya tumeupokea na tutaufanyia kazi. Mapendekezo na ushauri wake katika suala la pili nao tunaupokea na tutaufanyia kazi, ili kuboresha zaidi Tume ya Utumishi wa Walimu. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora swali la Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena

Na. 270

Kuwatumia Wataalam Wastaafu Nchini Kutoa Ushauri

MHE. PROSPER J. MBENA aliuliza:-

Nchi nyingi duniani ikiwemo Japan, Uholanzi na Marekani hutumia wataalam wastaafu kwenye sekta mbalimbali za uchumi katika shughuli mbalimbali za kutoa ushauri ndani na nje ya nchi zao. Wataalam hao (*volunteers*) wanatoa mchango mkubwa kwenye kushauri.

(a) Je, ni lini nchi yetu italga utaratibu huo mzuri wa kuwatumia wataalam wake wastaafu ipasavyo badala ya kuwaacha tu mitaani?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kumbukumbu ya taarifa ya wataalam wastaafu wake (*directory*) kwa kila mmoja kwenye fani yake (*profession*) ili kuweza kuwatumia wataalam wastaafu hao pale ushauri wao utakapohitajika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Angella Kairuki tafadhali.

WAZIRI WA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu wa kuwatumia wataalam wastaafu kwa kuwapatia mikataba

pale wanapohitajika. Matumizi ya wataalam hao yamefanunuliwa katika aya ya 12.2 ya Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 1998, pamoja na Kanuni ya D. 28 ya Kanuni za Kudumu (*Standing Orders*) katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009. Miongozo hii inaelekeza kwamba endapo utaalam wa mtumishi unahitajika sana Serikali inawajibika kumuomba mtumishi kuendelea na kufanya kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuanzisha kanzidata ya wataalam wastaafu ili kuweza kuwatumia pale watakapohitajika.

SPIKA: Mheshimiwa Mbena, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Chakula Duniani (*FAO*) ni moja kati ya wafadhili wa miradi hii ya kilimo kwenye nchi yetu na wanao mkataba maalum kwa wataalam wao wanaostaifu kuendelea kufanya kazi kati ya umri wa miaka 60 mpaka 70 na labda ni-*declare interest* tu kwamba mimi ni mstaifu, lakini nauliza swali hili kwa maslahi mapana ya nchi.

Je, kwa nini Serikali mpaka sasa haijasaini mkataba wa utumiaji wa wataalam (*national experts*) na Shirika la *FAO* wakati kuna nchi zaidi ya 67 wanachama wa *FAO* wameshasaini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo mahususi fupi, karibu sana Mheshimiwa Waziri Angella Kairuki, tafadhali.

WAZIRI WA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya Serikali nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha utumishi wetu wa umma, lakini

zaidi kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia maslahi na mustakabali wa wastaafu wetu. Nipende tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwa takwimu za mwaka 1995 mwezi Machi, ndipo ambapo Tanzania ilikuwa bado haijaweza kusaini mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 1998 Tanzania ilikuwa imeshasaini na kwa sasa hivi tunayo *Technical Cooperation among Developing Countries* pamoja na *Countries in Transition* na ninaamini Serikali itawezekunufaika, lakini pia na wataalam wetu katika sekta mbalimbali, lakini nimshukuru kwa kuleta hoja hii na tutaendelea pia, kufuatilia na mikataba mingine ya kimataifa ili watu wetu waweze kunufaika.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando.

Na. 271

Kuboresha Miundombinu ya Usafiri wa Anga Nchini

MHE. OTHMAN OMAR HAJI aliuliza:-

Pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) kuwa na uchakavu wa mitambo ya kuongezea ndege na miundombinu duni ya usafiri wa anga nchini, *TCAA* imechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Shirika la Usafiri wa Anga Duniani kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 na hivyo kuwa mwakilishi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Je, kupitia nafasi hii ya kipekee, Serikali kupitia *TCAA* ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya usafiri wa Anga hapa nchini, ili iweze kulingana na ile ya nchi nyingine za *SADC*?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*) inaendelea kuboresha mitambo ya kuongozea ndege hapa nchini. Tayari mchakato wa usimikaji wa rada nne za kuongozea ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, Uwanja wa Ndege wa Mwanza na Songwe unaendelea. Aidha, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 kuanzia tarehe 9 Novemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo *TCAA* imekamilisha mradi wa usimikaji wa mtambo Mashariki upande wa nchi yetu unaofanya kazi ya kutambua na kuongoza ndege zinazopita katika anga la juu (*Automatic Dependent Surveillance Broadcast*) na mtambo wa mawasiliano ya sauti katika kituo chetu cha kuongozea ndege cha *Julius Kambarage Nyerere International Airport* na nchi nzima kwa ujumla na hivyo kuboresha usalama katika anga la Tanzania. Aidha, *TCAA* wamekamilisha usimikaji wa mitambo ya mawasiliano kwa njia ya redio baina ya waongoza ndege na marubani (*VHF Radios*) and area cover relays na hivyo kuwa na uhakika wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa na *TCAA* kupitia Serikali katika kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga nchini ni pamoja na kukarabati mnara wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Pemba na kuendelea na mchakato wa ununuzi na usimikaji wa mtambo wa kuwezesha ndege kutua kwa usalama katika kituo cha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zote zinazochukuliwa na Serikali zinalenga katika kulifanya anga la Tanzania kuwa salama zaidi na hivyo kuvutia mashirika mengi ya ndege ya kigeni kuja hapa nchini kwetu. Aidha, Tanzania kupitia nafasi

hii ya ujumbe wa Baraza la Washirika la Usafiri wa Anga Duniani kwa kuziwakilisha nchi za Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) itaendelea kuhamasisha mashirika ya ndege ya kigeni kuja nchini kwa kupitia mikutano mbalimbali ya kimataifa ambayo mamlaka uhudhuria na hivyo kuongeza mapato ya mamlaka na kwa nchi kwa ujumla kutokana na miundombinu ya usafiri wa anga nchini kuendelea kuboreshwa.

SPIKA: Mheshimiwa Othman Haji swali la nyongeza kama lipo.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba katika majibu yake wajipange sana katika mikakati yao kwa sababu Shirika la Anga la Kenya bado wanatufilisi kwa kuchukua mapato ya nchi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2015/2016 *TCAA* iliingia mkataba na Kampuni ya *COMSOFT GMBH* ya Ujeruman. Kwa kuweka mitambo ya kisasa ya kuongozea ndege na kufuatilia safari za ndege yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4. Kwa sababu mkandarasi huyu hakuweka dhamana katika kazi, yake mnamo mwaka 2014/2015 mzabuni alitangaza kafilisika.

Kwa kuwa shirika liko kimya kuhusu suala hili Mheshimiwa Waziri naomba kukuuliza, ni kwa kiwango gani shirika limeweza kuokoa fedha hii ya walipa kodi zilizopotea? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, Mheshimiwa Waziri, Mamlaka ilipokutana na Kamati ya *P/C* ilikuwa na kilio kwamba wana ukosefu wa wataalam wenye sifa katika usafiri wa anga. Katika hotuba yako uliyoiwakilisha muda mchache tu mwaka huu ulisema kwamba *Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam kinatoa wataalam wa mafunzo tofauti na* wenye viwango vya kimataifa wa ndani na nje ya Tanzania. Je, Mheshimiwa Waziri wataalam hawa...

SPIKA: Mheshimiwa swali kwa kifupi tafadhali.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: ...wataalam hawa wanaomaliza chuo unawapeleka wapi?

SPIKA: Majibu mafupi Naibu Waziri, Mheshimiwa Atashasta Nditiye tafadhali.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimuhakikishie tu kwamba kwa ufungaji wa rada nne hizo ambazo Mheshimiwa Rais amezindua tarehe 2 Aprili, tuna hakika anga letu lote tutalimiliki sisi kwa maana ya kuhakikisha usalama wake. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi kwamba nchi jirani zitafanya hicho kitu badala yetu. Lakini nikijibu swali lake la kwanza nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha iliyolipwa na Serikali hajapotea bado ipo na sasa hivi kuna taratibu zinafanyika kuhakikisha kwamba pesa yetu inarudishwa kwa wananchi walipa kodi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu ukosefu wa wataalam nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna wataalam 40 ambao wamepelekwa kusoma ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaiendesha mitambo yetu hii ya rada ambayo inafungwa kwa ufanisi wa kutosha.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Magolyo tafadhali.

Na. 272

Ujenzi wa Barabara ya Kahama – Busisi na Kahama – Mwanangwa

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Wakati akihutubia mkutano wa kampeni Kharumwa Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Nyang'hwale

kwamba barabara ya Kahama – Busangi – Kharumwa – Buyagu – Busisi itajengwa kwa kiwango cha lami; na llani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 imesema barabara ya Kahama – Bulige – Solwa – Mwanangwa itafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Je, kuna maandalizi gani yanayoendelea ya kutekeleza ahadi hiyo ya Rais na ile ya llani ya Chama cha Mapinduzi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza nianze kwa kuwatakia ndugu zangu waislam wote nchini mfungo mwema katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kahama – Busangi – Kharumwa – Buyagu hadi Busisi yenye urefu kilometa 156.68 ni barabara ya mkoa inayounganisha mikoa mitatu ya Shinyanga, Geita na Mwanza. Aidha, barabara ya Kahama – Bulige – Solwa – Mwanangwa yenye urefu wa kilometa 150 ni barabara ya mkoa inayounganisha mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Barabara hizi ni mionganoni mwa barabara ambazo Serikali imepanga kuzijenga kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea kutekeleza ahadi za viongozi wakuu kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, barabara ya Kahama – Busangi – Kharumwa – Buyagu – Busisi itatekelezwa kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kahama – Bulige – Solwa – Mwanangwa (kilometra 150) ni kweli ipo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika, kama ilani inavyoelekeza. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Mheshimiwa Maige swal la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Chifu Kwandlkwa, Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo amerasimisha hapa kwa sababu tunayaongea sana haya hata jana tulikuwa tunaongea ofisini kwake. Lakini nilipenda tu angalau anisaidie kurasimisha pia mengine ambayo tuliyaongea lakini hayako kwenye jibu hili la msingi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, barabara ya kutoka Kahama kwenda Mwanza kuititia Bulige imematika kabisa kile kipande cha kutoka Bulige kwenda Mwakitalyo kwa sababu ya hizi mvua zinazoendelea, lakini vilevile hata ile ya kupita Busangi - Kharumwa hadi Busisi na yenyewe imeharibika kwa kiasi kwamba magari madogo hayawezhi kabisa kupita. Wakati mipango hiyo ya kujenga kwa kiwango cha lami ikiendelea ni hatua gani Serikali inafanya kwa dharura ili kuzitengeneza barabara hizi ziweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, swal la pili, Serikali ilishaahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kahama kuititia Segese – Mgodi wa Bulyanhulu hadi Geita kwa kiwango cha lami. Kwa miaka miwili mfululizo mwaka wa fedha uliopita na huu mwaka tulionao sasa hivi, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Nilitaka tu Mheshimiwa Naibu Waziri kama ulivyonithibitishia

mimi tulivyokuwa wenyewe, wathibitishie wananchi na watanzania ni lini hasa sasa ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Kahama - Geita utaanza. (*Makof*)

SPIKA: Jibu la swali hilo fupi ni lini ujenzi utaanza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza pongezi alizozitoa nazipokea. Lakini nitakuwa mchoyo kama sitakushukuru wewe binafsi wakati wa mjadala wa Bajeti ya Maji ulilisemea sana Jimbo la Ushetu, kwa hiyo nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nimjibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nakupongeza sana kwa kufuatilia barabara hizi ambazo zinaunganisha Mji wa Kahama ikiwepo hii barabara muhimu uliyoisema inayotoka Mji wa Kahama ikipitia maeneo ya Ntobo, maeneo ya Segese ikipitia pia katika Jimbo la Mheshimiwa Bukwimba ikielekea kule Geita na wewe mwenyewe unafahamu kwamba tumeanza ujenzi wa barabara hii kiwango cha lami.

Kwa hiyo, niwathibitishie tu wananchi wote maeneo hayo kwamba ujenzi umeanza ila juhudhi zitaendelea kufanyika kuweka fedha za kutosha ili barabara muhimu hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, niwape pole wananchi kote nchini kwamba tumejapata mvua nyangi na Mheshimiwa Ezekiel unajua kwamba barabara hii unayoitaja inayopita maeneo haya ya Mwakitalyo kwenda Mwanangwa kumekuwa na shida kubwa kwamba barabara zimekatika lakini bado pia kuna wananchi ambao nyumba zao zilidondoshwa kutokana na kuwa na mvua nyangi.

Mheshimiwa Spika, sisi upande wa Serikali tumejipanga kwa hatua ya kwanza kwamba kwanza tunayo bajeti kwa ajili ya kutibu *emergency* kama hizi. Tutatumia fursa hiyo, lakini pia tunafanya uratibu maeneo yote nchini lakini pia ninazo taarifa kuwa Mkoa wa Shinyanga kwamba

Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mwanza amefanya survey kwenye barabara hii na kutambua mahitaji muhimu ya maboresho katika barabara hii. Kwa hiyo, nikuombe tu uvute subira na niwatoe hofu wananchi kwamba barabara hii tunaenda kuifanya marekebisho na niwapongeze kwa kweli Mameneja wa *TANROADS* mikoa yote kwa kazi nzuri ya uratibu wanayoendelea kuifanya muda huu ambao tuko kwenye shida. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa nawaona lakini tuvumiliane, dakika zimebaki chache na bado tuna maswali matatu hivi. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi. Huku upande wa CHADEMA sioni nihamie CCM. Nimekuona Mheshimiwa.

Na. 273

Kiwanda cha Kubangua Korosho

MHE. LATHIFAH H. CHANDE aliuliza:-

Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Mtama (*Cashewnut Factory*) kilichopo katika Jimbo la Mtama kilikuwa chini ya Bodi ya Korosho na kiliuzwa kinyemela kwa Kampuni ya *Lindi Farmers* ambayo ilikodishwa kwa kampuni ya Kichina ya *Sunshine Industries Limited*, kampuni ambayo inawalipa wafanyakazi ujira wa shilingi 70 hadi 80 kwa kubangua kilo moja ya korosho.

(a) Je, Serikali ina taarifa ya kukodishwa kwa kiwanda hiki?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani juu ya mazingira magumu ya wafanyakazi ambao hawana mikataba ya kazi katika kiwanda hiki ambacho kinamilikiwa na wageni?

SPIKA: Swali hilo la Mheshimiwa Lathifah, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda, Biashara na Uwekezaji, *Engineer Stella Manyanya* majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA
UWEKEZAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Mtama kilibinafsishwa kwa kuuza hisa asilimia 100 kwa Kampuni ya *Lindi Farmers Association* ambayo inakimiliki. Kufuatia umiliki huo, kiwanda hicho kilikodishwa kwa makubaliano maalum kwa Kampuni ya *Sunshine* ili iweze kukiendesha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa kwamba Kampuni ya *Sunshine Industrial Company Limited* inaendesha kiwanda hicho kwa kubangua korosho kwa mkataba wa miaka mitano kuanzia mwaka 2013 hadi 2018 ambapo unahuishisha kujenga, kuendesha na kuhamisha. Baada ya mkataba kumalizika mashine na mitambo vitakuwa mali ya *Lindi Farmers Association*. Uwekezaji wa zaidi ya shilingi bilioni moja umefanyika tangu mkataba huo wenye gharama ya dola 100,000 kwa mwaka uliposainiwa.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuona viwanda vinafanya kazi na kuleta manufaa kwa Watanzania ikiwemo kutoa ajira, kulipa kodi na kuongeza thamani ya malighafi. Hata hivyo, msimu wa mwisho mwaka huu kiwanda hicho hakikupata korosho za kutosha kutokana na ushindani wa bei ya korosho ghafi na hivyo kupelekea wanunuizi kugombania korosho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama wa wafanyakazi viwandani, Serikali inaendelea kutoa wito kwa waajiri wote kuzingatia sheria za usalama kazini. Aidha, nitumie fursa hii kuzihimiza mamlaka zinazohusika na ukaguzi wa usalama kazini kusimamia kwa karibu sheria hizo. Pamoja na hatua hizo, waajiri wote wanapaswa kuijunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Fund – WCF*)

ulioanzishwa hivi karibuni na sheria yake kuitishwa na Bunge lako tukufu. Hii itawawezesha kunufaika pale wanapoumia kazini kutokana na majanga mbalimbali. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu tutaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sheria hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Lathifah swali la nyongeza tafadhali.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Spika, ahsante, je, masharti ya mauzo hayo yaliruhusu ukodishwaji?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kutokana na kwamba malengo ya Serikali ilikuwa ni kuweza kubangua tani 200,000 za korosho na hii ikapelekea kwamba hata Bodi ya Korosho pamoja na mfuko wa kuendeleza zao hili la korosho ilitenga pesa kwa ajili ya kujenga viwanda katika Mkoa wa Pwani, Ruvuma pamoja na Mtwara. Sasa wakati tunasubiria hivyo viwanda viweze kujengwa kwa nini Serikali isifufue viwanda vilivyoko ili kuweza kutimiza hayo malengo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa *EngineerStella Manyanya* tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali ina taarifa juu ya huo ukodishaji kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi.

Katika swali lake la pili nipende tu kuzidi kumuhakikishia ni kwamba kama amekuwa akifuatilia hata kuititia bajeti yetu, lakini pia ziara mbalimbali tunazofanya, Serikali imeamua kuona kwamba viwanda vyote vilivybinafsishwa vinafanya kazi yake kama iliyokusudiwa, lakini pia kuhamasisha viwanda vingine viweze kufanya kazi hiyo ikizingatiwa kwamba korosho ni zao kubwa na ni zao ambalo linapendwa duniani na hivyo si vyema tu kusafirisha ikiwa ghafi ni bora kuiongezea thamani ili faida yake iwe ni kubwa zaidi na kuleta tija zaidi katika nchi.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kelele nydingi. Mheshimiwa Salma Kikwete nimekuona tafadhali.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa viwanda ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu, lengo la viwanda ni kuleta tija kwa Taifa na wananchi wake kwa ujumla ili waweze kunufaika.

Je, Serikali haioni kuwa sasa hivi ni wakati muafaka wa kwenda kutembelea kiwanda hicho kule Mtama?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Stella Manyanya* tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa viwanda ni muhimu sana na viwanda hivi vitakapofanya kazi vizuri vitawezza kuwa na tija kubwa katika Taifa letu. Swali lake, je, hatuoni sababu ya kwenda kutembelea huko.

Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka kwamba mwezi wa kwanza nilikuwa pia kwenye mzunguko katika Mkoa wa Lindi kufuatilia Kiwanda cha Wanga ambacho kinajengwa katika Jimbo hili la Mtama na kuweza kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zinakabili na hivi sasa hivi wanafanya vizuri. Kwa hiyo, vilevile katika masuala haya ya viwanda vya korosho tutafanya hivyo ili kuona kwamba viwanda hivyo vinaleta tija kwa ajili ya nchi yetu.

SPIKA: Mheshimiwa swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kutoka kwenye swali namba 273 la msingi ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Lathifah Chande.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa nia ya Serikali ya kutaka kuwa na viwanda kwenye maeneo mengi na kwamba mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi kimkakati kabisa miaka ya 1970 tayari tulikuwa na viwanda vingi tu vya korosho

Masasi ukienda Lindi, ukienda Nachingwea na maeneo mengi tu.

Sasa swalii, mara nyingi tumekuwa tukiwasiliana na Waziri anatueleza kwamba kuna kesi mbalimbali mahakamani ambazo zinasababisha viwanda vile visiendelezwe, lakini wamiliki waliouziwa vile viwanda sasa hivi wanavitumia kama maghala. Wakati Serikali inasubiri hizi kesi ziishe Mahakamani wengine wanapata faida kwenye maeneo hayo hayo.

Sasa swalii langu, kwa nini wasiwasimamishe watu wale kutumia viwanda hivi kama maghala kwa sababu wanajipatia pesa na Serikali haipati faida yoyote?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo la Mheshimiwa Cecil Mwambe. Mheshimiwa Nailbu Waziri *Engineer Stella Manyanya* tafadhali, kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, kimsingi nchi yetu inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa sheria lakini vilevile tusingependa kuona sheria zikatumike kama kichaka cha kuwanufaisha watu wachache. Tumeshfanya hivyo katika mashamba ya mpira Kihui ambapo mtu alikuwa na kesi, akasingizia kesi ye ye akawa anaendelea kuvuna, tukafanya jitihada ameondoka. Kwa hiyo, hata hayo tutayafulilia na ushauri wako tutauzingatia.

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea, lakini kabla ya kuendelea nimefanya utafiti wangu leo watu wengi wamependeza sana kwa kuvaa kanzu na kofia, hongereni sana. Tukumbuke tu kanuni kwamba tunapovaa lazima tuvae inavyotakiwa vilevile inavyovaliwa kule Pwani na miguuni sio kuvaa kiatu cha kamba, hapana unavaa kobazi. (*Makofi*)

Lakini upande wa akina mama pia *hijab* leo zimekubali lakini katika *hijab*, *hijab* namba moja leo hii ni ya Naibu wangu Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika hebu simama kidogo hapo. Ahsante sana, hiyo

inaonesha Utanzania wetu jinsi ambavyo sisi ni wamoja.
(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub kwa niaba yake
Mheshimiwa Ally Keissy uliza swali. *(Kicheko)*

Na. 274

Uhaba wa Sukari – Tanzania Bara

MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y MHE. JAKU HASHIM AYOUB) aliuliza:-

Pamoja na kuwepo viwanda vingi nya sukari hapa nchini bado kuwekuwa na uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo kususan kwa upande wa kilo 50 ni shilingi 65,000 kwa upande wa Zanzibar ambako kuna kiwanda kimoja tu cha sukari, lakini kwa Tanzania Bara mfuko huo wa kilo 50 ni shilingi 120,000:-

(a) Je, kuna tatizo gani linalofanya sukari iuzwe kwa bei juu kiasi hicho kwa upande wa Tanzania Bara?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuweza kuwapatia wananchi unafuu katika upatikanaji wa bidhaa hiyo?

(c) Kwa upande wa Zanzibar katika kipindi ambacho matumizi ya sukari kwa wananchi yanaongezeka mfano, mwezi wa Ramadhan Serikali inahusisha ushuru wa kuingiza sukari nchini, je, kwa nini Serikali ya Muungano isizingatie utaratibu huu mzuri ili kuleta unafuu kwa Tanzania Bara?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Zanzibar lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa maafisa masoko katika masoko ya Dar es salaam na Zanzibar unaonyesha kuwa bei ya sukari kwa gunia la kilo 50 ni shilingi 101,000 hadi 105,000 kwa Dar es salaam na shilingi 71,000 hadi 77,000 kwa uzito huo huo upande wa Zanzibar. Mapitio ya bei hizo na kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza kwenye swali hili kipengele (c) tofauti ya bei katika eneo la Dar es salaam na Zanzibar kwa kiasi kikubwa inatokana na utozaji wa ushuru na kodi. Inaonekana dhahiri kuwa kiasi cha kodi inachotozwa kwenye gharama ya mfuko wa kilo 50 Zanzibar ni kidogo wakati Dar es Salaam ushuru na kodi ni asilimia 25 na 18 vyote kwa pamoja.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya sukari nchini kwa wastani vinazalisha tani 320,000 kwa mwaka wakati mahitaji ya sukari ya mezani ni tani 455,000. Chini ya utaratibu maalum Serikali huagiza upungufu katika uzalishaji (*gap sugar*) ili kutosheleza mahitaji ya soko. Katika kipindi hiki cha Februari – Mei ambapo viwanda vyetu vimefungwa kwa ajili ya matengenezo na kupisha msimu wa mvua za masika kiasi cha tani 135,000 kimeagizwa kuziba pengo na sehemu kubwa ya shehena hiyo imeshawasili nchini.

Aidha, chini ya utaratibu wa maalum wa kulinda na kuhamasisha viwanda vya sukari ni viwanda vya sukari nchini vinaruhusiwa kuagiza upungufu wa sukari. Utaratibu wa wenyewe viwanda unaambatana na masharti ya kupanua mashamba na viwanda vyao ili katika kipindi cha miaka mitatu tuwe na uzalishaji wa kutosha mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika sehemu (b) ya swali hili zimeagizwa tani 135,000 ili kuhakikisha kuwa tunakidhi mahitaji ya soko. Kulingana na sheria za kodi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, sukari inayoagizwa toka nje ya Jumuiya hutozwa ushuru kwa kiwango cha 100% na 18% ya gharama (*CIF*) ila kwa kulenga kuwapa nafuu walaji sukari hapo juu inatozwa kwa kiwango cha 25% na 18% ya gharama.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, asante sana. Kwanza nampa pole ndugu Jaku jana kwa kutolewa nje ya Baraza la Wawakilishi na Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, lini sasa utafanyika utafiti maalum wa uagizaji sukari upande wa Zanzibar ili kulinda Kiwanda cha Mahonda?

Mheshimiwa Spika, lini sasa Zanzibar itajiunga na Mfumo wa Kodi wa *TANSIS? (Makof)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, kimsingi Wizara yetu imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Waziri upande wa Zanzibar, kwa hiyo, katika suala hili la kufanya utafiti juu ya sukari Zanzibar ni suala muhimu sana ili kuona kwamba kunakuwa na sukari ambayo itawezesha hata kukifanya hata Kiwanda cha Mahonda kifanye kazi yake vizuri zaidi na kuwe na ile bei ambayo ni shindani. (*Makof*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, hajajibu swali la pilii.

SPIKA: Mtakumbuka swali hili lilikuwa ni mwendelezo tu wa lile swali ambalo tulisema lirudiwe wiki iliyipita, itoshe kusema hivyo lakini kwa kweli ukisoma maswali yaliyokuwa yameulizwa na majibu ni vitu viwili tofauti, lakini inatosha kwa leo tuvuke hapo twende na mambo mengine. (*Makof*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, la pili hajajibu.

Na. 275

Ulipaji wa Kodi Kupitia Njia ya Simu

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

TEHAMA imekuwa kichocheo cha maendeleo na hivyo kurahisisha ulipaji wa gharama (*bills*) mbalimbali kupitia miamala kwa njia ya simu. Mathalani, muda wa maongezi, ving'amuzi, umeme, kodi na laini mbalimbali.

Je, mlipaji aweke ushahidi wa aina gani katika kumbukumbu ngumu (*hard paper*) ili wakaguzi wa *TRA* waone au *TRA* itaridhika kwa kumbukumbu ya muamala?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 35(1)(2), cha Sheria ya Usimamizi wa kodi ya mwaka 2015, kila mlipa kodi au mtu ye yeyote anayetakiwa kulipa kodi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatakiwa kutunza kumbukumbu za miamala katika mfumo wa kumbukumbu ngumu au mfumo wa kielektroniki. Aidha, kifungu cha 35(3) kinamtaka mlipa kodi kutunza kumbukumbu zake kwa muda wa miaka mitano kuanzia tarehe ambayo muamala umefanya au kwa muda zaidi kulingana na matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Sheria ya Usimamizi wa Kodi kifungu cha 69(3)(b) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*The Value Added Tax Act, 2014*) kinamtaka mlipa kodi aliyesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika mfumo wa malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kuwa na risiti ya *EFD* au ankara ya kodi (*tax invoice*) wakati akiwasilisha taarifa zake za mwezi (*VAT return*).

SPIKA: Mheshimiwa Richard Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kanzidata zinatunzwa na hizi kampuni za simu na sio sisi wamiliki wa hizi kampuni na kwa kuwa inaweza ikatokea simu ikapotea au ikaibwa na kumbukumbu mtu asiwe nayo. Sasa je, Serikali iko tayari kupokea maelezo ambayo yatakuwa yameandikwa kwenye vocha ya malipo ambapo mfanyabiashara ameweeka tu ile *reference number*, je Serikali itakuwa tayari kuikubali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tulivyoanzisha mifumo ya *electronic devices* (*electronic signature device, electronic fiscal device* na *electronic tax register*) wafanyabiashara wakubwa (*large tax payers*) walipewa bure kwa maana ya kwamba waliweza ku-*claim* kutoka kwenye uandaaji wa *VAT return*. Sasa kwa mpango huo ambao ulifanyika kwa wafanyabiashara wakubwa, je, Serikali haioni haja sasa ikatoa hizi *EFD* bure kwa wafanyabiashara wadogo au ikaweka ruzuku ambapo itawawezesha...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa umeeleweka. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango tafadhali, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwenye majibu yangu ya msingi nimesema kifungu cha 35(3) kinamtaka mlipa kodi mwenyewe kutunza kumbukumbu zake kwa miaka mitano mfululizo. Kifungu hiki kinaweka utaratibu wa kwamba unapokuja kukaguliwa na watu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania wanakutaka uwe na hizi kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe tu walipa kodi wetu wajitahidi kuwa na hizi kumbukumbu kama sheria inavyotuelekeza lakini kwa jithada za Serikali yetu ya Awamu

ya Tano makampuni yote ya simu yametakiwa kupitisha miamala yao katika kanzidata yetu pale Kinondoni. Kwa hiyo, kama mlipa kodi atakuwa amepoteza kumbukumbu zake ni rahisi zaidi kuzipata taarifa zake pale katika kituo chetu cha Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili, napenda kulihakikisha Bunge lako tukufu kwamba ni sahihi tuligawa mashine hizi kwa wafanyabiashara hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam na sasa tunaandaa utaratibu wa kuwafikia wafanyabiashara wetu wote, lakini sio kwa kuwapa bure kwa sababu hata wale wa mwanzo hawakupewa bure, kilichofanyika anapewa mashine ya *EFD* halafu anakatwa kwenye kodi yake ambayo alitakiwa kuilipa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na mfumo huo na kuanzia tarehe 1 Julai, Mamlaka ya Mapato Tanzania itaanza yenye we kugawa mashine hizi badala ya kutumia mawakala ambaao wametuingiza gharama zisizo za msingi kwa wafanyabiashara wetu na tuna uhakika tunapolichukua jambo hili hata gharama za mashine hizi zitakuwa ndogo kwa wafanyabiashara wetu.

SPIKA: Hayo majibu yanatia moyo sana, hongereni sana Wizara ya Fedha na Mipango, mkianza kutoa hizo mashine itasaidia sana kuliko mawakala. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swalii la mwisho la leo la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba, kwa niaba yake tafadhalii. (*Makofii*)

Na. 276

**Changamoto Zinazowakabili Wadhibiti Ubora wa Elimu
Ngazi ya Wilaya**

**MHE. HAWA A. GHASIA (K.n.y MHE. ABDALLAH D.
CHIKOTA) aliuliza:-**

Wadhibiti wa Ubora wa Elimu ngazi ya Wilaya wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa vitendea kazi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kushughulikia changamoto za ofisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yao?

(b) Je, ni lini Wizara itapeleka Wadhibiti Ubora wa Elimu katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba badala ya kutegemea wale wa Halmashauri ya Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule kama chombo cha udhibiti wa ubora wa elimu. Kutokana na ongezeko la Halmashauri na Wilaya mpya nchini, kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika idara hii ikiwemo upungufu wa Wadhibiti Ubora wa Shule, ofisi na vitendea kazi kama vile magari. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo ununuzi wa magari, ujenzi na ukarabati wa ofisi pamoja na kuongeza idadi ya wadhibiti ubora wa shule.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imehuisha mfumo wa udhibiti ubora wa shule ambapo kiunzi cha udhibiti ubora wa elimu kimeandaliwa kwa lengo la kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wa elimu ili washiriki kikamilifu katika kusimamia ubora wa elimu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa idara ya udhibiti ubora wa shule inajengewa uwezo ili itimize majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Nanyamba ni mionganoni mwa Halmashauri ambazo hazijafunguliwa ofisi

ya udhibiti ubora wa shule. Katika kukabiliana na hii, Serikali imepanga kuanzisha huduma ya udhibiti ubora wa shule katika Halmashauri zote nchini ambazo hazijafunguliwa ofisi, ikiwemo Nanyamba pindi zoezi la kuongeza Wadhibiti Ubora wa Shule litakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, nasisitiza kuwa Wadhibiti Ubora wa Shule waliopo katika Halmashauri mama waendelee kudhibiti ubora wa shule katika Halmashauri hizo mpya wakati Serikali inaendelea na utaratibu wa kuanzisha huduma hii katika Halmashauri hizo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ina umri wa zaidi ya miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake, je, mchakato wa kuanzisha ofisi mpya ya udhibiti ubora inachukua muda gani ikiwemo ni pamoja na kupata vitendea kazi pamoja na watumishi wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri mama ambayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, bajeti ambayo imetengewa na imepelekwa na Serikali imeweza kukagua shule 18 tu kati ya shule 106; je, Serikali inapoilekeza ikakague Nanyamba kwa bajeti ipi ambayo imeipeleka? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kuhusu ni muda gani inahitajika kazi ya kuanzisha ofisi ya udhibiti ubora itachukua, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna muda maalum, yote inategemeana na upatikanaji wa fedha na tunachosema tu ni kwamba kwa sasa tumejipanga kwamba tutahakikisha kwamba Wilaya zote zinakuwa na wadhibiti

ubora. Kwa hiyo, tutaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba ofisi hizo zinakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba Halmashauri mama ya Mtwara yenewe bado hajjaweza kufanya ukaguzi kwa kiwango kikubwa.

Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo letu ni kuhakikisha kwamba kadri tunavyoendelea tunapanua uwezo wa wadhibiti ubora wetu kuweka kufanya udhibiti ubora. Kwa hiyo, hata kama sasa kiwango cha udhibiti ubora kilichofanyika bado ni kidogo lakini lengo letu ni kuendelea kuongeza fedha ili tuhakikishe kwamba tunaweza tukafanya hiyo kazi kwa ufanisi na kwa wingi zaidi.

SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa naangalia kama kuna Mbunge wa Mkoa wa Singida amesimama, lakini sijaona hata mmoja maana yake nimeambiwa Mkoa wa Singida safari hii iliyopita ndiyo imeshika mkia kwenye elimu. Mheshimiwa Sannda tafadhali.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika jitihada za kuendelea kuinua ubora wa elimu suala la kuimarisha kitengo hiki cha udhibiti ubora ni suala ambalo kwa kweli halina mjadala. Hali ilivyo sasa hivi wale wenzetu pale ni kama wamevunjika moyo na wamekata tamaa kwa kukosa motisha.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Serikali itawaweka hawa watumishi wa kitengo hiki kwenye viwango kama ilivyo maafisa elimu au walau waweze kupewa posho za madaraka kama zilivyo za Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Wataribu wa Elimu Kata? (*Makofi*)

SPIKA: Jibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Olenasha tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali kujaribu kuboresha namna tunavyofanya udhibiti ubora. Kitu cha kwanza kikubwa ambacho kimefanyika ni kubadilisha mfumo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikuwa tunazungumzia kuhusu ukaguzi au tulikuwa tunawazungumzia wakaguzi wa shule, sasa hivi mfumo ule umebadilika tunasema ni udhibiti ubora. Mfumo ambao wanaohusika sio wale wadhibiti ubora tu lakini hata walimu wenyewe na wadau wengine kama wazazi kwa mfano kama kuna watu wanamiliki shule binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mfumo uliopo sasa ni mfumo ambao ni shirikishi; tunaamini mfumo huo utatusaidia kwa sababu kila mmoja wetu anahuksika.

Mheshimiwa Spika, vilevile changamoto ambazo zipo kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwa mfano kama magari, vitendea kazi na idadi ya Wadhibiti Ubora wenyewe kama nilivyosema Serikali inaendelea kuboresha na kwa kuanzia nafikiri karibuni tutagawa hata magari kwa zaidi Halmashauri 40 kama sehemu hiyo ya jitihada zetu za kuhakikisha kwamba tunaondokana na upungufu wa vitendea kazi vilivypopo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna mpango wa kujenga ofisi zaidi ya 50 kwenye Halmashauri zetu, lengo ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha huduma ya udhibiti ubora.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kusema kwamba kwa sasa hatutegemei tena tuwasikie Wadhibiti Ubora wakifanya kazi za kipolisi, ni lazima washirikishe wadau wote wakati wanafanya zoezi la udhibiti ubora.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane tu tuishie hapa kwa leo. Ninayo matangazo ya wageni.

Ninao wageni 20 kwenye Jukwaa la Spika ambaao ni wanafunzi kutoka kule Kongwa, kumi wanasoma *St. John* na kumi kutoka *UDOM*. Naomba msimame pale mlipo. Karibuni sana vijana wangu kutoka Kongwa. Elimu ndiyo jambo la kwanza, mazanie sana suala la elimu. Tunahitaji hizo *degrees* zote kule Kongwa, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wa Mheshimiwa Mpina, Waziri wa Mifugo na Uvvi ambaao ni familia yake kutoka Jimboni kwake Kisesa ambaao ni pamoja na kaka yake, Juma Mpina, karibu sana Bwana Juma. Unajua kule Usukumani mtu akiitwa Juma, haimaanishi ni muislamu, hapana. Hili ni jina la kawaida tu. (*Makofii*)

Pia yuko Abel Mpina, mdogo wake na Mbuke Edward, mdogo wake. Pia amekuja Mheshimiwa Constantine Shilingi, Mbunge mstaafu. Mheshimiwa Shilingi uko wapi, hebu nyoosha mkono. Huyu alikuwa Mbunge wa kule Kisesa miaka ile, karibu sana. (*Makofii*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvvi ni wanachama 28 wa Chama cha Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama wakiongozwa na Ndugu Elisha Matunga, karibuni sana, wako pale. Karibuni sana wafanyabiashara wa mifugo na nyama. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 11 wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambaao ni wajasiriamali na saluni za kike kutoka Jimboni kwake Korogwe Mjini, Mkoani Tanga wakiongozwa na Saumu Kapande. Wale pale, karibuni sana. Hawa ni wataalam wa masuala ya saluni. Waheshimiwa Wabunge mkitaka *consultations* baadae, basi...! Saluni za Korogwe hizo. (*Makofii*)

Wageni 72 wa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoani Ruvuma na wengine 13 wa Chuo Kikuu cha Dodoma

wanaotokea Jimboni kwake mwenyewe Madaba. Ooh, aise! Ninyi wote ni Wangoni? Karibuni sana mjengoni. Karibuni sana wote kutoka Madaba, Ruvuma, Peramiho, wapi, karibuni sana Bungeni. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaao ni Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo vilivypo hapa Mkoani Dodoma wanaotokea Mikoa ya Lindi na Mtwara (*MTWALISO*), wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Mmuni Nevis. Wale kule, karibuni sana. Kwa kweli inatia moyo kwamba sasa hivi katika nchi yetu tunakuwa na wasomi kutoka kila pembe. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa George Lubeleje ambaao ni viongozi wa CCM Kata kutoka Mpwapwa, Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mheshimiwa Bezaleri Mnyambwa, Diwani wa Kata ya Mima, karibuni sana ndugu zangu kutoka Mima, mbarikiwe sana, tutaonana baadae saa saba na Mheshimiwa Diwani Bezaleri, karibu sana. Huko Mima mimi ndiyo nilianza darasa la kwanza huko huko. (*Makofi*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaao ni makada wa CCM kutoka Iringa Mjini wakiongozwa na Martha Ngunha. Karibuni sana wageni wetu kutoka Iringa Mjini, Mheshimiwa Ritta Kabati yuko hapa, anaendelea ku-trot. Habari za haraka haraka zinasema mwaka 2020 hapatoshi hapa. Kuna wakati siasa inanoga kweli. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Mendrad Kigola ambaao ni viongozi wa Kamati ya Siasa kutoka Mufindi, Mkoani Iringa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mufindi, Ndugu Daudi Mlowe. Karibuni sana kutoka Mufindi. (*Makofi*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Amina Makilagi ambaao ni familia yake kutoka Musoma Vijijini, Mkoani Mara

wakiongozwa nan Ndugu Theodora Makilagi ambaye ni mama yake mdogo. Hao hapo, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ambao ni viongozi wa Baraza la Vijana la CHADEMA (BAVICHA) kutoka Bukoba Mkoani Kagera. Karibuni sana wageni wetu kutoka Kagera. Naona hawapo eh! (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Wapo!

SPIKA: Karibuni sana wageni wetu kutoka Kagera. (*Kicheko/Makofi*)

Tunao wachungaji 82 wa Jumuiya Kuu ya Wabaptisti wa Tanzania kutoka mikoa mbalimbali nchini ambao wamekuja Dodoma kwa ajilli ya mukutano wao wa kitaifa. Ndugu zangu wa *Baptist Church*, ooh, karibuni sana. Tunawakaribisha Dodoma mwendelee na mukutano wenu kwa amani, lakini misisahau kutuombea, mtusaidie kufukuza mapepo hapa kwenye ukumbi huu. Myakemee, yashindwe na yalegee mapepo yote. (*Makofi*)

Wanafunzi 34 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kutoka hapa hapa, majirani zetu, karibuni sana wageni kutoka *CBE*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine ni pamoja na tangazo la *Team Managerwa Bunge Sports Club*, Mheshimiwa John Kadutu, anasema timu yetu ya *Bunge Sports Club* ya mpira wa miguu itapambana na *Mwanza Veterans* kesho kwa upande wa *netball/na football*. Jumapili kutakuwa na *football/kati* yetu sisi na *Police Bunge Forces Football Club*. Mechi zote ni saa 10.00 jioni. Kwa hiyo, saa 10.00 jioni tuwe tunaenda pale Jamhuri tunaangalia timu yetu inavyofanya kazi vizuri na wakati huu wa mfungo, basi inasaidia kupeleka saa haraka haraka ukienda mpirani.

Tangazo kwenu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha ambalo litafanyika

katika Kambi ya Jeshi ya JKT Makutupora hapa Dodoma, Wabunge wote mloliojandikisha kwa ajili ya zoezi hilo mnaombwa kufika katika viwanja vya Bunge hapo geti la Waziri Mkuu kesho saa 1.00 asubuhi kwa ajili ya safari hiyo kwa kutumia magari maalum. Hamtakwenda na magari yenu wenyewe. Kwa hiyo, wale ambaao mnapenda kwenda kulenga shabaha, kesho mfike hapo saa 1.00 asubuhi kwenye zoezi hilo.

Mara ya mwisho tulipofanya zoezi la kulenga shabaha bingwa nilikuwa ni mimi, sasa kesho nanyi mkajitahidi mvunje hiyo *record*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Dunstan Kitandula anaomba tuwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba yale maonesho ya viazi, mahindi na maharage lishe bado yanaendelea leo katika saa 5.00 asubuhi na saa 8.00 mchana katika maeneo yetu yale ya maonesho.

Kuna maonesho y a vyakula lishe hivi vya viazi, mahindi na maharage, yanaendelea katika muda huo nililotaja. Mkipita pale kwenye eneo letu la maonesho, basi mtawea kufaidika na jambo hilo muhimu kwa Waheshimiwa wapiga kura.

Tutakapoanza uchangiaji, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi ataanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaj Bulembo, Mheshimiwa Ally Keissy ajiandae, Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Hussein Bashe na wengine tutaendelea.

Katibu tuendelee.

(Hapa baadhi ya Wabunge Walisimama)

SPIKA: Basi, tulia kwanza, naona kuna watu wamesimama. Wale wa kila siku leo siwapi nafasi.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Eeh, Katibu nitajie majina.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Mwitwa Waitara na Mheshimiwa Lathifah Chande.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mheshimiwa Lathifah anza.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) pamoja na 46(1).

Mheshimiwa Spika, leo sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa swali langu namba 273 ambapo Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali langu, alilipotosha Bunge kwa kusema kwamba Kampuni ya *Sunshine* haikuza korosho za kutosha wakati kampuni hiyo katika mwaka huu wa 2017/2018 ilishiriki mara kadhaa katika minada na ilishinda katika kununua korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile sijaridhishwa na majibu ya swali langu la nyongeza ambapo nilimwomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini Serikali isifufue vile viwanda vilivyopo katika Mikoa yetu ya Lindi na Mtwara wakati tunasubiria huo ujenzi ili Serikali iweze kufikia yale malengo ya kuweza kubangua tani 200,000 za korosho? Amejibu pasipo kutuelewesha ni hatua zippi watakazochukua katika kufufua viwanda hivyo?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa nini swali langu halikujibiwa vizuri. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwikwabe.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Natumia Kanuni ya 68(7), pamoja na kwamba

jambo hili linakuhusu wewe mwenyewe, lakini naomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati tumeingia kwenye Bunge hili kwenye *briefing* mojawapo ulieleza kwamba utaboresha Bunge na haya mambo ya makatarasi mengi kujaa hapa mezani yatapungua kwa sababu tutapewa kompyuta mpakato. Sasa naona kama muda umekwenda sana, tunakaribia kumaliza kipindi cha miaka mitano, hizo kompyuta kwa kweli sijaziona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwamba hili jambo ambalo lilikuwa ni ahadi yako katika kuboresha utendaji mzuri uliotukuka katika Bunge hili, utalitekeleza lini kabla ya miaka mitano kuisha? Ni hilo tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba mwongozo wako kwa jambo hili muhimu sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1) kuhusu jambo la dharura ambalo linaendelea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taharuki kubwa kwa Watanzania kutokufahamu msimamo wetu katika diplomasia ya kimataifa na hii ni kufuatia mauaji ya Wapalestina yaliyofanywa na Waisraeli hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nchi kadhaa zimejaribu kuonesha hisia zao na kwa namna gani wamekasirishwa na jambo hilo hasa zile nchi chache ambazo zina Ubalozi nchini Israel, zimeonesha hasira zao. Kwa mfano, *South Africa* wenzetu wao wamemrejesha nyumbani Balozi wao aliyekuwa kule Israel, lakini pia wamemtimua Balozi wa Israel aliyekuwa Afrika Kusini ili kuonesha...

SPIKA: Mheshimiwa Mtolea, hutuletei jambo ambalo kwa kweli halijatokea mazingira haya, wala hatujawa nalo...

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 47(1), naomba Kiti chako kitupe muda Bunge lijadili jambo la dharura, sijasimama kwa 68(7).

SPIKA: Haya.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sasa ili kupata msimamo wa pamoja, uturuhusu Wabunge tupate angalau dakika 30 tujadili jambo hili na tuielekeze Serikali kitu cha kufanya ili na sisi kama Watanzania tuoneshe hasira zetu katika hili kwenye wigo huu wa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba busara zako.

SPIKA: Katika hili, jambo gani yaani? Umetumia neno 'hili', ni jambo gani?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, tujadili mauaji ya Wapalestina yanayofanywa na Waisraeli kwa sababu na sisi kwenye Sera yetu ya Kimataifa hatukubaliani na mauaji hayo. Sasa kwa sababu Serikali imekuwa kimya, haijasema lolote... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuomba mwongozo wako. Nimesimama kwa Kanuni ya 46, sitaisoma, lakini kimsingi inataka maswali kujibiwa kikamilifu na kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka nilipata nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza ambalo lilikuwa ni mwendelezo wa swalii namba 273 lililoulizwa na Mheshimiwa Lathifah na wakati ninauliza swalii lile nilichanganya pia na swalii la msingi kwa sababu, kama ambavyo Mheshimiwa Lathifah

amekuwa akisema, kwamba kipengele (b) cha swali lake hakikujibiwa kiufasaha.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi ni kwamba wale wafanyakazi hawana mikataba na waajiri na hii imetokea maeneo mengi tu, kwa sababu wakati wa ubanguaji wa korosho wanachukuliwa wafanyakazi wa *level/ya chini kabisa* ambao wanapewa zile ajira za muda mfupi. Hata hivyo, hakuna maelekezo ya moja kwa moja watu hawa kupata mikataba na mwisho wa msimu mara nydingi wale wenye viwanda na hii imetokea Masasi, Mtama na maeneo mengine wanakimbia, wanawaacha wale watu na madeni yao, hawataki kuwalipa wakisingizia kwamba hawajabangua vizuri au hawajapata faida.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasema tuwaambie hao wafanyakazi wakajunge *WCF (Workers' Compensation Fund)* wakati kazi kubwa ya *WCF* ni kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa salama mahali pa kazi, wakipata matatizo ya ugonjwa na mengine.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na tatizo kubwa sana la masuala ya viwanda vilivyobinafsishwa kwa eneo kubwa sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Sasa naomba Kiti chako, kwa nini kisitoe maelekezo Kamati ya Viwanda na Biashara ikaenda kujiridhisha yenye we kwenye vile viwanda vilivyobinafsishwa nchi nzima ikiwemo pamoja na viwanda vya korosho ili ije kushauri vizuri Serikali pamoja na Kiti chako.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, jana wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya anajibu swalii namba 261 linalohusu ugonjwa wa *hepatitis* au *inflammation of the liver*, sasa ugonjwa huu wa *hepatitis* unafanana na ugonjwa wa *yellow fever* (homa ya manjano). Ugonjwa wa *hepatitis* dalili zake ni mate ya njano, macho ya njano, mkojo wa njano na *yellow fever* dalili zake ni macho ya njano, mkojo wa njano.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka tu Mheshimiwa Waziri wa Afya awaelimishe wananchi magonjwa haya, kwa sababu mtu anaweza kwenda hospitali akatibiwa ugonjwa mradi tu mtu akionekana ana macho ya njano, mate na mkojo wa njano akadhaniwa kwamba ana *yellow fever* kumbe ni *hepatitis*. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Afya itoe elimu kwa wananchi na madaktari waweze kutofautisha haya magonjwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wabunge. Yote mliyoyaauliza tumeyachukua kama Meza, tutarudi kwenu kwa wakati muafaka.

Tunaendelea na uchangiaji, Mheshimiwa Dkt. Sware wa kwanza, Mheshimiwa Alhaji Abdallah Bulembo wa pili, Mheshimiwa Ally Keissy wa tatu. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2018/2018 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi, na mimi niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliypopo mezani.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa sekta ya uvuvi. Naanza na sekta ya uvuvi kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu ni sekta ambayo inaweza ikalitoa Taifa hili katika hali ya uchumi uliodorora tulionao sasa hivi. Sekta hii Mwenyezi Mungu ametujalia rasilimali ambazo tunaweza tukazitumia, tuna maziwa makubwa matatu hapa nchini yenye kilometra za mraba zaidi ya 54,000; Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Spika, tuna maziwa *size* ya kati na madogo zaidi ya 45; tuna mito mikubwa mingi, mizuri zaidi ya 20 na kitu; tuna Ukanda wa Pwani wa Bahari wa kilometa 1,420 na ukanda huu ndani ya maji ambayo wavuvi wetu wanavua zina kilometa za mraba 64,000 na ukanda wa uchumi *EEZ* wa zaidi ya kilometa za mraba laki mbili na kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, rasilimali zipo, viumbe ambavyo tunaweza tukavivuna au kuvifuga viro, wavuvi na wanaofanya shughuli za uvuvi wako zaidi ya milioni nne, wavuvi wenyewe wako 200,000 na zaidi. Sasa ukiangalia rasilimali watu tulionayo na rasilimali zenyewe za uvuvi tulizonazohaziendani na tunachokipata. Maduhuli ya mwaka 2017 yaliyokusanywa na Wizara kwenye sekta ya uvuvi ni shilingi bilioni 21 tu. Nina uhakika pia kwamba shilingi bilioni hii 21 imeongezeka kwa sababu ya shilingi billioni sita tuliyoiopata kwenye *operation sangara*.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii bajeti yake kubwa yote ni shilingi bilioni 14 tu, lakini iliyoenda hii bajeti inayoishia mwaka 2017/2018 ni asilimia 52 tu. Bajeti ya maendeleo iliyoitengwa katika sekta hii ilikuwa ni shilingi bilioni mbili, lakini kwa miaka mitatu yote iliypita inasomeka sifuri kwenye vyanzo vya ndani. Sekta ya uvuvi sasa hivi wakisema wanafanya chochote cha maendeleo, basi ni katika mikopo ya Benki ya Dunia kwenye Mradi wa *Sio Fish*, lakini kama Taifa hatujawekeza katika sekta hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mifugo na uvuvi kwa ujumla wake tunachangia katika pato la Taifa asilimia saba na kitu. Asilimia 5.6 inatoka kwenye sekta ya mifugo na asilimia 1.9 inatoka kwenye uvuvi, lakini ukiangalia hata hiyo mifugo yenyewe haijapewa kipaumbele japokuwa *in-contribute more* hata kuliko kwenye sekta ya madini ambayo *in-a-contribute* 4.5 nafikiri katika pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia uwekezaji jinsi ulivyo mdogo, tunasema kwamba kuna changamoto katika uvuvi, tunaenda kwenye ufugaji (*aquaculture*) lakini kitengo hiki

kilitengewa shilingi milioni 800 tu katika kuhakiksha *Aquaculture* inakua nchini na imepata sifuri na haikuweza hata kukusanya maduhuli yoyote, inasomeka sifuri.

Mheshimiwa Spika, tangu miaka ya 1990 au 1980 tulikuwa tuna viwanda takribani 18 vya uchakataji wa mazao ya samaki. Tunapoongea sasa hivi, tuna viwanda nane tu, vingine vyote vimefungwa. *By then* katika viwanda 18 walikuwa wameajiri wafanyakazi 4,000 na zaidi na walikuwa wana-produce tani 1,000 na kitu za samaki. Sasa hivi viwanda vya samaki vimeajiri watu chini ya 1,000 na wana-produce tani chini ya 200, nafikiri ni tani 170 za samaki.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kusema kwamba kumekuwepo na kilio kikubwa sana katika usimamizi wa rasilimali hizi za uvuvi ambazo tayari hatuzipi vipaumbele. Serikali illianzisha mchakato mzuri kabisa kupitia sera yake ya 1997 ya uvuvi ya kutengeneza hivi vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi yaani *BMUs*. Sasa hivi nchini nafikiri tuna *BMUs* 700 na kitu. Vikundi hivi katika upande wa Pwani pamoja na Ziwa Victoria, vimeterekezwa na Serikali. Kazi mahususi ya vikundi hivi ilikuwa ni kujisimamia wenyewe na kusimamia kazi za kulinda rasilimali hizi za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, tumeshindwa kugatua madaraka kwamba Wizara husika iachie TAMISEMI isimamie *BMUs* kama ilivyo kwenye sheria tuliyojiwekea wenyewe namba 22 ya mwaka 2003 ya Uvuvi. Badala yake kumekuwa na mkanganyiko wa nani asimamie rasilimali za uvuvi wakati Halmashauri husika *through* TAMISEMI ndiyo walitakiwa wasimamie hao wavuvi wadogo wadogo wakiongozwa na *BMUs*?

Mheshimiwa Spika, sasa tumeona kumekuwa na matukio ya kutokujipanga vizuri kwa Serikali na kuanzisha hizi *operation* za papo kwa hapo ambazo zinaleta gharama kubwa sana katika utekelezaji wake na kuwaumiza wale wananchi, wakati tungekuwa na zile *BMUs* tungeziwezesha na kutoa elimu, basi hawa *BMUs* wangeweza kuzilinda hizo rasilimali na kuleta tija katika sekta hii ya uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tu ni katika Halmashauri ya Pangani, walikuwa wanatumia mawakala kukusanya mapato ya uvuvi. Walikuwa wanakusanya takribani milioni 25,000, lakini Halmashauri hii ya Pangani ilihuisha *BMUs* na wakawatumia hao *BMUs*kama mawakala na sasa hivi wameweza kukusanya mapato ya shilingi bilioni 140 na kitu, yaani *ime-triple the amount*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwawezesha, siyo tu wanaweza kuingiza fedha za Halmashauri husika na kujivezesha na wenyewe pia kujifanyia shughuli zao, lakini pia wanalinda zile rasilimali za uvuvi. Sasa kwa nini hatuwi na hii mikakati ambayo tumejiwekea ambayo ni endelevu na iko *tangible*? Badala yake tunakurupuka na operesheni ambazo zinaleta vilio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema tunakurupuka? Mbele yangu hapa, hii barua nafikiri nakala imekufikia, ni kutoka kwenye Chama cha Wavuvi wakiomba Bunge liingilie kati kwenye *Operation Sangara* na nina-quote machache waliyoyaandika. Wanasema ili kupata uhalisia wa mambo tunaomba kukutana na Kamati husika tuzungumze nayo, lengo likiwa ni pamoja na kuundwa Tume ya kutembelea na kuzungumza na wavuvi kwenye maeneo husika, hivyo kubaini hali halisi ya matokeo ya *operation* hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kama ilivyokuwa kwenye *Operation Tokomeza*, yaani ya majangili, miaka ya nyuma Bunge na Umma walipata kujua uhalisia wa matokeo ya operesheni hiyo na matukio mengine baada ya Bunge kuunda Tume na kurejesha ripoti zake Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama wavuvi wamejitungia, ndiyo maana wamekuwa na uwezo wa kuja hapa Bungeni kutoa kilio chao kwamba hiyo *operation* ilivyoendeshwa imeleta madhara makubwa sana, kwa sababu baadhi ya maeneo wametumia nguvu za ziada, risasi za moto, mapanga na mabomu. Wameleta madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hatukatai, mimi kama mwana mazingira sikatai kuhusu kutunza mazingira au kuleta *operation special* kwenye maeneo ambayo ni sugu ya uharibifu wa mazingira. Ila ni njia na mikakati gani tunayoitumia ili zilete uharibifu?

Mheshimiwa Spika, mfano tu mzuri ili tuweze kwenda sawa, *traffic* akikamata gari au basi lenye abiria akamkuta dereva hana leseni au amebeba mzigو siyo au amezidisha idadi ya abiria, nini kinafanyika? Anampa faini au anaenda mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye uvuvi, mvuvi anapokamatwa kama ametenda kosa, labla hana leseni au amevua samaki kwa kutumia nyavu sizo, basi huyu mvuvi atatozwa faini, watataifisha zile mali na wanachoma moto mtumbwi au boti. *Traffic* ana uwezo wa kuchoma gari moja kwa sababu umevunja sheria? *Traffic* anataifisha gari kama umevunja sheria? Basi haya ndiyo yaliyotokea katika *Operation Sangara*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nia na lengo la Wizara inaweza ikawa nzuri lakini utekelezaji wake umeleta maafa makubwa zaidi kwa wavuvi hawa. (*Makof!*)

Kwa hiyo, naliomba Bunge lako liunde Tume kama walivyoomba hawa wavuvi, waangaliwe kwa jicho cha ziada ni nini kimetokea ili tupate kujifunza kwa operesheni zijazo, kwa sababu najua wanaenda *operation* namba mbili sijui au ni namba tatu, liangaliwe hivyo hivyo katika operesheni nyingine zitakazokuja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia kumeletwa mbele yangu kilio kutoka kwa wavuvi, Chama cha Wavuvi vilevile wakihusisha *operation* hii na upatikanaji wa nyenzo za kuvulia. Sasa hivi nyenzo hizi kama vile nyavu na maboya yamekuwa ya bei juu sana kwa sababu ya kutokuingizwa au na baadhi ya hizi nyenzo zimezuiwa kuingizwa katika *borderya* Sirali. Kwa hiyo, wanaomba nyavu hizi ziwe *available* na ziweze kupatikana na kwa bei ile ambayo inaleta tija katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, niliongelee jambo lingine liliololetwa mbele yangu ambalo ni Sheria ya Uvubi. Wadau wakuu wa Sheria ya Uvubi ambao ni wavuvi wenywewe, wanalamika kwamba hawajahusishwa katika kuirekebisha sheria hii mpya ambayo inakuja *soon* mezani kwako, wapate kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru na mengine nitaandika kwa maandishi. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie Wizara hii ambayo kwa kweli tuna majonzi sana. Nashukuru sana leo umekaa hapo mbele, ni bahati. Kwa nini, nianzie na msemaji wa sasa hivi ambaye amepita.

Mheshimiwa Spika, kuunda Tume ya Bunge kwenda kuangalia matatizo na madhara yaliyowakuta wafugaji na wavuvi haiepukiki. Kwa nini? Wavuvi wa Tanzania leo wako kwenye utumwa, kwa sababu ni watu ambao wanaishi. Nataka kutoa mfano kidogo. Ukienda Ukerewe ni kisiwa, lakini kuna Kisiwa kidogo Kulazu, kuna Kisiwa kingine Kweru, kuna Irugwa, Liegoba, kuna Burara, ukienda Bukoba kuna Bumbile, kuna Gozba na Msira. Hawa watu wanaishi visiwani, maisha yao ni kuvua samaki tu. Wamelea watoto, wamesomesha watoto, wana *ma-degree*, ni samaki peke yake, hawana kitu wanachojua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu leo ni kilio siyo kidogo, ni kikubwa. Watu wamejinyonga na kupigwa risasi kwenye *operation*. Hii hatari ni kubwa. Wana-CCM wenzangu niwaambie, tutaenda kuomba kura sisi, tunaombaje kura hawa watu wanaoteswa hivi kwa *operation* ya ajabu hii? *Operation* zimeshafanyika nyingi, katika Bunge hili tunaona haiwezekani utu wa mtu ukaharibika kwa sababu Mheshimiwa Mpina ni Waziri. Huo Uwaziri hauwezi kuwa mtu mmoja halafu CCM ikashindwa kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili Tume haiepukiki. Nina imani Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi haijamwagiza Mheshimiwa Waziri afanye hivyo na haiwezi kumwagiza hivyo. Chama cha Mapinduzi ni chama cha watu, Rais wetu anajinafsisha, anaongelea wanyonge, wanyonge wa Kanda ya Ziwa, wa Pangani, Mtwara, Mafia wanaenda kuhudumiwa na nani kama sio sisi Wabunge tulimo humu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, bado miezi tisa mnaenda kuomba kura kwenye Serikali za Mitaa, mnaenda kusema nini kwa hali hii? Mnaendaji kuongea na watu hawa? Mtanzania anakuwaje mtumwa kwenye nchi yake? Wafanyakazi wanalia, wafanyabiashara wanalia, watu wote wanalia, inawezekanaje? Hapana, Mheshimiwa Mpina huwatendei haki Watanzania! Huwatendei haki! Hii kuna siku Mungu atahukumu. Haiwezekani watu wamekuwa watumwa katika nchi yao kwa sababu ya kuvua. Ziwa lipo, tumelikuta, maeneo haya tumeyakuta, watu wanaishi hivyo, leo ni mateso. Haikubaliki hata siku moja, haikubaliki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, neno hili ni gumu sana kulisema. Wafugaji wana dhambi gani? Kufuga ni dhambi? Mtu kuwa na ng'ombe ni dhambi? Mheshimiwa Waziri anafuatwa mpaka kwenye viwanja vya Bunge hataki kuwasikiliza watu, wewe ni Waziri wa nani? Waziri wa Wizara ya kufanya nini? Kama huhudumii watu, Uwaziri wako ni wa nini? Kama huwezi kusikiliza sekta, ni nini hiki? Wako hapo nje, kila mtu anagawa karatasi, nimeumizwa, ng'ombe wangu wameuzwa wamefanya nini, kwa nini? Hii haiko ndani llani ya CCM, kwamba utakuwa Waziri, badala kumsaidia Mheshimiwa Rais, unamsababishia matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya semina ya uvuvi, ilikuwa nzuri kiasi chake, lakini yule mseminishaji anasema Mheshimiwa Rais amempongeza Waziri kwa jukumu analofanya. Nilisema pale pale na ninasema hapa, niliwaambia msimchanganye Mheshimiwa Rais na hilo, Rais hawezi kushangilia wananchi wanateswa, hawezi kushangilia wananchi wake wanaumizwa. Rais amepigwiwa kura, anatakiwa kurudi kuomba kura kule. Kwa nini

mnamchanganya Mheshimiwa Rais na matatizo ya mtu mmoja ambaye ni Waziri? Kwani Mheshimiwa Waziri kwenye sekta hii ana muda gani? Si miezi tisa! Miezi tisa tu nchi inavurugika, amani inakosa, watu hawalali, hapana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tupe Tume, ije na majibu. Simamisha *operation* zako. Mheshimiwa Waziri juzi ameenda Mwanza, amesema shughuli hii itaendelea, yale mambo ni ya wanasiasa. Wewe umetoka mbinguni? Wewe hujapigiwa kura? Hatujaja kwako kuomba kura wewe? Wewe umetoka mbinguni? Wanasiasa ni wapi? Haiwezekani, lazima tuwalinde wananchi wetu, lazima wananchi wetu wapate haki yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya huko nyuma nilikuwa kwenye CCM naongoza kitu fulani, nilitembea nchi nzima hii. Pili, nilipata bahati ya Mheshimiwa Rais kutembea naye. Watanzania ni wanyonge, watu wanaishi kwa mlo wa siku moja, watu wanajishughulisha na mambo yao, mtu anapewa Uwaziri anaona kazi ni hiyo. Haipo hivyo! CCM haitakubali, Serikali haitakubali, kila mtu abebe mzigo wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ulega nakuhurumia, ukiwa Naibu Waziri huna mamlaka, mwenye mamlaka ni Waziri wako. Kwa nini mnataabisha watu? Kwa nini tunatesa Watanzania? Au niseme, inawezekana Mheshimiwa Mpina unataka Wapinzani watushinde? Ni nini hii? Inawezekana ni *style* hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Tume kutoka ndani ya Bunge hili na *operation* zisimame. Hakuna *operation* haina muda. Kila *operation* ina muda wake. Bunge hili lituambie *operation* moja ni miezi mingapi? *Operation* mbili ni miezi mingapi? Leo unaambiwa inaenda *operation three*. Unamchukua Hakimu wa Mahakama ya Kutembea, unachukua watu wa *operation*, anakamatwa mvuvi, watu wanasema faini isiyokwenda benki, tunataka pesa *cash*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hawa wanalala *guest house*, haki ya mvuvi iko wapi? Atapewaje haki yake wakati hawa watu wanakaa kwenye hoteli? Kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jana Mbunge wangu wa Musoma Mjini pale anasema vizuri samaki wanaongezeka. Wanaongezekaje samaki? Nyavyu hazipo. Walikuwa wanavua watu 1000, leo wanavua watu 200, utaona samaki kama zipo, hazipo. Wasafirisha samaki wanaambiwa lazima muwe na mambo ya *cold room* sijui nini, watayatoa wapi? Lazima samaki wote waende viwanda ili viwanda vigate faida, ndio mtu asafirishe. Kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ni gumu kuliko kuwa kwenye ugumu. Tunasema suala hili ni gumu kwa sababu Wabunge wa CCM mtaenda kuomba kura. Maswali haya mtakutana nayo, lazima muwe na majibu. Halwezekani watu wakawa wananyanyasika katika nchi yao na sisi tunaangalia, tunakubali. Wana-CCM iteteeni CCM, kesho kutwa kuna kura hapa, tutashindaje? Tutashinda kwa *style gani?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kura zinapigwa na watu, hakuna Mbunge anayeingia humu kwa kupewa, ni sisi wachache, tumekuja kwa bahati mbaya huku labda au nzuri, muda wetu umeshaisha, mimi ni mstaafu wala siwazi chochote, sigombe popote, lakini kuisemea CCM, nitasema wakati wowote na mahali popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina umeingiaje kwenye mtego huu? Kuna mtego mmoja umeingia, nakusikitikia sana na ninakuhurumia sana. Nimesema mara mbili ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nilishasema mtu anaitwa Vediga, jana umemkaribisha hapa Bungeni mfanyakazi mzuri, ana viwanda na nini, lakini huyu ndio analeta Wahindi peke yake wanafungua *butchery* kuanzia Mtwara mpaka Singida, hakuna hata Mswahili anayefanya kazi hiyo. Wewe nawe umeingia kwenye mtego huo? Umeingia mtego huo tayari? Nakupongeza. Kwa sababu kama mtego mzuri umekunasa,

acha ukunase. Haiwezekani mtu anayetesa Watanzania, anayenyanya Watanzania wetu, leo wewe ndio umemleta kwenye *gallery* kwamba ni mfanyakazi mzuri. Viwanda viko vingapi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili najua kuna wadogo zangu wengi inawagusa kwa sababu huyu ni mwenzenu. Nasema yuko kwa Mheshimiwa Mama Jenista, yuko kwa Mambo ya Ndani, kuna jibu siku litarudi hapa ndani. Haki ya Watanzania itapatikana na haki ya weupe mnaowatanguliza mbele itapatikana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sina zaidi, naomba kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri na Serikali mniambie mnaunda Tume, mniambie *operation* inasimama na kama operesheni haiwezi kusisimama, shilingi mimi sina. Leo nasema siungi mkono hoja katika hoja iliyopo mbele yako. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawakilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Bulembo. Sasa Joseph Selasini ana safari naomba nimpe nafasi ya dakika tano. Dakika tano Katibu!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, mimi niendeleze alipoishia Mheshimiwa Bulembo. Hadithi iliyopo ni kwamba nyavu ziko za aina mbili; ya dagaa na ya sagara.

Mheshimiwa Spika, nyavu za dagaa kapewa mtu mmoja Arusha kwa njia ya ajabu ajabu. Nyavu hizo zikiingia majini mwezi mmoja, zinakatika. Matokeo yake wafanyabiashara wanaagiza nyavu kwa njia ya panya, Serikali inakosa mapato, Mheshimiwa Waziri anajua, lakini yuko kimya, hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nyavu za sangara zimechukuliwa madukani, zimechukuliwa kwa wavuvi, zimechomwa, nyavu zimeagizwa na wafanyabiashara bandarini, hairuhusiwi kutoka kwa sababu yuko mfanyakazi amepewa ili yeye ndio auze hizo nyavu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, watu wanateseka, wananyang'anywa pesa zao, shilingi milioni 20, risiti inaandikwa shilingi milioni tano. Kwa hiyo, naungana na Mheshimiwa Bulembo kwamba lazima *operation* hii isimame na uchunguzi ufanyike kwa sababu kuna harufu ya rushwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bulembo amesema vizuri, hii ni Wizara ya siasa kama ilivyo kilimo na maji, ni Wizara za siasa. Mheshimiwa Rais amenunua Bombadier, sawa; anajenga reli, sawa, lakini wananchi wa kawaida Wizara hizi zitawaondoa madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumza ni kuhusu Vituo vya Uhamilishaji. Mwalimu Nyerere alianzisha Vituo vya Uhamilishaji hasa maeneo ambayo sisi tuna *zero grazing*. Vile vituo vimekuwa sasa hivi na matokeo ya vile vituo kufa, *in-breeding* ni kubwa na *in-breeding* inasababisha magonjwa, inasababisha ukuaji mbaya wa mifugo na maziwa kupungua. Naiomba Wizara ieleze mkakati wa kurejesha vile vituo ili kupata madume bora ya ng'ombe na mbuzi ili kuongeza kipato cha wananchi kwa njia ya maziwa na nyama.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kulisemea kwa dakika zangu hizo ni kuku. Akina mama wengi wamesomesha watoto wa nchi hii kwa miradi ya kuku wa kienyeji na hao tunaoagiza, lakini hakuna chochote kilichosemwa na Wizara kuhusu mkakati uliopo wa kuendeleza ufugaji huu wa kuku.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hata ulaji wa mayai katika nchi hii umepungua kuanzia kwa watoto mpaka watu wazima na kwa sababu hiyo, lishe hii ambayo inahitajika sana kwa vijana wetu imepungua. Naomba Wizara ikija hapa ieleze mkakati ambao itatumia kuendeleza kuku na hasa kuku wetu wa kienyeji ambao wanapotea kidogo kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri akija hapa vile vile atueleze, ule ukatili uliofanywa Namanga wa kuchoma

vie vifaranga vilivyotoka Nairobi ni kwa sababu gani? Maana tuna sheria inayolinda wanyama. Vifaranga wamechomwa hadharani, ni uharibifu wa mazingira, ni ukatili, ni kuhatarisha mahusiano na wenzetu wa kutoka nje na kadhalika. Mheshimiwa Waziri atueleze, waliofanya ukatili ule wamechukuliwa hatua gani? Ili jambo hili lisipite hivi hivi bila kusemewa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu viwanda nya ngozi. Tulipandisha *export levy* hapa ya ngozi kwenda kwenye 8%, matokeo yake sasa hivi machinjio mengi wananchi wakipeleka ng'ombe zao wanaambiwa ondoka na ngozi; na pa kuipeleka ngozi hakujilikani. Ngozi zinaoza, zinanuka kwenye machinjio, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba ngozi za nchi hii zimetumika kwa ajili ya kukuza uchumi katika Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha ngozi, kwa mfano Kanda ya Kaskazini, kile cha Himo pale hakitoshi kuchukua ngozi nydingine zote. Tumezungumza habari ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ilete mkakati wa namna ambavyo ngozi italiingizia hili Taifa pato na kuondoa adha ambayo wananchi wanapata kwa sababu ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba kero hizi ambazo tunazitungumza ni kero za wananchi. Na mimi naamini kabisa kwamba...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Selasini. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Ally Keissy na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli tukichunguza, labda kwenye bahari kuu, lakini kwenye maziwa samaki wamepungua sana. Nitatolea mfano *Lake Rukwa*. *Lake Rukwa* miaka kumi iliyopita kulikuwa na samaki wengi sana, wanalisha mpaka Zambia na sehemu mbalimbali za nchi hii. Leo *Lake Rukwa* hakuna samaki hata mmoja. Sisi kule kwetu *Lake Tanganyika* wanavulia mpaka vyandarua. Tunagawa vyandarua bure, wananchi wetu wanachukua vyandarua wanafanya ndiyo uvuvi.

Mheshimiwa Spika, hizi samaki tulizopewa na Mwenyezi Mungu; je, wazazi wa zamani miaka 50 iliyopita wangetumia uvuvi kama huu uliopo sasa, tungekuta samaki? Haiwezekani. Lazima tuwaelimishe wananchi wetu waache uvuvi haramu, uvuvi wa ovyo ovyo. *Lake Victoria* miaka kumi tu, leo ni asilimia 50 ya samaki. Miaka kumi ijayo Ziwa Victoria hakuna samaki hata mmoja, hakuna.

TAARIFA

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hata maziwa yote yatakuwa ni hivyo hivyo.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Toa taarifa. (*Kicheko*)

SPIKA: Sijamwona mtoa taarifa. Mheshimiwa nimekuona, Mheshimiwa Lathifah eeh?

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Sabreena Sungura.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Sabreena endelea.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba anasema Ziwa Tanganyika watu wanavulia mpaka vyandarua.

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkoa wa Kigoma na ni Mkoa ambao Ziwa Tanganyika tuna asilimia kubwa sana ambayo ipo Mkoani kwetu. Samaki wanaovuliwa katika Ziwa Tanganyika hawafiki hata robo kwa sababu ziwa lile lina kina kirefu sana na wavuvi wetu wana zana ambazo ni dhaifu sana za kuvulia. Kwa hiyo, kuna samaki wengi sana ambaao hawavuliwi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mzungumzaji aongee ukweli ambaao upo kwa wananchi. (*Makof*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, huyu hajavua. Mimi nimevua tangu utoto wangu. Mpaka sasa piga simu kwa Afisa uvuvi, Kipili, atakwambia ni vyandarua vingapi vimekamatwa? Kwa ushaihidi vyandarua vinavua, wewe hujui chochote, wala hujaingia majini. Mwanamke gani akaingia majini kuvua? Acha kudanganya Bunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hizi samaki tumepewa sisi na vizazi vijavyo. Haiwezekani mtu ku-*support* uvuvi haramu, lazima tuwaelimishe wanachi wetu waache uvuvi haramu. Leo nenda Ziwa Tanganyika, wanakuja *Wa-congoman*, sisi watu wetu huku hawaendi Zaire kuvua, lakini nenda kwenye visiwa vya Mvuna, nenda Mwanakerenge, wamejaa *Wa-congoman* na nyavyu haramu wanavua samaki na dagaa. Yeye anasema ana ziwa, alishaingia ziwani kuvua huyu? Haiwezekani! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hizi samaki tumepewa za urithi kulinda vizaizi vijavyo. Leo sisi tunavua, wanavua vizazi miaka 15 iliyopita hakuna samaki. Mfano, Ziwa Rukwa muulize Mheshimiwa Malocha, Mbunge wa Ziwa Rukwa, waulize Wabunge wa Ziwa Rukwa, hakuna samaki *Lake Rukwa*, samaki zote zimekwisha na ilikuwa samaki malori na malori wanapeleka Zambia kuza. Leo samaki *Lake Rukwa* hakuna.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo na Ziwa Tanganyika, ukianza tu mwezi wanaingia kuvua migeureka ndugu yangu hajifika hata nchi sita au nchi saba, wanaita *nyamnyam*. Migeureka kwa kawaida inangojewa iwe mikubwa, lakini

wanaingia kuvua kuharibu samaki mpaka wanatupa kule Ziwa Tanganyika. Haiwezekani! Hizi tumepewa ni rasilimali yetu na vizazi vijavyo. Haiwezekani watu waingie kuvua jinsi wanavyovua.

Mheshimiwa Spika, nimeona viwanda vilivyokuwa *Lake Victoria*, leo vimebakira nusu, hakuna viwanda. Lazima tulinde vizazi vya samaki vinavyozaana samaki. Ile Sheria ya kuvua mita 500 kutoka mwambao wa Ziwa Tanganyika haitekelezeki. Jana tu nimepigiwa simu na mtu wa Kabwe, kuna kokoro zaidi ya kumi zinavutwa kule Kabwe, nimepigia Bwana Samaki simu, chunguza hizo kokoro. Kwa majina, ninao. Kokoro inavuta na mayai na kila kitu, imeharibu samaki. Ndugu zangu tusitake kupata kura kwa ajili ya kubembeleza ili tuharibu uchumi wa nchi. Tuelimishe watu wetu.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kubembeleza, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani ndio wanaharibu nchi hii kwa kubembeleza kura wanadanganya wananchi. Tuwe wakweli. Hatuwezi kwenda kinyume tuharibu uchumi wa nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nachangia habari ya mifugo. Tumenunua ndege *Bombardier* kwa ajili ya kukuza utalii. Tutakuza utalii kwa kutazama ng'ombe katika nchi? Tutakuza utalii kwa ajili ya kuja kutazama ng'ombe au kutazama twiga na tembo na simba na chui? Leo tunataka tupunguze mbuga za wanyama kwa ajili ya wachungaji. Ndugu zangu tufuge kisasa, siyo tuchunge.

Mheshimiwa Spika, hatutaki uchungaji! Ng'ombe ukimkuta kachoka, mchungaji kachoka, haiji. Hakuna ng'ombe zaidi ya kilo 150. Ukimchinja ukitoa utumbo na kila kitu unapata kilo 100 au kilo 70. Utasema nakuza mifugo? Haiwezekani. Lazima tuige nchi zinazoendelea kwa ajili ya ufugaji. Hatuwezi kuwa wachungaji kila siku, mchungaji anachoka na ng'ombe anachoka, haiji. Lazima tutafute sehemu ya kuchungia mifugo yao, wakae sehemu moja, siyo kuhama hama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo nazungumza habari ya Nkasi, kuna ng'ombe zaidi ya 130,000. Nkasi ilikuwa ni sehemu ya kilimo, sasa imekuwa na mwisho italeta migogoro kwa ajili ya wachungaji. Wanakuja na mifugo, mifugo inakondeana kila sehemu wanataka majosho na Serikali ndugu zangu, tufuge ng'ombe wa kisasa. Tuna ng'ombe zaidi ya 25,000 lakini hata maziwa hatuna, nyama ya kisasa hatuna, tunaagiza nyama ya kisasa nje ili watu wale nyama. Ukitaka steki, hakuna nyama ya steki, maana yake ng'ombe kakonda ni mifupa mitupu. Haiji! Lazima tupunguze mifugo, tufuge mifugo yenye uwezo ili ng'ombe afike kilo 800 au kilo 900.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu hatuvezi kuwa wachungaji sehemu zote tunakwenda barabarani kuchunga, hakuna hicho kitu. Lazima tufuate sheria na sheria ni msumeno. Haiwezekani wewe kukutetea hapa kwa ajili ya kuja kuomba kura.

Mheshimiwa Spika, hata mimi nilliingia Bungeni kwa kuomba kura, lakini nasema ukweli na watu wangu wanansikia. Siwezi kuwatetea wavuvi haramu wanakokoa kila kitu mpaka mayai ya samaki na mjukuu wangu aje kuvua wapi? Siwezi kumtetea mfugaji anaharibu ardhi, mito inakauka, vyanzo vya maji vinakauka, tutakunywa wapi maji? Wakati nchi yetu imebarikiwa na maji nchi nzima, lakini leo vyanzo vya maji vyote vimekwisha. Haiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatubembelezi kura kwa njia ya namna hiyo ya kudanganya danganya. Tuwaelimishe wananchi wetu, tuweze kwenda sawa na hili tutakwenda sawa. Hata akija kiongozi anaharibu nchi, ndiyo tumchague huyo, haiwezekani! Lazima twende na sheria, tufuate sheria. Sheria tumetunga Bungeni hapa, hakuna sheria Mheshimiwa Mpina alizotoa mfukoni kwake akaenda kwa wavuvi, hakuna. Sheria zimetoka Bungeni hapa, hazikutoka popote. Sheria ni msumeno, hata ningekuwa mimi Waziri nitakuwa hivyo hivyo, wewe ukiwa Waziri utakuwa ni hivyo hivyo au kwa sababu unaomba urudi Bungeni, hili Bunge ndugu zangu, umekuja, utatolewa, atakuja mwingine, ataendelea. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Sixtus Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na maeneo mazuri yenye uwezo wa kuifanya mifugo ikaneemeka na maziwa makubwa na bahari yenye uwezo wa kutuletea samaki wa kutosha. Baraka hizi zisipotumika vizuri hazitofautiani na mwanafunzi mwenye akili darasani halafu hana jithada, mwisho wa siku lazima atafeli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 36 ya familia za Kitanzania zinajihuisha na ufgaji. Nchi yetu ni nchi ya pili Barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya ng'ombe, inazidiwa na Ethiopia tu. Nchi yetu kwa sasa ina ng'ombe zaidi ya milioni 30. Takwimu zinatuonyesha kila mwaka kwa wastani wanaongezeka ng'ombe milioni moja. Kwa hiyo, ng'ombe milioni 30 ni fursa. Naiomba Wizara isitazame mifugo na uvuvi kama tatizo na kinachotupatia shida ni kuitazama kama tatizo, tunajinyima fursa ya kuitazama kama fursa na kuifanya ikaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwa utaratibu ukachanganua, kama nchi yetu ina ng'ombe milioni 30, tuchukulie ng'ombe wanaoweza wakauzika, yaani tukafanya *strategic farming* tunavuna ng'ombe kimkakati, tuwavune kimkakati ng'ombe milioni tano kwa mwaka, tafsiri yake, tutapata shilingi billioni tano. Ukipata shilingi billioni tano ukaenda kwenye upande wa maziwa, kila ng'ombe walete lita moja moja, katika hii hesabu utakuwa na lita bilioni sita. Ukipata shilingi billioni tano kwa mwaka tu nchi yetu inao uwezo wa kupata trillioni 1.8 kwa mwaka. Kwa upande wa kuuza ng'ombe hujagusa ngozi, hujagusa kitu chochote, unaweza ukapata trillioni 2.8 kwa mwaka. Kwa hiyo, sekta ya ng'ombe peke yake tukiitengenezea mkakati mzuri tunaweza kupata kwa mwaka trillioni nne.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona, ni kwamba hatujatazama hii fursa na tukaangalia zile changamoto zake vizuri tukaziweka pembedni. Tukienda hivi tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nina mfano mmoja. Kulikuwa na *DC* mmoja kama sikosei alikuwa wa Iramba, alipofika Iramba akatengeneza programu ya kuku mmoja, nyumba moja, familia za Iramba zikazalisha Kuku wa kienyeji wengi sana, ndani ya muda mfupi watu walijenga, mpaka kuku tunaokula hapa ni mchango wa Nawanda alipokuwa *DC* wa Iramba. Kwa nini tusifanye hivi kimkakati kwenye ng'ombe?

Mheshimiwa Spika, ng'ombe wengi siyo tatizo, uchache siyo tatizo, tatizo, tunawavuna vipi? Tukitengeneza utaratibu wa kuwavuna ng'ombe kimkakati, kila mwaka mnaondoa ng'ombe milioni tano, wanazaliwa milioni moja; *automatic echo system* itaji-set. Ni jinsi tu ya kupanga. Kupanga ni kuchagua, tukiacha kama inavyokwenda, hatutaweza. Ng'ombe watakuwa tatizo, kilimo kitakuwa tatizo na samaki watakuwa tatizo.

Mheshimiwa Waziri Mpina, hoja hapa ni ndogo tu. Mifugo kweli kuna maeneo ni matatizo. Kuna maeneo wanaingia kwenye hifadhi, kuna maeneo kule wanashambulia mahindi, kuna maeneo wanasababisha *soil erosion*, lakini lazima tutengeneze utaratibu. Mifugo imeshakuwa utamaduni. Kitu kikishakuwa utamaduni, jinsi ya kukiondoa lazima kitaleta *resistance*. Njia pekee ni kwenda nacho sambamba, *automatic* kitakuja kitapotea. Kama ng'ombe wanakulete triliuni nne kwa mwaka hakuna mtu ambaye ataacha kuuza ng'ombe wake, atauza tu kwa sababu wanamletea faida. Ni kutengeneza tu *modality* nzuri ya kuuza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni huu utaratibu wa kupiga chapa. Utaratibu wa kupiga chapa huu umepitwa na wakati. Sijui unamgonga ng'ombe kiunoni, anatoka na muhuri mkubwa, tunapoteza thamani ya ngozi. Wenzetu wana hereni (*pin*). *Pin* ina *serial number* anagongwa sikioni hapa anakuwa na *data*, anajua joshoni atakwenda lini, leo

atapigwa sindano sjui ya kifaduro, yaani kila kitu, chanjo, wenzetu wanafanya hivi. Kumpiga ng'ombe muhuri, ngozi *automatic* inapoteza thamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ijaribu kwenda kwenye teknolojia, tuweke *serial number*, anagongwa, inakwenda kwenye *database* ya Wizara, unajua kabisa ng'ombe "x" alipata chanjo siku fulani, *data* zinakuja. Hata ng'ombe aliyekufa unajua kabisa alitoka kwenye familia ya mtu fulani kwa sababu tayari tuna-*database*.

Mheshimiwa Spika, lingine, kama nilivyo sema awali, zaidi ya asilimia 36 ya Watanzania wanajihuisha na ufugaji, ama mbuzi, au ng'ombe au kuku na kitu kingine chochote kile. Mazingira hutofautiana, kwa maeneo ya kwetu sisi kule Mbinga hatuwezi kuwa na ng'ombe tukawachunga, maeneo hayako. Lazima maeneo yetu sisi, twende kwenye mkakati sasa ninaousema ndugu yangu Keissy namuunga mkono kuhusu kufuga kisasa. Kwamba utafuga ng'ombe wachache, eneo dogo, tija kubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ukienda kufuga ng'ombe wachache, eneo kubwa unapata hasara. Haya mambo lazima tuyangalie. Hii Dunia haifanani, Tanzania siyo kisiwa, lazima tui-*map* hii nchi yetu kiufugaji. *zone* zile zenye ardhi ndogo, mfumo wa ufugaji lazima utakuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, mimi hapa nina hekari 2,000 zinanitazama mbele yangu, nina ng'ombe 300, nifuge ng'ombe wanne kwa ajili ya nini wakati ardhi ninayo? Tunatofautiana. Kuna maeneo lazima tubane, ardhi haitoshi, lakini kuna maeneo tunaweza tukafuga tu, haina tatizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, namwombwa Mheshimiwa Waziri, mifugo ina thamani kubwa sana na kuna muda nadhani tunakosea. Mimi ni mkulima wa mahindi, sisi wakulima wa mahindi adui yetu namba moja ni mfugo kwa sababu akiingia ng'ombe anamaliza.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye familia zetu, mtu mwenye ng'ombe mmoja, mwenye mbuzi wawili, mwenye kuku ni biashara ambayo inatusaidia sana. Thamani ya ng'ombe mmoja inakuwa kubwa kuliko magunia 20 ya mahindi. Ukitaka sasa hivi kumpeleka mtoto shulenii, magunia 20 ya mahindi hayauziki, lakini ng'ombe mmoja, uchu wa nyama haujawahi kwisha, ng'ombe anauzika, mbuzi anauzika. Kwa nini tusiitazame hii kama fursa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja la mwisho niseme kidogo kwenye kusafirisha samaki. Mheshimiwa Mpina tunjisahau kuwajua Watanzania. Hulka ya Mtanzania akitoka kwenda kumtembelea jirani, kama ametoka shambani ana kawaida ya kubeba unga, akitoka ziwani ana kawaida ya kubeba dagaa na samaki ili anakokwenda asiende kumtia mzigo anayemtembelea. Mtu kabeba kwenye gari samaki wawili, anakwenda kumwona jirani yake, tatizo liko wapi? Sasa hivi kwenye mabasi huwezi ukabeba hata samaki wa mboga. Nikikaa hapa sasa hivi nikitaka samaki kutoka Mwanza, nitafute *cooler box*, nitaweza?

Mheshimiwa Spika, haya mambo hebu tuya-moderate, tuyaweke katika hali ambayo tunajua kabisa kusafirisha samaki wawili, dagaa ni utamaduni wa Mtanzania ili anakokwenda kule asiwe mzigo. Anatoka anakwenda Dar es Salaam, hakuna mboga; anabeba dagaa zake kutoka Mwanza au samaki wake watatu, unaweka kwenye basi, unamtoza mtu *fine*. *Why?* Kwa nini tunjisahau kuwa sisi hatujafika hiyo *stage* ya kuwa na *cooler box* na kuwa na yale malori yana-pack samaki yanafirisha? Hata yakiwepo, yatakuwa mangapi? Watakula wangapi hao samaki watakaosafirishwa kwenye hayo magari? Tuwe wa kweli. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: *Oh, my God!*

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

Waheshimiwa Wabunge, mimi mwenyewe huwa nashangaa takwimu za ng'ombe kwamba ng'ombe wetu ni mamilioni hayo. Sijui wataalam wetu watakuja kutuambia. Kwa uzoefu wangu ng'ombe wamepungua sana. Mimi mwenyewe ni mchunga ng'ombe, nimechunga sana ng'ombe. Ng'ombe wale siwaoni Mkoa wa Dodoma, sioni! Tulikuwa na ng'ombe sisi, makundi ya ng'ombe kweli kweli! Kwenye vyanzo vyetu nya kunyweshea maji ilikuwa ng'ombe kuanzia saa 9.00 usiku mnanywesha hadi saa 9.00 usiku, makundi kwa makundi, kwa makundi. Leo hii ukienda maeneo hayo, yaani pako peupe, kwa sababu kilimo kimechukua maeneo yaani utachunga wapi?

Leo hii ukitaka kuchunga ng'ombe uwe na roho ngumu. Ni kesi kila siku, yaani maeneo yamechuliwa mno na kilimo. Sasa hao ng'ombe walioongezeka wameongezeka wapi? Wataalam wanajua, lakini kwa Mkoa kama huu wa Dodoma, ng'ombe wamepungua yaani walioko ni robo ya waliokuwepo miaka ya 1970. Wamepungua sana. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa na nianze kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia Bungeni kwanza nilipewa kadi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 1995, kwa hiyo, mimi ni CCM kwanza kabla ya Ubunge. *I am putting this on record.* Katiba ya Chama changu sehemu ya kwanza kwenye madhumuni ya kuanzishwa Chama cha Mapinduzi, dhumi namba saba linasema: "Kusimamia haki na maendeleo ya wakulima, wafanyakazi na wananchi wengine wenye shughuli halali za kujitegemea na hasa kuona kwamba kila mtu ana haki ya kupata malipo yanayostahili kutokana na kazi yake." (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimesoma dhumi hili kwa makusudi kabisa ili Serikalini wajilize swali, je, wanatimiza

wajibu wa wanachama wa CCM zaidi ya milioni sita/saba/nane ambao walikaa kwenye foleni na kuomba kura za nchi hii ili kuweka Serikali madarakani? (*Makofii*)

Ninarudia, mahusiano yaliyopo kati ya Serikali na wananchi ni mahusiano kati ya *principal and agent*. Mkataba uliopo kati ya Watanzania na sisi, ni CCM na wananchi na siyo Serikali na wananchi. Chama kimepigiwa kura, tumemnadi Mheshimiwa Rais Magufuli tukampa dhamana ya kuunda Serikali, akasimamie na Serikali yake maslahi ya wananchi wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali yafuatayo; juzi tumepitisha bajeti na kwa masikitiko makubwa sana tutapisha na hii, ndiyo kawaida yetu. Jana tumepitisha bajeti ya kilimo; kilimo kinachangia asilimia 30 ya *GDP* ya nchi hii, killtengewa 0.8% ya bajeti ya maendeleo. mifugo na uvuvi inachangia 7% tumewatengea 0.04% ya bajeti ya maendeleo. Halafu tunakuja hapa tunasema kuna kuharibu mazingira, *this is nonsense*. Hamna lugha nyingine ya kutumia zaidi ya hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba unisikilize kabisa, leo hii tumezuia wavuvi wasivue, haturuhusu wavuvi wavue kwa kutumia makokoro, sawa, *what is the option?* Tumetenga shilingi ngapi ya kwenda kuwafundisha wavuvi wetu ili waanze uvuvi wa kufuga wenyewe walioko kando kando ya Ziwa Victoria? Tumewaandaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie jambo la kusikitisha, mkulima mahindi yake leo shilingi 150 kwa kilo. Na mimi nakushuru sana, umetoa maelekezo kwamba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha jje kwenye Kamati ya Bajeti. Tumeanza nao vikao, na mimi nakuahidi, tusipolewana tutarudi humu ndani. Hatuwezi kuendelea na *business as usual*. Haiwezekani Serikali inashindwa kutimiza wajibu wake, tunaenda kuwaadhibu wananchi. *We cannot allow this!* Sekta ya mifugo bajeti ya mwaka 2017 *development budget* tumepeleka asilimia ngapi? *Zero!* Sifuri. Bajeti ya kilimo tumepeleka asilimia ngapi? Asilimia 18.

T A A R I F A

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naomba kama ni taarifa iwe ya kweli lakini.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mwongeaji. Anasema kwamba Serikali imetenga fedha kidogo fedha za maendeleo kwenye bajeti mbalimbali. Tatizo siyo kutenga, ni kwamba hakuna fedha. Tatizo ni kwamba Serikali haina fedha. Hiki ilichotenga ndicho ilichonacho. Nakupa hiyo taarifa.

SPIKA: Hiyo kwa kweli wala siyo taarifa hiyo. Endelea Mheshimiwa.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, namheshimu na nimefunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri mambo yafuatayo: Kwanza, nikizungumzia Sekta ya Mifugo. Ninaongea kuhusu Sekta ya Mifugo kwa mambo makubwa mawili. Moja, nimezaliwa ndani ya mifugo ndiyo sababu naifahamu. Toka mwaka 1983 hakuna *proper breeding programme* iliyoanywa na Serikali ya nchi yetu. Hakuna!

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mwalimu Nyerere iliandaa sehemu zinazoitwa *holding ground* kwa ajili ya *breeding programme*. Kwangu Nzega na Jimbo la Selemiani Zedi, kulikuwa na eneo linaitwa Kisasiga. Kule kwetu tuna ng'ombe zinazoitwa Tarime, Waziri anazijua. Ni ng'ombe ndogo, ngozi yake ni nyembamba, lakini zinaweza ku-survive kwenye ukame. Mwalimu akasema ili nimwongezee *value* huyu Msukuma, akaleta ng'ombe aina ya borani, akaziweka Kisasiga. Mwaka 1990 ziliuzwa kubinafisisha zote hadi ardhi. Pale pamebaki *open*, hakuna chochote. Mkoa wa Tabora kuanzia Nzega kwenda Tabora Kaskazini kwenda Urambo, kwenda Sikunge, kwenda Wilaya zote zaidi ya asilimia 60 ni hifadhi. Hawa wafugaji wanaenda wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unajua jambo linalonisikitisha, nami nataka nirudie humu ndani, Serikalini hatuna nia mbaya na Mawaziri, hapa kuna *politics* ya ajabu sana, mimi sio mwenyeji ndani ya Bunge, nina miaka miwili tu. Mbunge akisimama akiongea, atakuwa *branded a name aidha, anamchukia* Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Simchukii Mheshimiwa Dkt. Magufuli, *I have voted for him, I have campaigned for him for sixty days.* Na mimi kama Rais Magufuli asingekuwa mgombea wangu mwaka 2020, *I didn't care. Nisinge-care* kusema haya ninayosema ndani ya Bunge kila wakati, *but because I know he is my candidate,* nitasema *as far as* nimo ndani ya Bunge hili. Nataka niwaombe hii bajeti turudishe. Bajeti hii irudi na siyo kwa nia mbaya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo wafugaji wanauawa, nataka nikupe kichekesho. Kule Nzega wanakata leseni ya kufanya biashara. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, ukimsumbuu anakusaidia. Anakata leseni ya kusafirisha ng'ombe, inaitwa kabisa leseni ya kusafirisha ng'ombe nje Mkoo wako, analipa na mapato na kila kitu, akifika hapo Nala anakamatwa. Anakamatwa mama aliyebeba kuku 200 anazipeleka Dar es Salaam, anaambiya alipe faini ya *two million. What is this?* Nchi yetu leo mkulima ananyanyasika, mfugaji ananyanyasika, mvuvi ananyanyasika, machinga ananyanyasika na mfanyabiashara ananyanyasika. *This is unfair and we should not allow it.*

Mheshimiwa Spika, nakushauri unda Tume ya Bunge, mimi sio mtalaam wa Kanuni. Jambo la kusikitisha, nataka nikwambie jambo, Mheshimiwa Nape aliandaa Hoja Binafsi inayohusu wafugaji. Hizi Kanuni za ajabu tuzibadilishe kwa maslahi ya nchi yetu na chama chetu. Tukaitwa kwenye Kamati yetu ya Uongozi ya chama chetu. Nataka nikwambie, hata kama tukifuata kanuni na taratibu zote, hoja zinazohusu wananchi zinaenda kufia kwenye Kamati za Vyama. *Why are we here? (Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, kama tumeamua kuwa na mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ambapo vyama hivi vinatuleta ndani ya Bunge, tuna mihimili mitatu,

kila mhimili utimize wajibu wake kwa maslahi ya Taifa hili.
(*Makofi/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie ndugu yangu Mpina, hapa mkononi nina *document nitamkabidhi*. *Leather sector* tunaye mwekezaji amekuja ana kiwanda kikubwa sana Ethiopia. Tunasema *industrialization*, kama hatu-invest kwenye sekta ya kilimo na mifugo, *let us forget about industrialization*. Wizara ya Fedha inazungumzia 3.9% ya *inflation*. Mnajua bei ya batii ni shilingi ngapi? Ni shilingi 30,000, ng'ombe shilingi 150,000, mahindi shilingi 150, halafu tunasema tuna-control *inflation* kwa kuwatia umaskini watu. *We should not allow this*. Sekta ya *leather...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, ndio ya kwanza eeh!

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Tunakushukuru sana kwa mchango wako.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Tunaendelea sasa kwa upande wa CUF, atakuwa Mheshimiwa Hamidu Bobali na Mheshimiwa Selemani Bungara. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Wapo wazungumzaji wamenitangulia wamechukua baadhi ya hoja zangu, lakini naweza nikaongezea kidogo. Nianzie pale alipoishia mzee wangu, Mheshimiwa Bulembo.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Bunge, Wabunge walio wengi ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, pia Serikali inayoongoza ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Wakati wa utengenezaji wa bajeti viko vitu vinaangaliwa, inaangaliwa

Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inaangaliwa hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge lako, lakini pia unaangaliwa Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi...

SPIKA: Mheshimiwa Bobali ni dakika tano eh!

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika ahsante.

Mheshimiwa Spika, jana nimeangalia kwa makini sana, nimeipitia kwa mara ya kwanza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nimeona kumbe ilani imeandika vizuri sana juu ya uendelezaji wa sekta ya uvuvi na mifugo. Jana hiyo hiyo nikapitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lakini pia nikasikiliza na *clip* ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge lako mwezi Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, yaliyoandikwa kwenye Ilani ya CCM, yaliyoandikwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na aliyoyasema Mheshimiwa Rais, hayajatekelezwa yote kwenye sekta ya uvuvi na mifugo. Hayajatekelezwa! Bajeti imepata asilimia sifuri ya maendeleo kwa mwaka 2017 au mwaka huu tulionao, 2018. Maana yake ni kwamba sekta ya uvuvi na sekta ya mifugo ndiyo basi tena, imekwenda kuzimu. Waswahili wanasesma imekwenda kuzimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna ukanda wa bahari wa kilometra 1,400 kuanzia Mtwara mpaka unafika Tanga. Kwa maajabu makubwa kabisa, ni Tanzania pekee ambako wavuvi ndio maskini. Katika maeneo nchi tulizopakana nazo, ukienda katika visiwa vya Mauritius, ukienda Seychelles na maeneo mengine, Zanzibar tu inawezekana huu umaskini wa Zanzibar labda tumewaambukiza sisi. Hata maeneo ya Comoro, wale wavuvi sio masikini kama wavuvi wa Tanzania. Leo wavuvi wa Tanzania ndio wamekuwa na laana ya kuwa maskini jambo ambalo kwa kweli linasababishwa na usimamizi mbovu na sera mbovu za chama kinachoongoza, lazima tuseme ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jana nimekutana na wavuvi kutoka upande wa Kanda wa Ziwa, wana malalamiko makubwa. Wanalamika kwamba sasa hivi wamezuiwa kabisa kuvua. Hoja iliyoletwa mezani kwako ya kuunda Tume, naomba sana uiunge mkono. Kuna haja ya kubwa sana ya kuchunguza. Najua umeunda Tume ya Kuchunguza Uvuvi. Kuna haja kubwa sana ya kuangalia operesheni inayofanywa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maftaha amezungumzia hapa kwamba kule Mtwara kuna kijana amepigwa risasi. Kwa bahati mbaya yule kijana mimi namfahamu, amepigwa risasi ya kisogoni na hawa watu ambao wanasema wanapambana na uvuvi haramu. Nataka nikuhakikishie uvuvi wa mabomu haupo Mtwara, haupo Lindi, sasa hivi watu wameacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zamani tulikuwa hatupati samaki, nami niliwaambia, nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Nilimwambia Mheshimiwa Mpina, kama kuna jambo mlitusaidia na wananchi wameelewa, wameacha kupiga mabomu, niliwaambia kwenye Kamati. Wakati fulani nilimwambia Mheshimiwa Ulega alikuwa Mjumbe mwenzetu wa Kamati. Nilisema *operation* hizi za kwenda kupambana na uvuvi haramu, msipokuwa makini, mnakwenda kuua Watanzania wasiokuwa na hatia. Leo yametokea, watu wamepigwa risasi. Leo pale Jimboni kwangu Mchinga, vijana wa maeneo ya Ruvu, Mchinga na Kijiweni hawana shughuli nyingine zaidi ya uvuvi. Wakienda wanakutana na askari, wanawatisha, watu wanaacha uvuvi wanarudi. Tunawaongezea umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kwenda kuchunguza kilichoendelea kwenye *operation* hii inayoitwa tokomeza ni jambo muhimu na isifanyike kwenye ukanda wa ziwa tu, ufanyike pia maeneo ya Mtwara, maeneo ya Lindi na maeneo ya Kilwa kwa sababu pia watu wamedhurika kwa kiwango kikubwa sana na hii operesheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ufugaji, sisi watu wa Mkoa wa Lindi na Wilaya tatu siyo Wilaya zote. Mkoa wa Lindi kwenye maeneo mengine walikataa kupokea mifugo wakati wanahamishwa kutoka Ihefu, lakini Wilaya ya Lindi ambako mimi ndiko ninakotoka, Wilaya ya Kilwa na Liwale tulikubali. Tulikubali kwa sababu maeneo ya kuwaweka wafugaji tunayo. Kwa bahati mbaya walipoletwa ni kama tu tumewa-*damp*, hawajaendelezwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Hamidu.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Selemani Bungara, dakika tano pia.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataalah*. Pili, naishukuru Serikali ya CCM kwa kutufikisha hapa tulipofikishwa.

Mheshimiwa Spika, juzi niliwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba hata firauni alikuwa mbaya, lakini watu wake waliokuwa nyuma yake, wanamuunga mkono. Sasa huyu firauni aliota ndoto kwamba ataondolewa katika ufalme wake na akaamua kwamba kila nyumba kumi kuwepo na watu, kila atakapozaliwa mtoto wa kiume auliwe ili ufalme wake uendelee. Bahati nzuri akazaliwa Musa akamlea yeye mwenyewe na ndio yeye akamwangamiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kubwa sana Waheshimiwa, hayo mnayoyatetea katika upande wa Serikali ya CCM, leo Waheshimiwa wawili wamesema CCM tunakufa eeh! Na mimi naamini kwamba CCM itajua yenyeewe kama alivyosema Nyerere. Naomba sana Serikali ya CCM muendele na hayo mnayoyafanya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ya CCM mnatutaka Wapinzani lakini hamtutaki, lakini sisi hatuwataki lakini tunawapendeni. Tukiwaambieni maneno mazuri ndiyo tunawapenda hivyo, mfanye. Mkifanya tu mambo mazuri tu Tanzania, naomba sana Serikali ya CCM muwe wasikivu, moja hiyo.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie habari ya mifugo kwanza, Kilwa mmetuletea mifugo, tulikuwa hatujui mifugo tunashukuru sana sasa hivi tunapata maziwa mengi, lakini hamjawatendea haki wafugaji walikwenda kule, hawana malambo wala hakuna majosho. Naomba sana Serikali ya CCM kwa kuwa mliwatoa mlilikowatoa kuwaleta Kilwa hebu tuleeteeni malambo na majosho ili wakae vizuri wale wafugaji, hilo ni ombi la kwanza hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi la pili kwetu Kilwa tuna maeneo ya ng'ombe wale, kuna vijiji vingine vimeambiwa wafuge ng'ombe wengine wawe wakulima Mheshimiwa Ulega najua. Kwa mfano, kijiji cha Nakiu ni kijiji cha wakulima lakini kuna ng'ombe siyo chini ya 2000 tunawaomba kila siku ng'ombe hao waende katika sehemu husika hawaendi, tatizo kubwa inawezekana viongozi wa Mkoa na Wilaya kama wamepata rushwa hivi, Mkuu wa Mkoa huyu na Mkuu wa Wilaya ninawasiwasi wamepata rushwa, kwa sababu Mkuu wa Wilaya kaandika barua kwamba ng'ombe wa kijiji cha Nakiu watolewe mwezi wa Novemba waondoke, lakini mpaka leo hawajatolewa na ukimuuliza Mkuu wa Wilaya anasema hela za kuwatoa sina. Ukiwaambia polisi wakawatoe wanasesma hela hatuna na kijiji cha Nakiu kimewahi kutoa shilingi 1,500,000 kuwapa polisi kwamba hawana posho, hela wamechukua ng'ombe wapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii sasa Jeshi la Polisi hawana uwezo mpaka kijiji kitoe hela kiwape polisi, hela wamechukua na ng'ombe mpaka leo wapo, kweli hii Serikali, kwamba polisi hawana hela mpaka wanakijiji watoe hela na wanatoa hela halafu ng'ombe hawajatolewa? Mkuu wa Wilaya kala rushwa, Mkuu wa Mkoa kala rushwa, polisi wamekula rushwa na kama hawakula rushwa tuwaone

ng'ombe watoke, leo bila hivyo wamekula rushwa! (*Makofi/ Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara naomba ukae kidogo.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ama kuna mwongozo?

SPIKA: Ukae tu.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: *In Shaa Allah.*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Nchi tafadhali nimekuona.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ni jambo la utaratibu, Kanuni zetu na hasa kifungu cha 64(1)(a) kinataka Mbunge anapozungumza Bungeni awe anasema ukweli kuhusu taarifa alizonazo na ili taarifa ziwe za ukweli ni lazima awe na uthibitisho ambao anao kwenye mkono wake. Kanuni zinataka mtu anayetaka kum-prove Mbunge kwamba jambo analolizungumza siyo la ukweli na ye ye ni lazima awe na uthibitisho.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anapomtuhumu Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kwamba wamekula rushwa, hapo katika mkono wake hana uthibitisho kwamba kweli wale watu wamekula rushwa katika jambo hilo, kwa sababu hana ukweli wa jambo wa hilo na hajashika *document* yoyote na hajasema anawasilisha mezani kwako kwamba ushahidi wa jambo hili ni huu, kwa hiyo ni dhahiri kwamba anachozungumza hakina ukweli na ni tuhuma. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama hivyo ndivyo ninaomba afute hicho anachowatuhumu Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wamekula rushwa, lakini kama ana ukweli wa jambo hilo kwa mujibu wa utaratibu wa kuthibitisha na mimi ninathibitisha hana ukweli kwa sababu hana uthibitisho

anaowakilisha mezani aje alete taarifa za kuthibitisha jambo hilo kwa kutumia utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara una njia mbili, huzuiwi kusema, ama utakapokuwa na ushahidi wako basi utatuwekea hapa wa hayo, la huna basi ili kuweka maneno vizuri hebu futa ile kauli yako halafu uendelee, sasa chaguo ni la kwako mwenyewe.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kusema na nipe dakika moja tu nisema. Nimesema kijiji kimetoa fedha kwa ajili ya kuwapa polisi kuja kutoa ng'ombe, lakini fedha wametoa na ng'ombe hawakutolewa kwa mazingira haya nina wasiwasi watu wamepewa rushwa na kama kutoa rushwa basi ng'ombe wale watoke, kama hawakutoka wamepewa rushwa. Ndiyo hoja yangu mimi, nina uhakika kijiji kimetoa hela na ng'ombe hawajatoka. Sasa kama hawajatoka hela ile ndiyo rushwa, sasa kama wewe unasema habari hizi ni za uongo thibitisha wewe, tuende kijijini mimi na wewe kama hela hazikutolewa. (*Makofi/ Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Bungara dakika tano zimeisha.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, mimi mwanasiasa eeh! (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, anayefuata ni Mheshimiwa Jacqueline Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Mheshimiwa Msongozi. Hili Bunge! Mheshimiwa Jacqueline endelea tafadhali. (*Kicheko*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline subiri. Mheshimiwa Jenista unajua ndugu zetu wengine kidogo taabu huku, yaani kusagwa ng'ombe mpaka polisi waalikwe badala ya wao

wenyewe kusagwa tu, kusagwa ng'ombe mpaka ulete Majeshi? Mheshimiwa Jacqueline endelea. (*Kicheko*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwinci wa rehema mwinci wa utukufu kwa kunipa uzima ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Uvuvi.

Pia nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Ni ukweli usiopingika kwamba nchi ya Tanzania sasa inakwenda kupaa kiuchumi, kila baada ya wiki moja tunashuhudia uzinduzi wa miradi mbalimbali, hongera sana kwako Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, niwapongeze sana Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina na Naibu wako. Nitakuwa sijatenda haki kama sijakupongeza sana Spika kwa namna ambavyo unachapa kazi, kwa namna ambavyo unasimamia Bunge hili, sasa hivi Bunge limetulia, ukiona chombo kimetulia basi ujue kwamba msimamizi wa chombo hicho yuko makini na mambo yanakwenda bara bara, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la uvuvi wa samaki kwa maana ya sekta ya uvuvi. Katika sekta ya uvuvi nitajikita moja kwa moja Ziwa Nyasa. Nimesoma katika hotuba hii ya Waziri wa Mifugo, hotuba yake katika ukurasa wa 82 na 83 kwenye kipengele kila cha utafiti inaonesha kwamba katika utafiti ambao wameufanya katika maziwa yote pamoja na bahari kuna samaki tani 2,736,247 na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo; Ziwa Victoria lina tani 2,148,248; Ziwa Tanganyika tani 295,000; Ziwa Nyasa tani 168,000 na Bahari ya Hindi tani 100,000.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti huu ambao wameufanya naomba niende kwenye Ziwa Nyasa. Ziwa

Nyasa inaoneshwa kwamba pana tani 168,000 lakini naomba nimuambie Mheshimiwa Waziri kwa maana ya utafiti huo naona kwamba tani hizi ni chache. Je, Serikali au Wizara ina mpango gani wa kuinua au wa kuweka mikakati ambayo itaweka uzalishaji mzuri kwenye hilo ziwa ili ziwa hili liweze kuweka samaki wengi zaidi, ukizingatia kwamba Ziwa Nyasa ni ziwa la pili kwa wingi wa maji, kwa hiyo lina uwezo mkubwa sana wa kuweza kutunza samaki wengi.

Mheshimiwa Spika, pia jirani zetu wa nchi ya Malawi wamekuwa wakifanya uhifadhi wa samaki kwa maana ya *fish cage*, kwa hiyo kwa uzalishaji na utunzaji huo wa samaki umepelekea samaki wetu kutoka huku upande wa Tanzania wanakimbilia kule kwa ajili ya kwenda kupata chakula, kwa hiyo inaonekana kwamba kwenye Ziwa Nyasa upande wa Tanzania hatuna samaki wengi.

Ninaombwa Serikali yangu ifanye mkakati wa maksudi na ninaamini kabisa Wizara hii ina Mawaziri vijana ambao tumeona wanafanya kazi na wanakwenda maeneo mbalimbali. Ninaamini kabisa wana uwezo mkubwa wa kuweka mikakati mizuri ambayo itakwenda kuzalisha na kwa kuwa, namuona Mheshimiwa Mpina amedhamiria kabisa kukuza sekta hii ya uvuvi hebu nenda kafanye utafiti mzuri zaidi na uone namna gani mnaweza kuinua uzalishaji huu katika Ziwa Nyasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina toka umepata madaraka haya ya Uwaziri hujaenda kule Ziwa Nyasa ni lini utaenda Ziwa Nyasa ukatembelee ukaone namna ambavyo ziwa lile liliyo na ni ziwa ambalo lina vivutio vizuri sana vyatulii, kuna samaki wengi wa mapambo, kuna dagaa wazuri watamu kweli na siku moja hapa nilimtolea mfano dada yangu Mheshimiwa Jenista nikasema angalia hiyo *brand* ya Mheshimiwa Jenista namna alivyokuwa mzuri ni kwa sababu ya samaki wazuri watamu ambao wanatoka Ziwa Nyasa. Lakini pia nenda kamuangalie dada yangu Mheshimiwa Manyanya muda wote yuko vizuri kwa sababu ya samaki wazuri na mimi mwenyewe je? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, karibu sana Mkoa wa Ruvuma katika Ziwa Nyasa uone aina ya samaki watamu na wazuri ambao wana virutubisho vizuri na ukishakula wale samaki hata magonjwa yanakaa mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmewaona watoto wa Kingoni hao? (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, napata shida sana, nilidhani kwamba unapokuwa na Bahari ya Hindi maana yake kwa ukubwa wake tunaweza tukawa tunapata tani nyingi za samaki kule, kumbe hii methali inayosema ukubwa wa pua siyo wingi wa..., samahani. Nashangazwa na tani chache hizi ambazo zimeainishwa hapa kwa maana ya utafiti uliofanyika kwenye Bahari ya Hindi. Wizara mna mkakati gani wa kuweka mpango mzuri ambao utakwenda kuhakikisha kwamba Bahari ya Hindi tunaitumia vizuri ili tuweze kupata pato kubwa.

Mimi siyo mtaalam wa mambo ya uvuvi lakini naona niongelee, halafu ninyi kama Wizara mtaona namna ya kuweka vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara iwezeshwe kwa pesa, kama tunazungumzia kwamba waweze kuinua uchumi, waweze kufanya mambo mbalimbali kwenye sekta hii, basi tuhakikishe kwamba hii Wizara inapewa pesa ili iweze kutekeleza majukumu yote ambayo tunadhani kwamba yanafaa kwa Wizara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nirudie tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais aendelee kufanya kazi na kwamba wenzeni sasa Wapinzani wetu wamekuwa kama vile wamepanda basi ambalo wanaendesha gizani na wanatembelea taa za *parking*, Mheshimiwa Rais endelea kuchapa kazi, tuko nyuma yako, tunakuunga mkono sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge tutakaporudi saa 10 kamili jioni ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri halafu Mheshimiwa Waziri katika ile saa yenu moja baada ya hapo tutaendelea na utaratibu wa Kamati ya Matumizi.

Mheshimiwa Goodluck Mlinga nimeshakutaja atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala na Mheshimiwa Jumanne Kishimba ajiandae. Mheshimiwa Mlinga tafadhalii.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ni dakika 10?

SPIKA: Ndiyo ni dakika kumi.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa namna ya pekee naomba niishukuru taasisi moja ya kidini ambayo inachimba visima bure katika Jimbo langu la Ulanga, taasisi inaitwa *AlFayed Charitable Foundation* chini ya usimamizi wake wa Ndugu Khadija Ahmad, nadhani unaifahamu hii taasisi, hapa ndiyo najua uwezo wa wanawake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii taasisi kiongozi wake ni mwanamke na inafanya kazi vizuri, kwa hiyo hongera sana wanawake, imeshachimba visima 57 na wana utaratibu wa kuchimba visima 300. Kwa hiyo, Jimboni kwangu suala la maji mambo ni poa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niweke katika *record*, katika Bunge lililopita wakati yupo Naibu Spika, Mbunge machachari kabisa kwa upande wa CCM alikuwa Mheshimiwa Luhaga Mpina, sasa hivi kwa bahati mbaya machachari tumeongezeka na bahati mbaya wewe upo huko, kwa hiyo, tuache tukushughulikie sehemu zile ambazo unakosea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninapongeza zoezi la kupinga uvuvi haramu, kwa mfano Mto Kilombero samaki wamekwisha kabisa, lakini zoezi hili linaloendelea lina ukatili mkubwa, lina dhulumia kubwa, lina filisi watu, lina rushwa kubwa na linaleta usumbufu kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sidhani kama watendaji wa Serikali wana nia nzuri kama ya wavuvi ambao wanaishi katika yale maeneo na sijawahi kuona mkakati wa Serikali, labda tuseme mnawawekea pumba hawa samaki au mnawalisha au mnafanya nini, kwa nini mnakuwa wakatili kiasi hiki? Sielewi! Tunawafanya Watanzania kama siyo wapiga kura wetu, humu ndani tumeingia kwa kupigiwa kura, kwa hiyo tuwathamini watu waliotupigia kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni suala la nyavu na hii naomba niliseme wazi. Mheshimiwa Waziri Wizara yako imekithiri kwa rushwa, nasema hivyo kwa sababu viwanda vinavyotengeneza nyavu za samaki ni vichache na havina uwezo wa kukudhi soko, leo hii meli iko bandarini hawaruhusiwi kuingiza nyavu pale wanawekewa mlolongo mrefu na kwa taarifa nilizonazo wale wenye viwanda wamei-*corrupt* Wizara matokeo yake hamna mtu ye yeyote anayeruhusiwa kuingiza nyavu ili wao wauze, lazima tuseme ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa spika, suala langu la tatu ni biashara ya samaki. Samaki wengi tunaokula wanatoka nje ya nchi, hata watu wanaoruhusiwa kuingiza wote ni watu weupe, wote ni Wahindi, watu weusi wote wamezuiliwa na hii ni kwa sababu ya rushwa. Mheshimiwa Rais wetu mweusi tangu wa kwanza, kwa nini hatuwaamini watu weusi? Viongozi, Mawaziri wote watu weusi kwa nini hatuwaamini? Akija muhindi, mwarabu tunamatetemekeea, kwa nini tusiwaruhusu watu weusi ambao wana uwezo na wana uchungu wa nchi hii wasiweze kuingiza samaki?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la malisho ya mifugo, katika jimbo langu la Ulanga tuna mapori mengi kweli ...

T A R I F A

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, mzungumzaji anayezungumza sasa hivi analeta lugha za kibaguzi ndani ya Bunge lako, naomba abadilishe msemo wake na aendelee na mchango wake.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga endelea.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa Murrad utaniwia radhi nimewagusa, lakini hili suala linaumiza sana, kwa sababu watu wote wanaoingiza samaki hamna mtu mweusi hata mmoja, akienda wanasema hana uwezo! Kweli watu weusi hatuna uwezo? Hakuna watu wenye hela? Mabasi mbona wapo watu weusi wanamiliki akina Kimbinyiko wote siyo watu weusi? Hata Shabiby yule ni mweusi umeona lakini hawaruhuswi wanaambiwa hawana uwezo pamoja na Mheshimiwa Murrad. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la malisho ya mifugo, kwa mfano Ulanga tuna maeneo mengi sana ya mapori, lakini wafugaji wanapotaka maeneo ya kulisha wanaambiwa maeneo hamna, kwa hiyo hawa watu wamekuwa wanahangaika. Naishauri Serikali tuwatengee maeneo ya malisho, tukishawatengea maeneo ya malisho sasa hivi ziko mbegu ambazo zinapandwa kwa muda mfupi zinaota nyasi nzuri kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majosho ninaishukuru Serikali imeniahidi kunijengea majosho na malambo kwa ajili ya mifugo, napendekeza hizi mbegu za mifugo za madume bora ziweze kuuzwa kwa bei nafuu ili wananchi wetu waweze kumudu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la watu wa maliasili kukamata mifugo na kuishikilia kwa muda mrefu na kuhitaji pesa kubwa, hii imekuwa unyanyasaji mkubwa sana kwa wafanyabiashara wetu wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la masoko kwenye minada yetu wafugaji wanapopeleka mifugo sokoni wauze ama wasiuze wanatozwa ushuru, hili limekuwa linaleta usumbufu mkubwa, Serikali imeniahidi katika Jimbo langu la Ulanga litaweka utaratibu wa masoko mazuri ya mifugo, minada iwe ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni suala la upigaji chapa, suala hili siliungi mkono kabisa, kwanza ni unyanyasaji wa wanyama, pili ni gharama wafugaji ambao hatuwasaidii kitu tunaenda kupiga chapa tu kwao tunataka pesa, tatu ni usumbufu kwa wafugaji wenyewe na hata kwa wanyama. Sababu wanayosema wanapiga chapa kwa wanyama ni eti wasichanganyike na wanyama wengine ambao wanatoka nje ya nchi. Jamani mbona watu wa mipakani hatuwapigi chapa, kwa nini tupige chapa mifugo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naona hili zoezi lifutwe kwa sababu kwanza lina haribu hata thamani ya ngozi, kwa sababu ngozi ukishaipiga chapa thamani yake inashuka. Leo hii tunasema Tanzania ya viwanda, viwanda vyta ngozi vitakosa mazao ya ngozi kwa sababu ya ubora mdogo wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, machache mimi siungi mkono hoja, nataka huu mkazo wa kusitisha hii *operation* ya kuzuia uvuvi haramu, iundwe Tume ya Kibunge, litakapotolewa hilo ndipo nitaunga mkono hoja, la sivyo nitafanya kampeni ya Mbunge mmoja baada ya mwingine kuhakikisha bajeti hii haipiti na Mheshimiwa Waziri unajua uwezo wangu, nitafanya kampeni ya Mbunge kwa Mbunge kuhakikisha bajeti yako haipiti mpaka iundwe Kamati kwa ajili ya kuondoa hii *operation* haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Peneza kwa dakika tano.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema na kuweka wazi kwamba sitaunga mkono hoja hadi hapo masuala yangu ya kimsingi yatakapopewa majibu na hayo majibu anipatie Mheshimiwa Waziri akiwa anajua ninachokisema na nitayapima majibu yake kadri atakavyoyatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Tume ya kushughulikia mgogoro kuhusu masuala ya ranchi, alieleza humu Bungeni kwamba wananchi wawe na subira, alikuja Misenyi akaeleza wanachi wawe na subira ili tuweze kupata ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wananchi wanaendelea kuwa na subira Serikali itoe ufumbuzi wa migogoro ile, viongozi wengine wa nafasi za chini, wala sina sababu ya kuwataja majina na nafasi zao kwa sababu ni wa chini mno kiasi ambacho Mbunge kuwataja ni kuwaonea, wanaandika barua kwa wananchi kwamba waondoke mara moja kwenye maeneo yenye migogoro.

Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu chanzo cha migogoro ni Wizara yake atakapokuwa anajibu aeleze kwanini wanaendelea kufanya mizengwe ya kutaka kufukuza wananchi, kwenye maeneo ambayo bado hayajapatiwa ufumbuzi, wakati yapo maelekezo ya Serikali kwamba tusubiri tuwe na subira, wananchi wamekuwa na subira kwanini wao hawahitaji kuwa na subira? Hilo ni jambo la kwanza nitahitaji majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, pili ninayo ramani hapa inaonesha unapovuka Mto Kagera ukaenda mpaka Uganda eneo lote lile ni *Misenyi Ranch*, hakuna mtu ambaye hata kama ni mtoto angezaliwa leo anayeweza kukubaliana na ramani hii. Kwa sababu ya kanuni sitataja kiongozi mmoja ambaye alishaagiza ramani hii irejeshwe ili ifutwe kwa sababu haiko sahihi. Naogopa kumtaja kwa sababu mwininge anaweza

kusimama akasema Kanuni haziruhusu, sasa sitaki kuombewa mwongozo bila ya sababu, lakini ramani hii sio sahihi, kwa sababu unapovuka Mto Kagera unakutana na Makao Makuu ya Wilaya, unapoenda mbele unakuta vijiji, unakuta Kata, sasa unapokuja na ramani unaitumia kugawa *blocks Misenyi Ranch* kusema kuanzia Mto Kagera kwenda mpaka Uganda yote ni ranch, ukagawa ukapata *blocks* 22 siwezi kukubaliana na masuala haya. Ndiyo maana nasema Mheshimiwa akija atoe maelekezo na majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, pia ipo ramani nyingine inayooonesha kwamba *Misenyi Ranch* imezungukwa na vijiji, ukiangalia nyaraka mbalimbali ambazo nizazo hapa vijiji hivi vina hati, vimesajiliwa na vinatambulika na vilipimwa. Ukitosha taarifa hii kuna sehemu Mheshimiwa Waziri anasema kuna vijiji vimevamia *ranch*. Napenda niseme mimi kama Mbunge wa Jimbo la Nkenge kwamba ranchi ndiyo imevamia vijiji. Sasa hatuwezi kuruhusu mambo ya namna hii hatuwezi kuruhusu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtu wa mwisho kupokea mambo ya namna hii. Nikisema hivi, wako wengine walitaka kunipima sitaki kuwataja kwa sababu ukishakuwa Mbunge, Mbunge unashimamia Serikali, wako waliojaribu kunipima, kuna bwana mmoja alinipa barua akasema nenda uwaambie wananchi wako waondoke. Nilimjibu nikasema Mheshimiwa kwa nafasi yako huwezi kuniagiza, mimi naishimamia Serikali na wewe ni sehemu ya Serikali sasa lazima kila mtu aheshimu nafasi yake. Ukiwa Mkuu wa Mkoa, ukiwa sijui nani wewe fanya kazi yako na mimi acha nifanye kazi yangu. Hilo nililisema na naendelea kulisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtu wa mwisho kuwaambia wananchi waondoke kwenye maeneo yao ambayo wana haki ya kukaa, na mimi nikiwa hapa natamka wananchi wangu katika maeneo yao wakae mpaka hapo nitakaposema kwamba sasa Serikali imeleta taarifa Bungeni na taarifa hiyo nimeikubali, vinginevyo wanapoteza muda wao bure hizo barua wanazoandika wanapoteza muda wao bure na hii vita niko tayari kuisimamia, niko tayari kupambana

ndani ya Bunge, nje ya Bunge na kokote kule watakaponipeleka nipo tayari na nitafanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nisema kwamba mipaka ya ranchi na Misenyi na vijiji inaeleweka, mwaka 1968 ranchi hiyo ilipokuwa inaanizisha, walioanzisha ranchi hiyo walienda wakakutana na wananchi na wananchi hao baadhi yao bado wapo wanaendelea kuishi. Walikubaliana kwamba mipaka ya ranchi itakuwa Mto Kiboroga pamoja na Mto Kyakakuru. Mheshimiwa Waziri utakapotoa majibu hapa unieleze hii mipaka kwa nini hamuioni na kwa nini hamtaki kuitambua?

Mheshimiwa Spika, tulifanya *operation* kubwa ya kuondoa ng'ombe kwenye hifadhi za Serikali, ng'ombe wakaondolewa Biharamulo, jambo la kushangaza baada ya ng'ombe hao kuondolewa Biharamulo sasa wamepelekwa katika Ranchi ya Misenyi. Taarifa nilizonazo kwa mfano katika *block No. 15* mwenye kitalu amepokea shilingi 50,000 kutoka kwa wachungaji wawili wenyе ng'ombe 600, ukichukua shilingi 50,000 mara 600 unapata shilingi milioni 30. Hizo ni pesa kapokea tu kwa kuwapa ardhı ya vijiji watu wachungie. Nashangaa Waziri anaposema hana hela, hela unazo sema hutaki kuzikusanya.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kuna vitalu kumi vimefanyiwa tathmini, lakini ukiangalia ramani hii niliyoionesha hapa wao walismawana vitalu 22, kama una vitalu 22 kwa nini hivi vitalu vingine hutaki kufanyia tathmini unafanyia 10 tu? Hautaki kufanyia tathmini vitalu vyote kwa sababu taarifa zilizopo na nina uhakika hizi ni taarifa za kweli, mkitaka taarifa natoa hapa, ninayo taarifa hapa inaonesha katika Ranchi ya Misenyi katika zile *blocks* tulio wapa tukifikiri ni wawekezaji siyo wawekezaji ni wachungaji tu. *Misenyi Ranch* kumejaa ng'ombe za kutoka nchi jirani hakuna asiyejua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeenda kule nimeingia kwenye ranchi nilifanya ziara ya kushtukiza nimeingia mle kwanza ni

rahisi kuingia kutambua kwa sababu ng'ombe wote wa Ranchi ya Misenyi wanajulikana. Nilipoingia mle nikakuta kuna ng'ombe wengi tu ambao ni aina ya Ankole. Ranchi ya Misenyi haina ng'ombe aina ya Ankole, wale ng'ombe wote na ushahidi ninao nilipiga picha na hizo picha nimezihifadhi kwenye sehemu mbalimbali na zingine nimeziweka sehemu zingine ili zisiweze kuibwa, kwa hiyo mtu yejote asije akaniteka akafikiri akiniteka hizo picha atazipata, hutazipata kwa sababu zimehifadhiwa pengine na watu wana *password*.

Mheshimiwa Spika, ng'ombe wale cha kushangaza wala hawajapigwa chapa, sasa viongozi wakuu wa nchi wameagiza ngo'mbe wote wapigwe chapa lakini kule Ranchi ya Misenyi ng'ombe wamo, kwanza siyo wa *Misenyi Ranch*, lakini wanakula kwenye majosho ya *Misenyi Ranch* wanalindwa, nani anawalinda hao? Lakini kwa mwananchi mmoja tu akijaribu tu ng'ombe wake kuingia kwenye *ranch* anakamatwa anatozwa faini 50,000.

Mheshimiwa Spika, nasema wazi kabisa hapa, hakuna mwananchi wangu katika Jimbo la Nkenge katika Kata ya Kakunyu na maeneo yote atakayetoka kwenye ardhi hata kwa *inch* moja hadi hapo nitakaposema. Vita hii nipo tayari kuisimamia, ninazungumza mimi, Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala na katika hili nitaweka Ubalozi kidogo pembeni ili nifanye vizuri kwa sababu kuna rafiki yangu alikuwa ananiambia Mheshimiwa toka umekuwa Balozi umebadilika. Ndiyo nimebadilika kidogo lakini Balozi ni yule yule na Kamala ni yule yule na utaalam ni ule ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa wavuvi wa Kashenye, nazungukwa na Ziwa Victoria, wale wavuvi siku moja nilienda kule nilitaka niangalie wanapata samaki kiasi gani, nikakaa kwenye mwalo pale wakaenda kule, vijana walivyokuja hawakurudi na samaki. Nikauliza vipi samaki wapo wapi? Wakasema Mheshimiwa unajua kwa nini tulete samaki wetu hapa tukishawapata huko kwenye maji tunaenda kuwauza Uganda kwa sababu Uganda kodi zao kimsingi ziko chini, lakini tukikanyaga upande wa Tanzania

kodi nyingi mnoo lakini tukiwa tunakuja hivi, kuna *operation* juu ya *operation*, kwa hiyo tunaona ni bora tukishapata samaki wetu twende tuuze Uganda. Kwa hiyo, Mheshimiwa Balozi kwa kweli kama bado una muda wa kukaa hapa, kaa uendelee kusubiri hautaona samaki wowote. Kwa hiyo, nikapiga *salute* nikawashukuru nikaondoka. Hivyo Mheshimiwa Mpina hizi kampeni unazozifanya hebu ziangalie zisije zikatuletea matatizo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema siungi mkono hoja hadi hapo nitakapopata majibu ya kina kuhusu hoja nilizozitoa hapa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Upendo Peneza dakika tano atafuatiwa na Jumanne Kishimba.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba tu uniruhusu nisome kidogo baadhi ya vipaumbele katika sekta ya mifugo ambapo kuna kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kutenga maeneo ya malisho, kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo, kuimarisha tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kufanya sensa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015/2016 baada ya kuteuliwa kuwa Mbunge, nilipangwa katika Kamati ambayo ilikuwa ni kubwa kidogo kwa maana Kamati ya Kilimo, Mifugo pamoja na Uvuvi zikiwa pamoja. Vipaumbele ambavyo vinasemwa leo ni vipaumbele ambavyo vimekuwepo tangu mwaka wa kwanza kabisa mimi nimetuwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndani ya Bunge kipindi Wizara hii ipo pamoja bado haijatenganisha kulikuwa kumetokea ushindani wa aina fulani baina ya Wabunge kwa maana

Wabunge wa Kilimo na Wabunge walioitoka katika maeneo ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametusaidia, amezitenganisha Wizara hizi. Hata baada ya kututenganisha tatizo limebaki kama liliyokuwa tangu mwanzo nilipoingia katika Bunge hili. Mwaka wa kwanza kabisa 2016/2017 Serikali haikutenga pesa yoyote kwenda katika upande wa mifugo. Mwaka 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni sita kwa maana ya shilingi bilioni nne upande mifugo na shilingi bilioni mbili upande wa uvuvi. Pesa ambazo hazijapelekwa mpaka leo hii tunajadili bajeti nyine. Leo Serikali inatenga tena bajeti ya shilingi bilioni 12 kwa maana ya bajeti hii na nina wasiwasi kwamba pesa hizi vilevile zinaweza sizipelekwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kipaumbele cha kwanza kwamba kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kutenga maeneo ya malisho, tunashawishika Wabunge kuwaambia wananchi kwamba Serikali ni sehemu mojawapo ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Serikali ni washirika moja kwa moja kuhakikisha kwamba wakulima na wafugaji hawawezi kupatana na mapigano yaendelee. Kwa sababu kama tunatenga pesa na Bunge linapitisha ili kazi iweze kufanya na Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya wafugaji na hilo halifanyiki, maana yake ni kwamba wanaoshiriki kuwaua wakulima, wanaoshiriki kuwaua wafugaji na Serikali imo mionganoni mwao lakini wao ni *background players* katika mauaji hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ifike wakati sasa kwa sababu Serikali yenyewe inashiriki kwa nyuma katika mauaji haya, basi ione umuhimu wa kuona kwamba ni lazima pesa hizi ziwe zinatengwa ili kazi ambayo imepangwa kufanya iweze kufanya. Tunaongea kifua mbele kwamba Wizara imekusanya maduhuli shilingi bilioni 21 kutoka kwenye mifugo, lakini tukiangalia kwamba wamewasaida nini hao wafugaji mpaka kwa hizo tozo wanazozitoa, hakuna lolote ambalo linafanyika kuweza kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa tozo ambazo zipo kwa maana ya leseni za biashara, tozo za kusafirisha ng'ombe, tozo za kulipia kila ng'ombe wanapokuwa wakihama katika eneo moja kwenda lingine ni vizuri sasa hizo kodi zikapunguzwa, kwa sababu kama mtu humsaidii katika kuhakikisha ya kwamba anakuwa na mazingira bora ya kuweza kuwatanza wale ng'ombe wake, ni muhimu sasa Serikali walau ikapunguza maumivu kwa hawa wafugaji ili kuhakikisha kwamba wanaweza walau wakaendelea bila ya tozo hizi za manyanyaso.

Mheshimiwa Spika, katika kilimo Serikali ilipunguza tozo na sasa Serikali iangalie pia namna ya kuweza kupunguza tozo ambazo zinawakabili wafugaji ili na wao kwa kile walichonacho basi washiriki katika kusaidia mifugo yao na wao wenyewe badala ya kuendelea kuilipa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea pia kidogo suala ambalo ameliongelea Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala. Suala hili pia ni tangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba akiwa Waziri wa Wizara hii yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Kamati Serikali ilitoa ahadi ya kwamba inafanya mchakato wa kuhakikisha kwamba ranchi zote ambazo zilingaiwa kwa watu zamani, ambazo hazifanyi kazi ziweze kurejeshwa na watu wengine wapatiwe ili maeneo ya kufugia ng'ombe ziweze kupatikana. Suala hili sasa ni miaka mitatu halijatimia Wizara ni hii tumeendelea kuongea mpaka mwisho hakuna linalofanyika, kwa sababu tu Serikali inashindwa kutoa hela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ifike mahali sasa hawa wananchi ambao Rais anawaita anawapenda ni maskini, hebu tuwepende kwa vitendo kwa hela kupatikana ili kuboresha mazingira ya wananchi waweze kuwa vizuri. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Upendo Peneza. Mheshimiwa Jumanne Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa dakika tano. Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvubi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaonekana ndiyo Wizara ambayo itakuwa ngumu safari hii kwenye Bunge letu. Namuomba ndugu yangu Mheshimiwa Mpina ambaye anatoka eneo la wafugaji wa ng'ombe, tunaotoka maeneo ya ufugaji tunaomba hizi ranchi kwa mara ya kwanza ziruhusiwe wananchi wetu waweke ng'ombe mle, walipie officially Serikalini ili Serikali na Wizara yake ipate pesa badala ya sasa hivi pesa hizo zinaenda kwa watunzaji wa hifadhi hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo tunahangaika watu wanachukua ng'ombe kutoka Usukumanzi kwenda mpaka Lindi, lakini tuna Ranchi ya Mwabuki ambayo inaweza kuchukua ng'ombe zaidi ya 500,000 mpaka milioni moja. Wizara kama itaruhusu ng'ombe laki tano au milioni moja wakakaa pale Mwabuki, kutajengwa automatically viwanda vyta maziwa, vitajengwa viwanda vyta nyama bila hata shuruti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ranchi hiyo haina ng'ombe zaidi ya 500. Kuna fisi, kuna nguruwe, hakuna kitu chochote. Ingekuwa vizuri Wizara ikaanza kuchukua *action*.

Mheshimiwa Spika, tuna pori ambalo linatokea Kahama mpaka Kigoma, Mheshimiwa Dotto alikuwa analia sana mara nyingi maana yake amepakana nalo. Pori hilo lina urefu wa kilometra 400, upana kilometra 250. Halina wanyama, siyo *National Park* kwamba watalii wanaenda, kwa nini Serikali isitoe hata asilimia kumi ikaruhusu watu wakaweka ng'ombe zao na wakalipia officially Serikalini na ikapata mapato na wananchi wetu wakapata malisho.

Mheshimiwa Spika, nawalaumu sana wataalam wa mazingira, ni kweli wanatupotosha na ni waongo. Ng'ombe hali miti wala hali udongo, ng'ombe anakula nyasi. Ng'ombe akila nyasi kwenye pori wakati wa kiangazi moto unapokuja

unainusuru ile miti. Wataalam wanatuletea maneno ya Ulaya ya uongo kwamba ng'ombe akiingia kwenye lile pori ataharibu, ataharibu nini.

Mheshimiwa Spika, pori lile ni nusu ya nchi ya Uganda. Ni kweli ng'ombe waliopo pale wanaweza kudhuru nini? Leo wako ng'ombe pale wanatozwa pesa na watu wanapata pesa hakuna kitu chochote. Ni vizuri Mheshimiwa Mpina Serikali yako ili ipate pesa, ruhusu watu wachunge *officially*, uwatoze pesa *officially*, lakini wananchi wetu watapata manufaa na maendeleo pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye suala la uvuvi. Mimi kwangu sina ziwa wala mto lakini makao yangu ni Mwanza. Ukweli hali inayoendelea kule Kanda ya Ziwa ni hatari na sijawahi kuiona kwa zaidi ya miaka 30. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mwanza, ukiondoa kilimo, ukaondoa na dhahabu kinachofuata ni samaki. Leo hali iliyopo kule ni hofu, sijawahi kuiona kwenye maisha yangu. Mwananchi wa kawaida anakatazwa kubeba samaki kwenye pikipiki anakimbizwa, kwenye baiskeli anakimbizwa, matokeo yake haijulikani hasa samaki wanatakiwa kupigwa marufuku au inatakiwa nini. Kama kuna tamko la Serikali, basi Serikali itamke kwamba imesitisha ulaji wa samaki kwa muda hadi hapo itakavyojulikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wavuvi hawa wanaosemwa, kweli siungi mkono uvuvi haramu lakini hawezi akakosea mtu mmoja tukaamua kwenda kupiga watu wetu kwa *model* hiyo, kwa kweli nakataa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lawama kubwa naitupa kwa wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvumi. Nchi zinazoongoza duniani sasa hivi kwa uuzaji wa samaki, siyo nchi zenyen maziwa wala bahari, nchi ya Thailand ndiyo inazoongoza kwa samaki, Serikali inatoa vifaranga milioni 200 kila mwezi, inawapa raia wake wafuge ama kwenye malambo, mabeseni, ndoo, baada ya miaka miwili, samaki walio nchi kavu ni wengi kuliko waliopo ziwani. Kwa matokeo hayo,

Mheshimiwa Mpina na wataalam wake ambao tunawaita wachawi wa kizungu, maana wasomi wenzetu tunawaita wachawi wa kizungu, wenyeji wanaitwa wachawi wa kienyeji ni kweli!

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu ambao ni wasomi, msomi kugeuka kuwa mgambo kwenda kupiga raia inahuzunisha sana. Kazi hiyo ilitakiwa ifanywe na mtu ambaye hana *degree*, siyo kama Maprofesa alionao nao Mheshimiwa Mpina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo kama wataalam wasingetengeneza mayai ya kizungu, leo mayai ya kienyeji yangekuwa shilingi 5,000. Wataalam wasingetengeneza kuku wa kizungu, leo kuku wa kienyeji angekuwa shilingi 50,000. Wenzetu wasomi wao walikaa wakafikiri, badala ya kugombana na wananchi wakaja na *solution, solution* hilo ndio inayotufanya leo hatujaamka kwenda kugombana na wananchi wanaofuga kuku na mayai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wazalishé samaki, warudishe mbegu za samaki kila mwezi ziwani, wawagawie na wananchi mbegu za samaki bila kupeleka maneno yao ya mazingira, bila kupeleka maneno yao ya uongo ya mazingira, uongo mtupu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Mpina ajaribu kupunguza jazba. Ni kweli wananchi kule hawana nyavu. Nyavu zinazotengenezwa zinatoka Kiwanda cha *Sunflag*, kiwanda hiki kinatengeneza vyandarua hata kama tutaficha, lakini kweli nyavu hizo zinaweza kuvua samaki? Vyandarua haviwezi kuvua samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Mpina, asituone Wabunge kama ni watu wabaya, wote tunategemea samaki, tuna biashara zetu kule ambazo siyo samaki lakini zina uhusiano na samaki, hatuwezi kukataa, maeneo yetu yote yale yanahuksika na samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwangu Kahama samaki wanaliwa. *Population* ya watu imeongezeka, ulaji wa samaki umeongezeka, haiwezekani wataalam wetu, watu waliosoma kwa gharama kubwa wanang'ang'ana tu kupiga watu badala ya kung'ang'ana kutafuta ufumbuzi! Kama ndugu zetu wazungu walivyoleta ufumbuzi wa kutengeneza mayai, wakatengeneza na kuku wa kizungu, leo hatuna mgogoro unachagua mwenyewe unachotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kweli leo Maprofesa wazima wanaungana kwenda kupiga watu! Uzuri na Mheshimiwa Profesa Kabudi kama yuko hapa ingekuwa ni wanasheria au madaktari wangesimamishwa kwa ajili ya *degree* zao lakini sijui kwa *degree* zingine kwamba sheria inasemaje kama mtu aliyesoma anapoharibu heshima ya *degree* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo yote naomba vilevile kwa Mawaziri ambao tunaendelea na migogoro mingi hapa, kwa zile sheria ambazo Mawaziri wanazona kama zina matatizo, wazilete tena sheria hizo Bungeni zifanyiwe marekebisho kama Mheshimiwa Rais anavyofanya. Mheshimiwa Rais juzi alifanya mabadiliko akaleta Sheria ya Madini, amesema iletwe Sheria ya Mafuta ifanyiwe mabadiliko, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mawaziri wengine ambao wanaona kuna matatizo, leteni sheria hizo hapa zifanyiwe mabadiliko ili kuondoa ugomvi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Kishimba huwa anaongea taratibu lakini nimem-note ni kati ya Wasukuma wachache wenye *point* kali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Kishimba anasema wale mliosomea *degree* za *fisheries* sasa mmegeuka kuwa ma-boxer. Mkurugenzi Bohay na wenzako huko yaani, sasa ninyi ngumi mkononi tu jamani! Zalisheni vifaranga muwagawie wananchi, ni *point* muhimu kweli ili kupitia ma-ponds na

kadhalika tuwe na samaki wengi kuliko Ziwa Victoria. Tutakuwa tumefika mahali pazuri sana. Kwa kweli wavuvi mnatia albu, mmeamua kupiga watu jamani. (*Makof/ Kicheko*)

Lakini *point* ya pili pia ya *ranches* kuangalia namna ambavyo wananchi wanaweza wakashiriki kuweka mifugo na kufaidisha *ranches* ni *point* muhimu sana, ingawaje kule *Kongwa Ranch* Mheshimiwa Waziri kwa maana ya malisho thamani ya malisho ya mifugo imepungua sana kwa sababu magugu yamekuwa mengi mno. Sasa hivi ukipita kuna ua fulani jeupe liko *all over the place*, lile ni gugu moja hatari sana! Kwa maana malisho ile ranchi labda iko asilimia 40 or less. Kwa hiyo, mtu ukiangalia unaweza ukapiga hesabu ya eneo ulilonalo kumbe kimalisho ni eneo dogo sana, limevamiwa sana na magugu, inabidi kutafuta namna ya kuondoa magugu yale.

Mheshimiwa Mbarouk nilishakutaja dakika tano, baada ya hapo Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukutana na tukajadili mambo ya nchi yetu, lakini jambo lingine niwatakie heri ya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislam wote Tanzania na duniani kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kuzungumzia hali ya uvuvi Tanzania katika kitabu cha Wizara ukurasa wa 82 ambapo pana takwimu zimetolewa hapa kwamba Ziwa Victoria kwa mwaka kuna tani 2,143,248; Ziwa Tanganyika tani 295,000; Ziwa Nyasa tani 168,000; Bahari ya Hindi tani 100,000 maji ya Kitaifa ambapo ninavyoamini ni katika ule ukanda unaoanzia Jasini karibu na Kenya mpaka Msimbati ambapo ni kilometra 1,425 na mabwawa madogo madogo yanazalisha tani 30 kwa mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi sikubaliani nazo. Haiwezekani ikawa Ziwa Victoria litoe samaki tani 2,143,000 lakini ukanda wote wa bahari wa maji ya Kitaifa utoe tani 100,000 tu! Naomba Waziri atakapokuja atupe takwimu sahihi au labda niwe nimeelewa vinginevyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie hali ya uvuvi katika nchi yetu kwa ujumla. Wataalam wanasema *if you fail to plan, you plan to fail*, hapa ndiyo ninapoona pana tatizo, kwa sababu haiingii akilini kwamba Wizara badala ya kukaa na wavuvi kuwaelimisha elimu ya uvuvi wa kisasa, nyavu zinazotakiwa kisheria, vilevile pia kuwapa elimu ya madhara ya uvuvi haramu sasa kazi yetu imekuwa ni kuanzisha *operation*. *Operation* haitengenezi jambo na waswahili wanasema kosa siyo kutenda kosa, kosa ni kurudia kosa.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma kulikuwa na *Operation Tokomeza*, ikaleta balaa kubwa katika nchi yetu. Wafugaji waliuawa, ng'ombe wakapigwa risasi na hali ikawa mbaya katika nchi. Sasa inakuwaje Waziri Mpina sasa naye badala ya kurekebisha makosa anarudia makosa anatuletea *operation!* Naona hapa haliko sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nimtake atakapokuja, hivi katika fikra zake zote kama Waziri aliyeaminwa na Rais Magufuli, hana *plan* ya kufanya ni lazima aendeshe kwa *operation*. Wavuvi hawataki *operation*, naamini kwamba wavuvi ni watu ambao ni waelewa, wavuvi wamejaribu kuunda vyama vyao vidogovidogo lakini hata katika kanuni ambazo zinaanzishwa za uvuvi hawashirikishwi.

Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa na baadhi ya wavuvi hapa, malalamiko yao ni hayo. Wameandika barua tarehe 25 Julai, 2017 wakaambiwa kwamba wataitwa na Waziri, watacaa naye kikao ili warekebishe mambo, matokeo yake mpaka bajeti inaletwa hapa, Waziri hajawaita. Kama hilo halitoshi, katika hiyo *Operation Sangara*, kuna kitu ambacho mpaka sasa hivi sielewi. Nilisikia kwenye

taarifa ya habari kwamba hata mama lishe wanahusishwa na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, mama lishe kazi yake ananunua samaki, amewapikia chakula wavuvi, mama anaambiya atoe faini shilingi milioni mbili halafu banda lake la mama lishe linachomwa moto. Najiuliza sasa, huyu Waziri Mpina anayefanya ukatili huu ni kweli amezaliwa na mama? Kwa sababu ni lazima akina mama tuwaonee huruma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa taarifa yako akina mama baada ya kukosa ajira, ndiyo wanaolea familia. Sasa leo matokeo yake mama lishe wanachomewa mabanda yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuwachomea wavuvi nyavu. Kwetu baharini na hata kwenye maziwa, Tanga kuna dagaa wale wadogo wadogo wanaitwa uono, Mwenyezi Mungu ndiyo alivyowaumba hiyyo kama hivi binadamu kuna wengine warefu, wengine wanene, wengine wafupi; uono, dagaa wa Mwanza na dagaa wa Kigoma yale ndiyo maumbile yao. Sasa unapomwambia mvuvi avue na nyavu ya nchi nne au nyavu ya nchi mbili atamuaje dagaa yule? Hebu watutafutie njia mbadala, mnapowakataza Watanzania wasivue, ujue unahatarisha ajira ya zaidi ya asilimia 36 ya Watanzania ambao utawafanya wasiwe na ajira.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mpina atakapokuja hapa ku-*wind up* atueleze ni nyavu zipi zinazoweza kuvua uono, dagaa wa Mwanza na dagaa wa Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, *Operation Jodari*. Hii operesheni katika ukanda wetu wa Pwani imekuwa ni balaa, ni tatizo. Wavuvi wanalishwa samaki wabichi, wavuvi wanalishwa pweza wabichi, sijui kama unamjua pweza alivyo akiwa mbichi anavyokuwa. Mtu analazimishwa amle mbichi, hivi Mheshimiwa Waziri kama ni ye ye angeweza kula pweza mbichi? Kwa nini tuwfanyiwe wavuvi ukatili kiasi hiki? Kwa sababu uvuvi unaingiza asilimia

mbili ya Pato letu la Taifa. Ilikuwa ni kiasi cha kukaa nao na kuwaelimisha ili tupate mapato mazuri kwa Serikali lakini matokeo yake ni kuwapiga, wengine wanapigwa risasi.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Tongoni Tanga yupo mvuvi amepigwa risasi kwa sababu eti ni mvuvi haramu! Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje atupe njia mbadala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la leseni, leseni kila baada ya miaka miwili inapandishwa bei, kwa nini chombo kimoja kina wavuvi zaidi ya 25 wote wawe na leseni? Ninavyojuua mtumbwi ni sawasawa na basi au gari. Anatakiwa kepteni awe na leseni, wale wengine ni kama Wasaidizi wa kuvuta nyavu za jarife na kutupa mishipi, kwa nini kepteni awe na leseni, wavuvi wawe na leseni, chombo kiwe na leseni, samaki walipishwe ushuru, huu ni uonevu. Tunamtaka Waziri aondoe leseni kwa wavuvi, leseni ibaki kwa kepteni peke yake kama ilivyo leseni kwa dereva wa basi, kondakta hana leseni na *tanboy* vilevile hana leseni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, tuwape elimu wavuvi wawe wavuvi bora na wa kisasa. Amesema msemaji mmoja hapa kama sikosei Mheshimiwa Bashe kwamba katika Katiba ya CCM Ibara ya 7 inazungumzia majukumu ya CCM ni kulinda haki na kuhakikisha kila mtu anapata haki yake kutokana na kazi anayoifanya. Ninawashauri wavuvi mpo hapa, kama mtaona haki yenu hamuipati tishieni kama vile wenzenu wanavyofanya kurudisha kadi za CCM. Sasa hivi *operation zitasimamishwa* na ninyi mtabaki salama, lakini mkiendelea kuwa kimya, *operation zitaendelea*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya mifugo, Tanzania ni ya pili kwa mifugo katika Bara la Afrika, lakini tujulize ni wananchi wangapi wanakula nyama? Kama hilo halitoshi kwenye suala la upigaji chapa, tunatumia gharama kubwa lakini ni kuharibu ngozi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk. Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaamini nina dakika kumi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu mkubwa sana katika sekta ya uvuvi pamoja na mifugo, ndiyo maana ameiweka Wizara hii ili tuweze kupata nafasi kubwa sana katika kujadili changamoto zote zinazogusa sekta hii. Kwa hiyo ninampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba pasipokuwa na changamoto, hakuna mafanikio. Kwa hiyo, ninaamini kwa changamoto zote zinazojitokeza katika sekta ya uvuvi pamoja na mifugo ndiko tunakoelekea kwenye mafanikio. Ninaomba sana Wizara ipokee changamoto hizo na izifanyie kazi kwa sababu ndiyo hasa ilikuwa kusudio la Mheshimiwa Rais ili kuweza kuwasaidia wale wananchi ambao wanaguswa na sekta hii.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wangu wa Singida tuna ufugaji. Kwanza ni wafugaji lakini pia wakulima, tumekuwa na ufugaji mzuri na ukulima bila migogoro kwa muda mrefu sana. Migogoro huwa inakuja pale wageni wanapokuja kuingiza mifugo kwenye maeneo ambayo wenyewe hatukuwa tumekusudia kwa ajili ya kulisha mifugo lakini Serikali za Mkoa, Vijiji na Wilaya wemekuwa wakijadili na kuingia muafaka.

Mheshimimiwa Spika, kuna jambo ambalo Mheshimiwa Waziri katika taarifa yako, sielewi kama kweli unaona ufugaji wa kuku ambao hasa uko katika Mkoa wa Singida ni sehemu mojawapo ya kuwaondolea umaskini Watanzania, pia ni kipato kinachotokana na ufugaji wa kuku, sijaona kama umetilia mkazo. Singida kuku ni chanzo cha kipato, lakini bado ni chakula na ni utamaduni wetu. Hata

mtoto mdogo ukienda kumtembelea shangazi, anakupatia kuku kwa ajili ya kwenda kumfuga, kumuendeleza. Ni utamaduni wetu mgeni akifika ni lazima kwanza mboga ya haraka ni kuku. Waziri unatakiwa sasa uwatoe wananchi wa Mkoa wa Singida kwenye utamaduni kwamba ni ukarimu tu, iwe ni biashara tena biashara yenyeye tija kwa wananchi wa Mkoa wa Singida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wataalam walioko kule uwape maelekezo kama ambavyo mnaweza kutoa maelekezo kwenye mazao mengine, pia kwenye ufugaji wa kuku utoe maelekezo wataalam waende wakawasaidie na kutoa dawa, wafuatiliwe ili kuweza kukuza ufugaji wa kuku wa Singida ambao ni watamu sana wote mnafahamu. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Sana!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nikitoka kwenye eneo hilo niende kwenye uvuvi. Na sisi pia tuna uvuvi Singida, ukienda Ziwa Singidani na Kindai. Pia nataka nizungumzie Kitangiri. Kwanza nataka ielewewe na Waziri utakaposimama hapo useme, Wilaya ya Iramba ndiyo yenyeye Ziwa Kitangiri, useme hapo leo ili wananchi wote wasikie, kwa sababu Kitangiri tunaita Kiteka, wavuvi wanaovua pale wanaotoka upande wa Meatu, kwanza Serikali ya Halmashauri ya Meatu haitendei haki Serikali ya Halmashauri ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Iramba inapofunga ziwa lile kwa ajili ya kuhakikisha vifaranga wale wanakua, Meatu hawafungi na wakati haiko kwao! Ushuru wanapokea wao, hela zile haziji Iramba, kwa hiyo tunawadhulumu na hatuwatendei haki wananchi wa Iramba na Meatu wanakaribisha watu kutoka maeneo mengine. Wanapokea ushuru, unanufaisha Halmashauri ya Meatu. Sawa, sikatai lakini ninaomba taratibu zifuatwe. Iramba inaposema tunafunga ziwa hili, Meatu pia watangaze, wafunge! Pia ninaomba sana boti iletwe kwa ajili ya kufuatilia wale wavuvi haramu ambao hawana leseni na vibali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mkondo wa maji ambao umekuwa ukipitisha maji kwenda Kitangiri. Kata za Igunga wamekuwa wakilima kwenye mkondo ule kiasi kwamba inatishia Kitangiri kuondoka. Mheshimiwa Waziri naomba utakapoongea hapo utuambie unatulindia vipi Kiteka yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikimaliza Mkoa wa Singida mimi naomba niseme hivi, kuna suala la *operation linaloendelea*. Mheshimiwa Mpina una baba zako, una wadogo zako, una kaka zako, wote wako kwenye uvuvi, hata kama hujazaliwa nao kumbuka kila mtoto au kila mwanaume au kila mwanamke ni mtoto wa mwanamke aliyezaliwa na wanawake kama sisi. Ni hakika wale wavuvi hawatendewi haki. Mnapokamata zile nyavu unazichoma, kumbuka ameacha familia nyuma inamtegemea, kumbuka ana wazazi wake wanamtegemea, kwa nini usiende na utaratibu mzuri? Nyang'anya zile nyavu lakini lete mbadala wape nyavu nyingine, hata kama watalipia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli siungi mkono hiyo *operation* ni uchungu kwa sababu na mimi nina ndugu zangu wako kule. Kwa hiyo, naomba mnapochoma yale sijui makokoro, sijui kitu gani, naomba peleka nyavu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ameongea hapa Mbunge mmoja kwamba wasomi mliopo huko msifanye kazi kama watu ambao hamkwenda shule. Mheshimiwa Rais amewaweka hapo ili muwasaidie Watanzania na ili msaidie sekta hiyo. Kwa kweli hatuungi mkono uvuvi haramu, lakini ile *operation* namna mnavyoindesha kwa kweli haitendi haki kama binadamu wengine. Kwa hiyo, suala hilo naomba sana liangaliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo lingine hili la kuwabandika ng'ombe moto. Jamani, chuma cha moto kwenda kumbandua ng'ombe na kumfanya awe na kidonda. Mimi nimekutana na ng'ombe ana kidonda hakiponi. Naomba mtafute namna ya kuweka chapa wale

ng'ombe. Jamani, kwanza tunaharibu ile ngozi halafu ng'ombe anakonda. Naomba sana Mheshimiwa Mpina, wataalam wapo na mmesoma kwa kweli, tafuteni namna ya kutia chapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli, tunajua tunataka tudhibiti ng'ombe wanaotoka katika nchi jirani, lakini kwani mtu akisajili ng'ombe wake akasema Mheshimiwa Mlata ana ng'ombe 100, kesho mkimkuta ana ng'ombe 200 si atajieleza kawapata wapi? Tafuteni namna, basi wawekeeni hata vidani, wawekeeni kitu chochote wale ng'ombe jamani, tusiwatese jamani. Kwa hiyo, hilo mimi nilikuwa naomba liangaliwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, sisi tulikuwa tunapokea ng'ombe kutoka Meatu, Maswa, wanakuja pale Singida kupakia. Mabehewa yalikuwa yanapakia kupitia hii reli ya hapa Manyoni, lakini siku hizi usafirishaji wa ng'ombe umekuwa ni mgumu kwa sababu ile treni haiendi tena. Sasa sifahamu mna mawasiliano gani na sekta ya uchukuzi ili kuwapunguzia ng'ombe msafara mrefu, wengine wanafia njiani kwa sababu ile reli ilikuwa inarahisisha sana yale mabehewa kupakia ng'ombe wengi lakini na sisi Singida tulikuwa tunaweza kupata mapato. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, boresheni ranchi zenu, ukienda Kongwa kwa Mheshimiwa Spika, yale majani yanaota mpaka yanakauka, hakuna chochote kinachopatikana. Wekeni utaratibu mtu akiingiza ng'ombe mmoja mwambie kiasi fulani, mtu alete ng'ombe wake, alishe, kusanya hela, muwekee maji pale, alipie kama kuna matibabu, hebu fanyeni biashara kisomi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mlata. Msingi wa hoja yake, fanyeni mambo kisomi jamani. Siyo ngumi mkononi, siyo ng'ombe anachomwa na chuma cha moto, anachomwa kwenye paja namna hii mpaka anapata kidonda. Hata wazee wangu wa Kigogo wale wa zamani

walikuwa na namna ya kumtambua huyu ng'ombe wa nani, huyu ng'ombe wa nani. Hata sisi ukoo wetu tuna chapa ya kwetu wenyewe, lakini kwenye sikio sio kwenye paja. Sasa hawa ma-veterinarian wa leo hawa wanazidiwa na wale wazee wangu ambao hawakusoma hata ngumbaru. (*Kicheko/Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Saed Kubenea na mwisho atakuwa Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nina dakika kumi?

SPIKA: Ndio, dakika tano za kwako na tano za Mheshimiwa Anna Gidarya, dakika kumi.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme wazi baada ya mjadala kufungwa jioni, nitatoa taarifa kwa Kiti chako kwamba kwa kutumia Kanuni zetu nitaleta Hoja ya Kuundwa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza *Operation Sangara* yote ilivyofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina *square meter* zaidi ya 800 eneo la bahari, kutoka Mtwara mpaka Tanga, kutoka Pemba mpaka Mafia lakini eneo la uvuvi linachangia sehemu ndogo sana ya pato la Taifa letu kwa sababu hatujawekeza kabisa katika uvuvi. Wananchi wa Dar es Salaam sisi tunaishi kwa nyama, kuku na samaki lakini nchi yetu haiangalii kabisa katika eneo zima la nyama, hivi Tanzania inaagiza kuku, nyama na samaki kutoka nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ambayo tuna bahari ya kutosha, meli za nje zinakamatwa ndani, tunazitaifisha, tunapelekwa mahakamani, tunadaiwa fidia ya mabilioni, lakini sisi tunaagiza samaki kutoka nje, hii ni aibu! Ni aibu miaka 50 baada ya uhuru Tanzania yenyе bahari, maziwa na mito inaagiza samaki kutoka nje. Halafu Wabunge wa

CCM wanasimama hapa wanasema tutazuia bajeti, hakuna Mbunge wa CCM mwenye uwezo wa kuthubutu kuzuia bajeti, hayupo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama akiwepo na bajeti hii ikazuiwa, mshahara wangu wa mwezi huu nisilipwe, wapeleke kwenye majimbo ya hao Wabunge. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wa CCM mnakubali maneno hayo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kubenea endelea bwana. (*Kicheko*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nisilipwe. Hakuna Mbunge wa CCM anaweza kusimama katika maneno yake mpaka mwisho. Watapelekwa kwenye *caucus*...

SPIKA: Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Mwigulu amesimama hapo.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, alivyotaja mshahara nimeshtuka sana kwa sababu kumbukumbu zinaonesha ameukopea wote. (*Kicheko*)

SPIKA: Na mimi nashuhudia kwenye mafaili yangu Mheshimiwa Kubenea, sina hakika sana umebakiza kiasi gani? (*Kicheko*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nadhani ye ye ndiyo amekopa zote, mimi sijakopa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hiki kilichoandaliwa na Mheshimiwa Mpina, mimi namfahamu sana Mheshimiwa Mpina. Mwaka 2012 akiwa Mbunge alizua bajeti hapa, alikataa bajeti ya Serikali, leo Mheshimiwa Mpina anakaa kwenye Wizara, anachukua hela za wafugaji, anachukua hela za uvuvi, halafu harejeshi fedha kwa wananchi. Nashangaa nikimuona Mheshimiwa Mpina wa leo nikimuangalia na Mheshimiwa Mpina wa miaka saba

iliyopita, siyo huyu, siyo kabisa. Ni rafiki yangu, ni kaka yangu, tunaheshimiana lakini nikimuangalia yule Mheshimiwa Mpina wa miaka ile siyo huyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Kuna Sheria ya Hifadhi ya Bahari ya mwaka 1999, zaidi ya miaka 30 leo hajafanyiwa marekebisho. Wavuvi wetu katika maeneo ya pwani na visiwani, ukienda kule Mafia na Rufiji, utakuta eneo limetengwa kwa ajili ya hifadhi ya bahari lakini hifadhi ya bahari inaweka boyaa mita 100 inazuia wavuvi wasifanye kazi zao za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, leo uvuvi katika visiwa kama vya Mafia, Kware na Koma kwa Mheshimiwa Ulega, asilimia 99 ya wananchi wanategemea uvuvi. Pale Kware na Koma kwa Mheshimiwa Ulega wananchi hawalimi, wanategemea bahari lakini hifadhi ya bahari imeenda kuchukua maeneo ya bahari, imezuia wananchi wasivue, imeleta matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya maeneo Jeshi la Wananchi linatumika na hifadhi ya bahari kukimbiza wavuvi na kuzamisha boti za watu na kunyang'anya nyavu za watu, Jeshi la Wananchi. Nchi gani hii mnaongoza? Nchi hii tulionba uhuru ili wananchi wawe huru, wafanye mambo yao huru kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, baada ya kuwa huru Watanzania wamekuwa watumwa katika nchi yao. Wanazungumza Wabunge wa CCM hapa unaona uchungu, mnaenda kwenye uchaguzi kesho mtasemaje? Mtawaambia nini wananchi au ndiyo mtatumia dola na polisi kushinda? Hoja hizi za Mheshimiwa Bulembo hazijibiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jana kuna mtu ameniambia, sijui kama kweli, kwamba Waziri wa Mifugo anatoka Kanda ya Ziwa, hafahamu kabisa mambo ya Pwani. Mheshimiwa Ulega anatoka Mkuranga, lakini anatoka Kimanzichana, hata bwawa kwake hakuna. Mkurugenzi wa Uvuvi anatoka Kanda ya Ziwa. Sasa hiki kilio cha wananchi wa Pwani ambacho kilianza toka enzi za akina Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Ayoub Kimbau...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Aaaa. (*Makofi*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, dakika zangu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, pamoja na muda tulionao nitawaomba sana tuvumiliane. Kwa sababu ya muda wetu jinsi ambavyo umekuwa na ili twende vizuri, wachangie watu watatu tu ili tuweze kumaliza kwa haraka haraka, lakini hawa watatu nitawapa dakika tano-tano. Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Joseph Ngonyani na Mheshimiwa Richard Ndassa. Mheshimiwa Bilakwate kwa dakika tano.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uhai na nguvu za kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya kuendelea kuijenga nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu hii *operation* inayoendelea. Mheshimiwa Mpina mimi naamini unafanya kazi nzuri na historia yako kila mmoja anajua. Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mengi niombe uyazingatie.

Mheshimiwa Spika, *operation* hii ulianzisha kwa nia njema lakini naamini kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge baadhi ya watendaji wako wanakuangusha. Wana nia mbaya ya kutaka kuharibu lile zuri ambalo umeliandaa ili lisiweze kufanikiwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina ushauri wangu ninaokushauri, hebu fuatilia maoni ya Wabunge, baadhi naamini ni mazuri yanaweza kukusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini jambo lingine ambalo napenda kulisema kwa Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa na hoja zinajitokeza hapa Bungeni, linapotoka jambo linafanyika Mheshimiwa Mbunge anasimama anasema wapiga kura wangu. Mimi nikuombe Mheshimiwa Mpina, simamia sheria, fuata taratibu, kile ambacho kinamgusa mwananchi ambaye hakufuata taratibu lazima twende kwenye mstari ulio sahihi. Nchi hii imefika hapa tulipo, mimi ninalisema hili, mimi ni mwanasiasa, lakini mambo mengi yamechangiwa na wanasiasa. Hata kama mtaona ni baya lakini wanasiasa tumehusika kuharibu nchi hii. Ukitaka kugusa hapa wanasema wapiga kura, ukitaka kugusa hapa hao watu wangu, mambo mengi ambayo yameharibika sisi ndiyo tumesababisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimshauri Mheshimiwa Mpina jambo lingine, hili suala la ng'ombe kuchomwa moto kwa kweli siyo zuri. Hata kule kwangu nina ng'ombe wengi lakini wengine wana vidonda, yaani unajaribu kujuliza hivi hawa ni wataalam ni watu gani ambao wametoa ushauri huu? Hili jambo sio sawa, angalia namna nyingine ambayo mnawenza kuwatambua hawa ng'ombe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nikushauri Mheshimiwa Mpina, yako maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya wafugaji Iakini yamevamiwa. Kule kwangu kuna eneo limetengwa na Serikali likapewa *GN. No. 620*ya mwaka 1987, eneo hili limevamiwa, wameingia watu wenye pesa, wameingia mpaka wengine kutoka nje ya nchi, wafugaji hawana pa kufugia wanahangaika. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mpina ulifuatilie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Innocent. Mheshimiwa Joseph Ngonyani na Mheshimiwa Richard Ndassa ajiandae.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, naamini ulikuwa unamaanisha Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

SPIKA: Wameniandikia Joseph, endelea Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii na nikushukuru kwa fursa uliyonipa. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii asilimia miamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la upigaji chapa kwa sababu muda wenyewe ni mfupi. Kule kwangu Namtumbo nimepata malalamiko mengi sana ya wallopigiwa chapa. Chapa imepigwa na kuna *data/taarifa* fulani katika kile chuma wanachopigia chapa, lakini kila chapa iliyopigwa ng'ombe wale wameendelea kutibiwa na hakuna takwimu yoyote inayonekana katika ile chapa zaidi ya kidonda. Kwa hiyo, hata utambuzi kwamba huyu ng'ombe ni wa Wilaya fulani haupo kutokana na namna chapa ya moto ilivyokuwa inapigwa zaidi ni kidonda tu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kwamba njia inayotumika katika kupiga chapa siyo sahihi. Naomba kabisa jambo hilo lirekebishwe, itafutwe njia nyingine ya kuwatambulisha ng'ombe lakini siyo kuwachoma moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kwetu sisi Namtumbo eneo letu ni dogo sana, zaidi ya asilimia 67 ni hifadhi, tumeletewa ng'ombe kupita kipimo. Ng'ombe wamekuja wengi sana na matokeo yake wameleta ugomvi mkubwa sana kwa wale wakulima ambao sehemu kubwa ya Wana Namtumbo ni wakulima zaidi ya asilimia 90, inaleta ugomvi mkubwa sana. (*Makofi*)

Mimi sielewi, sijui kwa nini wafugaji hawatofautishi kati ya mpunga na magugu. Wanasema haya ni magugu, hizi ni nyasi, wakati ule ni mpunga. Wanasema hizi ni nyasi wakati yale ni mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana Namtumbo hatuna eneo, wale ng'ombe ambao wameingizwa naambiwa

kwamba walijazwa kwenye hifadhi, kwa hiyo walikuwa wanakula kwenye hifadhi hakukuwa na ugomvi. Kwa maana nyingine ng'ombe wengi walikuwa wanakula ndani ya hifadhi na wakulima walikuwa wanalima eneo lao. Sasa wale ng'ombe wameondolewa kwenye hifadhi wanakwenda wanavamia eneo la wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana tena sana mtusaidie kutatua tatizo hili. Njia pekee ya kutatua tatizo hili ni kuwaondoa wale ng'ombe au turuhusu wale ng'ombe waendelee kukaa ndani ya hifadhi kwa sababu sisi wakulima hatuingii kwenye hifadhi. (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Ngonyani. Mheshimiwa Ndassa kwa dakika tano, malizia wewe ni wa mwisho.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nimwombe sana Waziri wa Fedha pamoja na Waziri Mpina waangalie suala la usindikaji wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 tulisindika jumla ya ngozi 1,000,215 ambazo ziliipatia Serikali shilingi bilioni 34.7; mwaka 2017/2018 ikashuka ikaenda mpaka vipande 292 iliyozalishia shilingi bilioni 3.2. Kutoka kwenye shilingi bilioni 34 mpaka shilingi bilioni tatu, sasa tatizo ni nini? Hebu Serikali mkae kwa sababu ng'ombe ni haohao, tatizo ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutoka shilingi bilioni 34 mpaka shilingi bilioni 3 kwa mwaka mmoja na sisi Serikali tunatafuta pesa ili zikafanye kazi nyingine. Niombe sana Wizara ya Fedha kama liko tatizo la tozo au *export levy*, hebu mkae na mtazame kwa sababu tunapoteza mapato mengi sana. Inawezekana ngozi hizi badala ya kupitia kwenye utaratibu wetu mzuri zinapitia Kenya na Uganda, hebu litazameni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nishauri sana, ukitazama kelele zote hizi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wanaosababisha hasa ni wataalam wetu, wanatuangisha mno. Bajeti zote ukisikiliza, kwa sababu wana tabia nzuri sana ya kusema kwamba aah, Mawaziri si wa kupita tu, walishapita wangapi hapa bwana, hawa ni wapitaji tu hawa, kwa hiyo, wanafanya mambo yao. Sasa kwenye haya ndugu zangu naomba tubadilike kwa sababu kelele hizi siyo zetu sisi peke yetu humu, ni mpaka na wapiga kura wetu huko. Kwa hiyo, niombe sana wataalam wetu maana hata ukitazama hiki kitabu, kimesemwa na wenzangu hapa, Mheshimiwa Ulega kakamata lile chuma anachoma ng'ombe ambaye hajawahi kufuga ng'ombe hata mbuzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukija ukurasa wa mwisho wa kitabu chao, mtaalam ambaye ni daktari wa mifugo, Dkt. Maria na yeye kakamata chuma anambabua huyo ng'ombe. Tunataka kuuza ngozi, sasa mnaharibu ngozi. Kwa nini usitumie utaratibu wa kuchukua *tag* mkatoboa sikio, ndio utaratibu wa nchi zote duniani, mimi sijaona duniani wanachukua chuma wanamtoboa ng'ombe kwenye mapaja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niombe sana wataalam wetu mliangalie hili. Mheshimiwa Mpina, tunajua wewe ni mchapa kazi mzuri sana, mdogo wangu, fuata mambo mawili katika maamuzi yako, pamoja na sheria, tumia busara na hekima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa. Anachokwambia Mheshimiwa Mpina *lekagadoho*. (*Kicheko*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi haramu, jambo hili ni vyema likatolewa tafsiri sahihi vifaa ndio haramu au watu ambaao ndio wavuvi ndio haramu

kulingana na mkanganyiko uliopo katika maeneo mengi nchini na suala la kukomesha lifuate taratibu, sheria na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchomea wavuvi nyavu; utaratibu wa kutokomeza uvuvi haramu muafaka wake sio kuchoma nyavu kwani kwa kuchoma nyavu ni kusababisha wavuvi kupata umaskini pia jambo hili linatakiwa kudhibitiwa viwandani na sio ziwani au bandarini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tozo za kero kwa wavuvi, ni vyema Serikali ikapitia tozo zote ambazo ni kero kwa wavuvi wetu kwani suala la uvuvi nalo linachangia pato la Taifa letu na pia kupata kitoweo kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la utaratibu mbovu wa kusafirisha mifugo, kulingana na changamoto wanazokutana nazo wafugaji, mfugaji anapokuwa anatoa na kupeleka mifugo yake mnadani hata kama ni wachache wanamtaka kusafirishwa kwa gari (lori sio sawa).

Mheshimiwa Spika, leseni ya wavuvi itolewe moja kwa moja kwa kila ziwa au bahari. Jambo hili limekuwa na changamoto kwa wavuvi kwani kwa sasa leseni zinatolewa kwa kila Halmashauri jambo ambalo ni gumu kwani samaki wanahama kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la *operation* zinazoendelea zinaleta madhara makubwa sana kwani haifuati haki za binadamu, haki za wanyama pamoja na kupeleka migogoro.

Mheshimiwa Spika, mifugo mingi inayokamatwa haipewi matunzo mazuri kama vile chakula na maeneo ya kutunzia inakuwa sio rafiki na kusababisha mifugo hiyo kufa na kusababisha maumivu kwa mfugaji.

Mheshimiwa Spika, kutopelekwa kwa pesa ya maendeleo, hakuna shughuli yoyote inaweza kufanyika bila

kupeleka fedha iliyotengwa kwenye eneo husika ili kazi ilivyokuwa imetengwa ikienda kwa wakati ni rahisi kumaliza changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji ili kuondokana na migogoro iliyopo katika nchi yetu.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kuchangia Wizara hii muhimu sana tena sana kwa mustakabali wa nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla. Jimbo la Kigoma Kusini lina vijiji 61, kati ya hivyo vijiji 34 viko kwenye Ziwa Tanganyika, wavuvi wanategemea uvuvi ndio wamudu maisha yao. Lakini tuna tatizo kubwa sana tena sana, Idara ya Uvuvi Mkoa wa Kigoma tuna mwanamama pale ambaye ni Afisa Uvuvi Mkoa amekuwa kikwazo kikubwa sana kwa wavuvi. Kwanza hatol ushirikiano wowote kwa wavuvi, pili amekuwa ni mtu wa kuwakwamisha wavuvi kwa kuwatoza pesa ili wamtetemekee, wanaokataa wanachukuliwa hatua kwa visingizio vya kukosea sheria za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano wa Taasisi ya Tuungane iliyopo Kata ya Buhingu, Kijiji cha Mgambo. Taasisi hii hajulikani ina vibali gani kwa kusimamia masuala ya uvuvi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza wamekuwa ni kero kubwa kwa wananchi maeneo yote yenye dagaa na samaki wa kutosha, wao ndio wanayachukua na kuvua, lakini ukiwauliza wanadai wanalinda samaki wadogo ili wasivuliwe mapema.

Mheshimiwa Spika, tunae mdau namba moja anaitwa Amadi Saidi, ni Mtanzania wa kuzaliwa. Yeye na wazazi wake pale Buhingu na mimi pia nina undugu naye, lakini alichukua uraia wa Abu Dhabi, lakini ni mvuvi mkubwa. Tuombe Wizara imsaidie kumpatia vibali vya uvuvi vyote kwani kufanya kwake kazi ya uvuvi katika Kata ya Buhingu kuna manufaa makubwa sana, amejenga Kituo cha Polisi, amejenga madarasa, amenunua madawati ya shule za Kata ya Buhingu.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja/alitembelea na kuona kazi kubwa anayofanya Ndugu Amadi Said. Naomba pia Wizara itupati nyavu za ruzuku, mashine za maboti za ruzuku na ikiwezekana tupatiwe na maboti ya kuvulia samaki au kama Wizara inatoa mikopo ya wavuvi basi, sisi tupatiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunao mwalo umejengwa Kata ya Mwakizega, Kitongoji cha Muyoboz ili wavuvi waongeze thamani ya mazao yao ya uvuvi, nimuombe Mheshimiwa Waziri amshawishi Mheshimiwa Waziri Mkuu ili atakapokuja kufanya ziara Mkoa wa Kigoma mwezi wa Julai, 2018 basi huu mradi wa mwalo ufunguliwe rasmi kwani mwaka umekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunashindwa kupata soko zuri la ngozi kwa sababu ya ng'ombe kutotunzwa vizuri, kitendo cha kupiga mihuri ng'ombe ni kuzidi kuharibu soko la ngozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokomeza na ukomeshaji wa uvuvi haramu uje na mbinu na vifaa mbadala kwa wavuvi kwani hawa watu hiki ndio kimekuwa kipato chao kwa maisha yao yote.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini juu ya faini wanazotozwa hawa watu wanaokamatwa kwa makosa mbalimbali ya uvuvi haramu. Lazima hizi *penalty* zithibitishwe na sheria ya Bunge kwa kuwa zina sura ya kukomoana, lakini pia na *double standards*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipata wapi ujasiri wa kuchoma vifaranga vidogo kiasi kile kutoka Kenya kwa madai ya uingizwaji kiholela? Kwa nini hawakurudishwa Kenya? Huu ni unyama na ni kinyume na haki za wanyama. Wizara ya Mifugo inapaswa pia kulinda haki za wanyama,

kweli Wizara yako ililitia doa Serikali hii na kutufanya Watanzania tuonekane watu wa hovyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa samaki hawawezi kuzuiwa kutoka eneo moja kwenda na zoezi la uvuvi haramu limewekewa mkazo eneo la Tanzania Serikali/Wizara itueleze ni kwa kiwango gani kampeni hii inafanyika Kenya na Uganda kwa kuwa tunaweza kuwabana wafugaji wetu wakati Kenya na Uganda wanaendelea kuvuna.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie machache katika hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Same Mashariki lina wafugaji wengi ambaao bado wanafuga kienyeji. Wafugaji hawa walishatenga eneo kubwa kwa ajili ya kufanyiwa shamba darasa la jinsi ya kufuga kisasa na kupanda majani ya mifugo. Wilaya ya Same ina eneo takribani ekari 300,000 ambalo linafaa kwa ufugaji. Hivyo naomba Waziri awaeleze wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, ni lini wataalam watafika jimboni hapo kuanzisha shamba darasa? Jambo hili nimeshapeleka ombi kwenye Wizara hii na Mheshimiwa Naibu Waziri Ole-Nasha alifika jimboni humu mwaka jana, lakini akashindwa kuwatemeblea wafugaji hawa waliokuwa wamejiandaa sana kuonana naye.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili Jimboni Same Mashariki kuna bwawa kubwa lenye eneo la kilometa za mraba 24. Ziwa hili limejaa udongo na hivyo hata samaki hawawezi kuzaliana.

Mheshimiwa Spika, *UNCDF* walikuwa tayari kuanzisha mradi mkubwa kwa kutumia cages. Maandalizi yote yalikwishafanyika pamoja na kuweka muundo wa *PPP*, Halmashauri ya Wilaya ya Same ikishiriki kikamilifu. Lakini kutokana na tatizo hili la tope kujaa bwawani, wafadhilli wanajaribu kuona jinsi ya kutengeneza mabwawa ya samaki nje ya Bwawa hili la Kalemawe lililoko Kata ya Kalemawe, Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mito ya Hingilili na Yongoma inatiririsha maji yake kwenye hili Bwawa la Kalemawe, kutolitumia ni hasara kubwa kwa nchi yetu maana matokeo yake bwawa hili litakufa.

Naomba Waziri akihitimisha hoja yake anieleze jinsi atakavyoweza kusaidia ili bwawa hili lenye samaki linaweza likatolewe tope ili liweze kuleta kiwanda cha kuchakata samaki. Ahsante.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi. Hata hivyo, fursa nyingi hazitumiki vizuri na wananchi wa ngazi ya chini yaani wananchi wa kawaida wanashambuliwa badala ya kuelemishwa. Maafisa waliopewa dhamana ya kulinda na kusimamia sheria wameondoka kuwa binadamu na sasa wanapomkuta binadamu anatumia rasilimali hii, kwa namna ya makosa haelimishwi badala yake ananyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, nashauri elimu ikitolewa vizuri binadamu atakuwa mlinzi mzuri wa rasilimali za majini. Tabia ya kuwashambulia, kuwaka na kuwatesa sababu ya samaki wawili/watatu si sawa. Walitoka wapi hawa, wanaagizwa na nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji wa samaki haujajonesha kama ni kipaumbele, naomba Wizara ijitahidi kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, Ranchi za Taifa, Nkasi tunayo *Kalambo Ranch*, haina mtaji wa kutosha na mifugo iliyopo ni michache sana. Ranchi ni kubwa lakini mifugo ni michache na hakuna mtaji na miundombinu mingine ya kuimarisha ufugaji. Ranchi haina gari, watumishi wachache na vilevile haitengewi bajeti ya maendeleo na Serikali ili kuboresha ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo kwa wavuvi, katika Jimbo la Nkasi Kusini wavuvi hawajapata mikopo ya kuboresha uvuvi na hivyo uvuvi unaoendeshwa ni wa kizamani sana na hauna tija.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki, naishauri Wizara kutenga bajeti kuwasaidia wananchi wa Kata za Ninde, Kizumbi, Wampembe na Kala walioko kandokando ya Ziwa Tanganyika, waelimishwe namna ufugaji wa samaki ili kunusuru maisha yao kwani *operation* zinazoendelea wananchi hawa wanatii sheria na katazo la Serikali.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ya kupeleka mbele maendeleo ya nchi yetu. Nampongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Baraza lote la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba hii ya bajeti na kazi kubwa anayofanya yeye na Naibu wake kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie hoja ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara izingatie umuhimu wa kuongeza bajeti ya kutekeleza vipaumbele vya sekta ya mifugo kama vile upatikanaji wa maji, majosho, dawa, tiba na masoko.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bei ya mifugo kuyumba kila wakati kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa hususan katika Wilaya za Kaskazini Mashariki kwa nchi yetu ikiwemo Longido, Monduli, Simanjiro na Ngorongoro, naomba Serikali kupanga bei elekezi ya kuuza mifugo kwenye masoko yetu kama mazao mengine mfano zao la pamba na korosho ambazo hupangiwa bei kwa kilo.

Ng'ombe nao wapangiwe bei kwa kilo kwa ng'ombe hai na nyama ili wafugaji wapate tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko/minada inayoanzishwa mipakani na Halmashauri za Wilaya kama soko la Halmashauri ya Wilaya ya Longido lililopo Eorendeke. Soko hili libibuniwa na Halmashauri kwa makusudi ya kuinua mapato ya ndani ya Halmashauri na kuwapatia wananchi mnada wa uhakika na kuuza mifugo kwa faida ili kuinua kipato chao. Kwa kuwa Wizara imejitokeza na kuja kunyakua mnada wa Eorendeke na ninatambua kuwa pia Serikali Kuu inahitaji kodi, nashauri Serikali ichukue tu asilimia ndogo ya kodi na kuwaachia Halmashauri ndio wenyewe jukumu kubwa la kuendelea kuimarisha na kusimamia wafanyabiashara ili mnada/soko la mifugo la ndani liimarike.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda vyta kuchakata bidhaa za mifugo, napenda kuishauri Serikali iwakopeshe wananchi ili waweze kuanzisha viwanda vidogo vyta usindikaji maziwa, nyama na ngozi na pia Serikali ifufue viwanda viliwyokuwepo kwa mfano Kiwanda cha Maziwa kilichotolekezwa na mwekezaji Longido. Kwa kufanya hivyo wananchi watanufaika na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishauri Serikali ianzishe kiwanda kikubwa cha ngozi pamoja na mazao yote ya mifugo na kuwa na viwanda vidogo katika mikoa yote ya wafugaji. Ngozi ni bidhaa ya thamani sana kwa mfano Ethiopia ngozi zina bei kubwa ndani na nje ya nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa linalowakabili wafugaji la kupoteza mifugo kutohakana na kula mifuko ya plastiki. Licha ya mifuko hii ambayo imetapaka kila mahali katika nchi yetu kuchafua na kuharibu mazingira, mifugo wengi wanaangamia wakati wa kiangazi na kula karatasi hizo za plastiki. Naomba kuishauri Serikali ipige marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki katika nchi yetu. Rwanda na Kenya majirani zetu wao wamepiga marufuku na wamefanikiwa, sisi pia tuige mfano wao.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu mnada wa mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido iliyo Kijiji cha Eor Endeke Longido, mnada huu umejengwa kwa juhudzi za Halmashauri bila msaada kutoka Wizarani. Lengo la mnada huu ulio karibu na mpaka wa Kenya na Tanzania katika eneo la Namanga lilijengwa kwa kusudi la Halmashauri kujiongezea mapato ya ndani na wananchi kupata soko la mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, leo hii kuna kero kubwa imejitokeza baada ya Wizara kuja kuingilia mnada huo na kupanga kodi kubwa ya ushuru wa Serikali wa shilingi 20,000 kwa ng'ombe na shilingi 5,000 kwa mbuzi na kondoo. Kodi hii si rafiki kwa wananchi na hali hii imewakatisha tamaa na kupelekea kuanza kurudi tena kuitishia mifugo maporini kuvusha Kenya ili kuendeleza biashara zao. Hivyo kupelekea Serikali Kuu na Halmashauri kupoteza mapato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, naomba kuishauri Wizara na Serikali izingatie kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ipunguze kodi kwa kushauriana na wananchi, itoe huduma za *export permit* palepale mnadani badala ya kwenda hadi Arusha au Wizarani. Wizara ya Mifugo wakae na Halmashauri waafikiane jinsi ya kuendesha mnada huu ili uweze kuleta tija kwa wananchi, Halmashauri na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho wajasiriamali wa mifugo (wachuuzi) na wananchi wa Longido wanaiomba Serikali yetu siku iwayatafutie soko la ndani la uhakika kwani wasingetamani kupeleka mifugo kwenye minada na masoko ya nchi jirani kama siyo ni kutokana na kutokuwepo mnada wenye bei nzuri nchini ukilinganisha na nchi ya jirani.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya wafugaji waliopoteza ardhi kwa ajili ya uwekezaji na uhifadhi; mfano wa mashamba yaliyoko Kanda ya *West Kilimanjaro*, wafugaji walikuwepo *West Kilimanjaro* kabla ya Bara la Afrika kugawanywa na wakoloni mwaka 1884. Wajerumani ndio

wakoloni wa kwanza kuitawala Tanganyika na ndio waliowatoa wafugaji kutoka katika nyanda za juu zenye rutuba, mvua za uhakika, malisho na maji kwenda katika maeneo ya mbugani ambayo ni makavu na yasiyo na maji wanapoishi hadi leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1945 Serikali ya Uingereza baada ya kukabidhiwa koloni la Tanganyika na Umoja wa Mataifa wakati huo ukiitwa *The League of Nations*, waliwazawadia wanajeshi waliopigana Vita ya Pili ya Dunia yale maeneo. Wafugaji wakaendelea kubaki bila ardhi yenye maji na malisho ya mifugo yao nyakati za kiangazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1968 baada ya Serikali kutangaza Azimio la Arusha na kutaifisha yale mashamba, Rais wa Tanzania Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Mungu ampe heri ya milele) alipotembelea Wilaya ya Maasai kama ilivyojulikana wakati huo alisikitika alipobaini kuwa wafugaji hawana ardhi inayofaa kwa malisho na maji ya mfugo yao nyakati za kiangazi. Akaagiza wapewe ekari 5,500 kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. Tarehe 13/3/1973 Bunge lilitidhia wafugaji kurudishiwa hizo ekari 5,500 na tarehe 16/3/1973 Serikali ilitenga rasmi ekari 5,500 za malisho kuititia *GN No. 59*.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* ilipopitisha *operation* ya kubaini na kuweka alama mipaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro miaka ya karibuni eneo hilo lilijumuishwa katika Hifadhi ya *KINAPA (Kilimanjaro National Park)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri na kuiomba Serikali iwave wafugaji hawa ardhi mbadala katika mashamba pori ya *NDC*, *NARCO* na *NAFCO* yaliyoko katika ukanda huo wa *West Kilimanjaro*.

Mheshimiwa Spika, aidha kuna mashamba mawili ambayo matumizi yake yamekuwa yasiyo na tija, hususani *West Kilimanjaro Ranch* yenye jumla ya ekari 95,000 na ng'ombe wa *NARCO* wasiofika 200 na *Endarakwai Ranch*

yenye ekari 11,000 ambayo mwekezaji mmoja wa kiingereza, Peter Jones, analitumia kufugia wanyamapori na mifugo hawaruhuswi kuingia.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1982 Rais wa Awamu ya Kwanza, Hayati Mwalimu Nyerere alimwagiza aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Hayati Edward Moringe Sokoine (apumzike kwa amani) kuanzisha Ranchi ya Jamii ya Larkarian. Ardhi husika ilainishwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa wakati huo, Hayati Sokoine aliwahamasisha wafugaji wakachanga mitamba 1,500. Lakini baada ya kifo chake, mradi wa Ranchi ya Jamii nao ukafa. Baada ya Hayati Sokoine na Mradi wa Ranchi ya Jamii kufa, wawekezaji wakapewa ardhi hiyo ambayo inajumuisha mashamba nane yafuatayo; *Ndarakwai Ranch, Roselyn Farm, Tilonga Farm, Simba Farm, Mountain Side Farm; Engushai Farm, Mawenzi Farm* na *Leghumushira Farm*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa baadhi ya mashamba haya yamekuwa mashamba pori. Kwa hiyo, naomba kuishauri na kuiomba Serikali iwarejeshee wafugaji wa Kanda ya *West Kilimanjaro* ardhi hiyo au wepewe mbadala kwa ajili ya shughuli zao za ufugaji na hasa kufufua Mradi wa Ranchi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, *Ndarakwai Ranch* yenye ukubwa wa ekari 11,000 ilikuwa ni mojawapo ya maeneo muhimu ya jamii ya Kimasai ya kulisha mifugo yao hadi wakoloni walipojimilikisha. Ni baada ya Azimio la Arusha mwaka 1967 ndio Serikali ilitaifisha shamba hili na kuikabidhi *TBL*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992 *TBL* ilibinafsisha shamba la Endarakwai kwa Kampuni ya *Tanganyika Film and Safari Outfitters* inayomilikiwa na Bwana Peter Jones, raia wa Uingereza. Mwekezaji huyu aligeuza shamba hili kuwa pori la kufugia wanyamapori na amekuwa na ugomvi mkubwa na wafugaji wanapajaribu kwenda kulisha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa *West Kilimanjaro* wanaiomba Serikali iwarejeshee ardhi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kutoa kilio cha wafugaji, wafugaji wana matatizo mengi lakini kubwa zaidi ni la kunyang'anya ardhi yao ya asili katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ikiwemo eneo hili la *West Kilimanjaro* nililojadili, Serengeti, Tarangire, Mkungunero na maeneo mengine mengi ndani ya nchi yetu. Maeneo haya yalibadilishwa kuwa ya matumizi mengine yenye maslahi mapana kwa Taifa lakini tatizo ni kuwaacha wenyiji bila ardhi inayofaa ya mbadala kwa malisho na maji ya mifugo yao na watu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi ichukue hatua za kizalendo na watatue migogoro ya ardhi ya wazawa iliyotwaliwa kwa jina la uwekezaji na kugeuzwa kuwa mashamba pori yasiyo na faida kwa Serikali wala wananchi na badala yake, yamekuwa chanzo cha uflisi kwa wafugaji maskini ambao kila wanapokanyaga mashamba pori hayo wakitafuta malisho na maji wakati wa kiangazi wanakamatwa, wanapigwa na kutozwa faini kubwa zinazozidi kuwakandamiza kiuchumi na kuwaacha katika umaskini mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu ya kuwatumikia wananchi wangu wa Kyerwa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii muhimu kwa kazi nzuri na hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa; ni nzuri ingawa baadhi ya watendaji wenyewe nia mbaya wamegeuza baadhi ya hatua za kupambana na uvuvi haramu kuwa biashara ya kujinufaisha na uvuvi kuichafua Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kusimamia vizuri sekta ya mifugo na uvuvi ili tuweze kuongeza kipato kwa Serikali yetu. Ni jambo la kusikitisha nchi yetu ina mifugo mingi, tuna maziwa na bahari zimetuzunguka, lakini hatuoni faida inayolingana na kile tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa kama yatima, hawana mtetezi yejote. Hata pale wanapotengewa maeneo wamekuwa wakinyang'anya, wamekuwa ni watu wa kutangatanga. Kule Kyerwa miaka ya 1987 Serikali ilitenga eneo la Sirina, Ibada 1 na Rutifa Katabe kuwa maeneo ya wafugaji na yakatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kupewa *GN 620*. Hata hivyo maeneo haya inatafsiriwa wameingia na kujimilikisha kwa kuwahonga baadhi ya watumishi wabaya na leo hii wafugaji wananyanyasika na ng'ombe, akiingia kwenye maeneo yao walijoyapora ng'ombe wanatozwa faini ya pesa nydingi na wengine kuwakata mapanga.

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana katika hili Mheshimiwa Waziri aingilie kati kuwaokoa wafugaji wa Kyerwa ambao wamenyang'anya na kuonewa miaka mingi, wanahangaika kwa kutangatanga bila kupata msaada wowote.

Mheshimiwa Spika, niko tayari kutoa ushirikiano kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu jambo hili limekuwa kero ya miaka mingi. Kila kiongozi anayekuja ananunuliwa lakini mimi sinunuliwi kwa gharama yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nimitakie Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mafanikio katika vita hii ambayo watakutana na vipingamizi vingi, tunawaombea kusonga mbele mungu akiwa upande wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mungu kwa kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu inayoongoza kwa idadi kubwa ya mifugo Barani Afrika. Bahati nzuri Wizara hii inachangia 4.4% ya pato la Taifa. Pamoja na kuwa na mifugo mingi bado haijitoshelezi mahitaji ya ndani na nje ya nchi mfano:-

NA.		FAO	TANZANIA
1.	Nyama	50kg yr	11kg/yr – 0.03
2.	Maziwa	200 ltr/yr	45 ltr /yr– 0.013
3.	Mayai –	300/yr	72/yr – 0.2.

Mheshimiwa Spika, FAO inataka kila Mtanzania atumie kilogramu 50 ya nyama kwa mwaka, lakini anatumia kilogramu 11 ya nyama kwa mwaka. Pia kila Mtanzania anatakiwa kunywa maziwa lita 200 kwa mwaka lakini anakunywa lita 45 tu kwa mwaka. Hata hivyo, kila Mtanzania anatakiwa ale mayai 300 kwa mwaka lakini anakula mayai 72 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, viwango halisi vinavyotakiwa kuzalishwa ni kama ifuatavyo:-

NA		FAO	TANZANIA - UZALISHAJI
	Nyama	$50 \times 50,000,000 \text{ (peoples)}$ = $2,500,000,000 \text{ kg/yr}$	$550,000,000 \text{ kg/yr}$
	Maziwa	$200 \times 50,000,000 \text{ ltrs}$ = $10,000,000,000 \text{ ltrs}$	$2,250,000,000 \text{ ltrs}$
	Mayai	$300 \times 50,000,000$ = $15,000,000 \text{ /yr}$	$3,600,000,000$

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa FAO, Watanzania 50,000,000 kila mmoja anatakiwa kula 50 kg ya nyama, kwa hivyo Tanzania inatakiwa kuzalisha $2,500,000,000 \text{ kg/yr}$. Hata hivyo kwa mujibu wa FAO kila Mtanzania anatakiwa kunywa maziwa lita $10,000,000,000 \text{ yr kwa mwaka}$. Pia kuhusu mayai, FAO wanataka Watanzaia 50,000,000,000 watumie mayai $15,000,000,000$ kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hivyo Tanzania inazalisha mayai $3,600,000,000$ kwa mwaka kwa mfano hai ni dhahiri kabisa kwamba mahitaji ya uzalishaji ni mdogo mno kulingana na mahitaji mengine. Kwa hiyo basi mambo yafuatayo ni lazima yazingatiwe:-

1. Kuzingatia ufugaji wa kitaalamu.
2. Kuwawezesha wafugaji kutunza mifugo yao kibiashara.
3. Kuimarisha malisho ya uhakika hasa wakati wa kiangazi.
4. Kuimarisha matibabu kwa mifugo yote nchini.
5. Kutenga maeneo maalum ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, hii itawezesha kuongeza kipato na pia kuongeza uzalishaji ili kutosheleza mahitaji ya watanzania lakini pia kuongeza pato la Taifa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa sekta hii kuanza na sekta ya uvuvi. Sekta hii hajapewa msukumo wa kutosha kwani hadi leo bado Taifa linaagiza samaki kutoka nje. Pamoja na kuwa ubora wa samaki wa kutoka nje wanatiliwa mashaka, hadi leo hakuna uwekezaji wa kibiashara katika sekta ya uvuvi kwani hadi sasa hakuna meli kubwa ya uvuvi hasa kwenye bahari kuu wala hakuna kampuni yoyote ya sekta binafsi kuonesha uwezo wa kumudu kuingia kwenye sekta ya uvuvi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na maji ya kutosha, ya bahari na maziwa makuu, bado tunaagiza samaki na mazao ya samaki toka nje ya nchi. Tumechoka na samaki wabovu kutoka China, samaki vibua.

Mheshimiwa Spika, ni ipi sera ya Serikali ya Awamu ya Tano juu ya Wizara hii? Kama hakuna fedha za maendeleo zinazopelekwa kwenye Wizara hii pamoja na kuonekana kukusanya vizuri maduhuli ya Serikali bado hata hizo fedha wanazokusanya wenyewe Wizara ya Fedha hawataki kurudisha fedha hizo kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ni jambo lisiloleweka kuona Taifa lenye rasilimali za bahari, maziwa na mifugo ya kutosha bado tunaagiza samaki, nyama na maziwa toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uvuvi haramu unachangia kwa kiasi kikubwa na utendaji mbovu wa watendaji wa Wizara hii kwani si sawa sawa kunyang'anya nyavyu baharini, ziwani badala ya kwenye vyanzo vya vifaa au zana hizo zinazoitwa

haramu, je, wavuvi wanapata wapi zana hizo? Kwa nini Serikali inashindwa kusimamia uingizajiwa zana hizo haramu badala ya kuwapa hasara wavuvi kwa kuchomewa zana zao?

Mheshimiwa Spika, mifugo sasa nchini inaelekeea kuwa balaa badala ya neema kwani hakuna utaratibu wa kueleweka juu ya namna bora ya ufugaji wala namna bora ya uvunaji wa mazao ya mifugo ikiwemo nyama, maziwa, ngozi na mayai. Wafugaji wetu bado ni wafugaji wa kienyeji wa kuhamahama bila kujali Taifa linapata nini juu ya wingi wa mifugo ambayo kwa uhalisia inatuletea migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora wenye tija bado ni ndogo sana. Hivyo, Wizara inatakiwa kuwekeza zaldi kwenye elimu ili watu wafuge kwa tija. Hivyo kuweza kujitosheleza kwa kuwa na viwanda vyta kutosha katika kuongeza thamani kwenye mazao yanayotokana na mifugo. Hakuna uwekezaji wa kutosha katika sekta ya mifugo juu ya uchakataji wa mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Wizara haioneshi mipango wala dira ya kutupeleka kwenye ufumbuzi wa changamoto zilizo kwenye Wizara hii, kwa sababu kutokupelekewa fedha za maendeleo kunaonesha wazi kuwa hakuna dhamira ya kutatua changamoto za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kutawanya mifugo nchi nzima hakuwezi kuwa ni njia bora ya kukabiliana na changamoto hizo, tumeamua kusambaza mifugo kama tulivyoamua kusambaza mazao ya kilimo, jambo hili tusipolichukulia hatua kwa makini tunakwenda kuifanya Tanzania ya jangwa kwa kuondoa uoto wa asili wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji miradi ya uchimbaji wa malambo, mabwawa na maeneo ya minada hasa kwa mikoa ile ambayo si ya wafugaji kwa asili, mikoa kama ya Lindi na Mtwara bado hakuna malambo, mabwawa wala maeneo ya minada. Jambo hili linafanya mikoa hiyo kutopata

faida ya mifugo hiyo kwani hakuna faida ya moja kwa moja kwa jamii kwa kuhamishia mifugo hiyo. Serikali inapaswa kutafuta wawekezaji wa ndani na nje ili kunusuru sekta hii na kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, maafisa mifugo ni tatizo lingine kwenye sekta ya mifugo, mfano;- Mkoa wa Lindi si Mkoa wa wafugaji. hivyo, idadi ya maafisa mifugo haikuwa kipaumbele, lakini kwa hivi sasa baada ya Serikali kusambaza mifugo nchi nzima hivyo umuhimu wa maafisa mifugo ni mkubwa sana kwa Mkoa wa Lindi hasa katika Jimbo la Liwale ambako hakuna miundombinu ye yote iliyoandalisha kupokea mifugo. Kwani sasa nyama zinazwa bila kupima ubora wa nyama na hakuna sehemu maalum kwa ajili ya mnada wa ng'ombe hivyo, Wilaya ya Liwale tunahitaji wataalamu wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa wataalamu hao kunakuwepo na ufugaji usiotunza mazingira hivyo kuharibu vyanzo vy ya maji.

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kunijaalia uzima na kuweza kuchangia kwa maandishi. Nawapongeza watendaji wote kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote ambao sikuwataja kwa ajili ya kulinda muda.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wafugaji wetu na Watanzania kwa ujumla. Wizara hii ikiunganishwa na Wizara ya Kilimo zina uwezo wa kuongeza ajira na kuondoa umaskini. Zaidi ya hapo Wizara hii inaweza kuondoa umaskini na utapiamlo kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha hayo inabidi tufanye yafuatayo:-

- i. Kutenga maeneo ya wafugaji bila kuingiliana na wakulima.

- ii. Kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji wetu namna bora na ya kisasa itakayowezesha kuvuna na kupata mapato ya wanyama.
- iii. Wavuvi wetu waelimishwe namna bora ya kisasa zaidi ya kuvua samaki wengi.
- iv. Kuanzisha viwanda vyta kusindika samaki na nyama.
- v. Kujenga machinjio ya nyama kwa kiwango cha kisasa ili nyama zetu ziuzwe mahotelini, migodini na hata kwenye *super market* za ndani na nje.
- vi. Kupunguza mifugo yetu ili tuweze kuitumia na kuwa bora.
- vii. Kufuga kisasa ili kupata mifugo mingi na yenye ubora kuliko ilivyo sasa.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo yangu kwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Nina masikitiko makubwa kwamba huenda kama nchi yetu isingekuwa na maziwa makubwa kuzungukwa na bahari basi tusingekuwa na sekta hii ya uvuvi. Hii ni kwa sababu Wizara haioneshi kujali na kuthamini kusambaza huduma za uanzishaji wa mabwawa ya samaki kwenye maeneo ambayo hayana maziwa na mito mikubwa. Hivyo kutokuwa na tija inayokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Tanga wenye Wilaya nane ni Wilaya nne zilizoko pembezoni mwa Bahari ya Hindi ndio zinazopata samaki, Wilaya hizo ni Mkinga, Tanga, Pangani na sehemu ndogo ya Wilaya ya Muheza. Aidha, Wilaya ya Lushoto, Korogwe, Handeni na Korogwe hazina mito mikubwa wala mabwawa ya kuwezesha wananchi kupata kitoweo cha samaki.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limekuwa likileta madhara makubwa ya kiafya kwa wananchi hasa wa

Lushoto kutokana na upungufu wa madini ya chuma (*iron*) ambayo yanapatikana katika jamii ya samaki. Naomba kuishauri Serikali itujengee mabwawa ya samaki ili iweze kutibu madhara makubwa ya kiafya ya wananchi wa Lushoto.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na afya bora kwa wananchi wetu wa Tanzania na hata kupunguza bajeti ya Wizara ya Afya, Serikali ni lazima ichukue jukumu lake la kujengea uwezo watu wa Lushoto wapate mabwawa lakini pia na nchi nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, mifugo katika nchi yetu imekuwa haina faida zaidi ya kuonekana kama laana. Tunaomba sana mifugo ijengewe malambo, majosho ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo. Katika Jimbo la Mlalo, Kata za Mnazi na Mng'aro zina wafugaji wengi hasa ikizingatiwa zipo jirani na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ambalo ni eneo rafiki kwa ustawishaji wa mifugo. Nitoe rai kwa Serikali kuititia Wizara hii ili kusaidia wananchi wa maeneo haya ili waweze kuboresha mifugo yao. Nashauri pia Serikali iangalie kwa kina sekta ya maziwa hasa eneo la kodi kwa maziwa yanayoingizwa kutoka nje ya nchi. Nawasilisha.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nianze na suala la elimu ya uvuvi. Kwa kuwa wavuvi wadogo hawana uelewa wa nyavu zinazofaa na zisizofaa, ningeshauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa njia mbalimbali kama vile *tv, local radio* pamoja na vipeperushi vya lugha rahisi. Pia kutoa elimu mbalimbali ya madhara ya uvuvi huo, viongozi mbalimbali na vikundi wapewe semina kwenye eneo husika na Serikali iwasaidie wavuvi wadogo wadogo wenye vikundi mitaji yenye mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa ajira, Serikali iajiri Maafisa Mifugo kwenye maeneo mengi kwani upungufu ni mkubwa. Wafanyakazi wa Idara hizo hasa ngazi ya chini wapewe vitendea kazi kama vile pikipiki na kadhalika na madai ya watumishi wa ngazi zote yalipwe kwa wakati,

kupandishwa madaraja kwa wakati kutokana na elimu zao, kusiwe na watumishi wanao kaimu kwa muda mrefu na maafisa samaki waongezwe.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wapewe elimu ya ufugaji bora, kupunguza mifugo, kufuga kisasa, kuchungia eneo moja na kuondoa migogoro ya ardhi. Pia viwanda vyta maziwa (usindikaji) vijengwe kwenye mikoa yenyne mifugo mingi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara jje Mkoani Tabora kutoa elimu kwenye kiwanda cha maziwa ili kiboreshw, ikiwezekana kuingia ubia na wawekezaji, kutafuta masoko ya mafuta ya samli, kutafuta wawekezaji wa viwanda vyta nyama kwenye maeneo ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, pia kukagua machinjio mara kwa mara, usafi, uplimaji mifugo inayoingia machinjioni, Idadi ya ng'ombe wanaotoka safari na kuingia minadani.

Mheshimiwa Spika, madawa ya mifugo yapelekwe kwa wafugaji ili wasisumbuliwe na mawakala, kutengwe maeneo kwa ajili ya malisho, kujengwe mabwawa kwa maeneo yenyne mifugo mingi na ukarabati wa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti ya mifugo ili sekta hii iweze kuwa rafiki na wavuvi, wafugaji ili iweze kuboresha miundombinu. Bajeti ikiongezwa itasaidia ufuatiliaji na kero mbalimbali. Wafanyakazi kazi wapate mafunzo ya kisasa ili waboreshe elimu zao.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Nipende kusema ya kwamba sekta ya uvuvi ni rasilimali ya kujivunia sana hapa nchini kwetu na nchi yetu isingekuwa ya umaskini na kutegemea misaada kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naongea haya kwa uchungu sana jinsi wavuvi wanavyonyanyasika kwenye nchi yao kwa kuchomewa nyavu zao eti hazina ubora wa kuvulia, huu ni

uonevu wa hali ya juu sana, *otherwise* Serikali itoe nyavu mbadala zinazoruhusiwa na Serikali na si kuwakamatia wavuvi na nyavu zao na kusema hazina ubora.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iache kutumia nguvu ya dola (vyombo vy'a dola) kuwanyanya wa wavuvi hasa wa Mkoa wa Mara. Ukatili unaofanywa na vyombo vy'a dola kwa wavuvi si sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ilete nyavu zinazotakiwa kwa wavuvi wa maeneo yote na si kuwanyanya nyavu zao na kuzichoma halafu mnawaacha hewani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo; ukatili wa wanyama kuwekwa chapa kwenye ngozi njia inayotumiwa na Serikali si sahihi kabisa kwani ng'ombe huugua na kupata maumivu makali sana, huu ni ukatili wa hali ya juu. Haki za wanyama ziko wapi? Ubora wa ngozi unapotea, utaiuza wapi ngozi yenye alama kubwa?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itafute njia mbadala badala ya kuwachoma na chuma cha moto ni vema wangewavalisha *ring ambazo* zinakua na alama au wawekwe alama kwenye masikio na si kwa kuwachoma alama kubwa hadi kusababishia maumivu kwa ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, hii tabia ya kutaka kupata leseni ya biashara ya ng'ombe eti lazima ujisajili Bodi ya *TMB* kwa shilingi 102,000 *then* unakata leseni ya *export* shilingi 2,500,000 na kila ukisafirisha mifugo ulipe shilingi 2,500 kila ng'ombe mmoja (*movement permit*) *then* unalipa shilingi 5,000 kila ng'ombe *market fee* bado shilingi 3,000 kila ng'ombe kama kodi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nipende kuishauri Serikali ipunguze kodi kwa wafugaji wa maeneo yote. Nakumbuka mwaka jana baadhi ya maeneo kodi ilipunguzwa/kufutwa isipokuwa kwa mifugo tu. Ifikie mahali tumsaidie huyu mfugaji na siyo kumkandamiza.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe mwongozo nini mfanyabiashara wa ng'ombe anapaswa kuwa navyo ili kukidhi sifa za kusafirisha na kuza ng'ombe ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono hoja ya hotuba ya uvuvi na mifugo.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawapongeza Mheshimiwa Luhaga J. Mpina (Mb) Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu Mheshimiwa Abdallah H. Ulega (Mb) kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itilie mkazo katika sekta ya ufgaji wa nyuki, maana katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 Serikali hajiaonesha mkakati wowote katika kuwasaidia wafugaji wa nyuki nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwasaidie wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam kupata vyombo vyaa uvuvi vya kisasa ili waweze kuvua samaki wengi ambaao watakidhi matumizi ya wananchi na viwanda vyetu maana kuna wakati mwingine katika Soko la Kimataifa lilitopo *Ferry* (Kivukoni) Mkoa wa Dar es Salaam kunakuwa na uhaba mkubwa wa samaki.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali inunue meli kubwa ya uvuvi ambayo itakuwa na uwezo wa kwenda katika maeneo ya maji yenye kina kirefu na kuvua samaki wengi ambaao watatumika na wananchi wa Dar es Salaam pamoja na viwanda vyetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya wananchi waishio Mkoa wa Dar es Salaam hutumia kuku waliofugwa kisasa na hukua kwa wiki tatu hadi nne, pia hutumia na mayai ya kisasa. Kuna sintofahamu inayosemwa na baadhi ya watu kuwa nyama ya kuku hao pamoja na mayai yanayofugwa kisasa yana madhara kwa afya ya binadamu. Naishauri Serikali itoe kauli ili kuondoa sintofahamu ya kuwa kuku wa kisasa na mayai yana madhara kwa mlaji ili mfugaji aweze

kutumia mbinu mbadala, ikibainika kuwa kuku hao na mayai yana madhara kwa afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze ufadhili kwa wanafunzi wanaosomea kozi (fani) za mifugo na uvuvi ili kuweza kupata wataalam wengi ambao watasaidia kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwamilikishe wafugaji ardhi ya kutosha kwa ajili ya malisho na kuweza kuchimba mabwawa kwa ajili ya wanyama (mifugo yao) ili kuondoa migogoro baina ya wafugaji na wakulima ambao inaendelea kuwepo hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pindi mfugaji akilisha mifugo yake katika shamba la mkulima, Serikali isimamie (mfugaji)) aweze kulipa fidia kwa mkulima maana mazao hulimwa kufuata hali ya mvua. Hivyo fidia hiyo ilingane na mazao yaliyoliwa ili mkulima awe na uwezo wa kutumia fidia hiyo kuweza kununua mazao (nafaka) hiyo ili kumsaidia kwa matumizi ya familia yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho namuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri Luhaga J. Mpina (Mb) na Naibu Waziri Abdallah H. Ulega (Mb) ili muweze kuyaende majukumu yenu ya kila siku.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa hii na nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mabadiliko makubwa aliyoyafanya kwenye uongozi wa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari (*MPRU*) kwa kuteua mtendaji mpya na kuvunja bodi ya taasisi. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aharakishe kuunda bodi kwani pesa za maduhuli kwa Halmashauri ya Mafia zimekwama kutolewa kwa sababu *MPRU* haina bodi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni uwekezaji uliofanywa na MPRU kwenye Kisiwa cha Shungimbili na Hoteli ya Thanda. Mwekezaji anatakiwa alipe *service levy* ya 0.3 kwenye Halmashauri ya Mafia lakini wawekezaji hawa wamegoma kulipa ada hii kwa maelezo kuwa wanalipa moja kwa moja kwenye MPRU. Hii ni kinyume na sheria kwani ada hii ni haki ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, vilevile mwekezaji huyu *Thanda Hotel* mwaka jana wakati nachangia nilimuomba Waziri awaaagize wafute jina la *Thanda Island* kwani Kisiwa kile kinaitwa Shungimbili na siyo Kisiwa cha Thanda. Waziri aliahidi kuwa maelekezo yameshatolewa kwa mwekezaji kufuta jina la *Thanda Island* lakini mpaka hivi sasa tovuti rasmi ya hoteli hiyo inasomeka kwa jina hilohilo la *Thanda Island*. Nimuombe Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mipaka ya Hifadhi ya Bahari katika Kisiwa cha Mafia, ,mwaka 1994 wakati Hifadhi ya Bahari inaanza ilianza na vijiji vitatu tu yaani Jibondu, Chule na Juani, hivi sasa hifadhi ipo katika vijiji 13. Cha kushangaza zaidi uongezaji wa vijiji vya hifadhi umefanyaika kinyume na matakwa ya kisheria na wananchi wa vijiji husika hawakushirikishwa na wameingizwa kwenye hifadhi bila ya kupewa fursa ya kuulizwa na wao kutoa ridhaa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni maduhuli yatokanayo na watalii kuingia katika maeneo ya hifadhi. Kanuni ya Hifadhi inayopanga mgao wa asilimia 70 kwa Hifadhi, asilimia 10 Halmashauri na asilimia 20 vijiji husika haipo sawa hasa kwa kuzingatia Halmashauri ya Mafia ina majukumu makubwa katika jamii kama elimu, afya, barabara na maji. Tunaomba Mheshimiwa Waziri abadilishe kanuni na mgao uwe 50/50 baina ya Halmashauri na MPRU.

Mheshimiwa Spika, suala la ubinafsishaji wa Visiwa vya Nyororo na Mbarakuni, namuomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe MPRU inashirikisha Halmashauri kwenye uwekezaji wowote katika Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii muhimu kwa ustawi wa Taifa letu, Wizara ambayo Serikali ikiwekeza kimkakati na kuhakikisha inapeleka fedha za maendeleo kama zinavyopitishwa na Bunge basi Watanzania zaidi ya 10% ambao wamejajiri moja kwa moja kwenye sekta hii wataweza kuinuliwa kuliko hali ilivyo sasa ambapo tumeendelea kushuhudia wafugaji wakihangaika vilevile wavuvi na wafanyabiashara wa samaki na dagaa wamekuwa wakinyanyasika sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM ni kweli haina dhamira ya dhati kwenye maendeleo ya watu bali vitu ambavyo Watanzania chini ya 5% ndiyo wanatumia, mathalani ndege ambazo zimenunuliwa kwa fedha taslimu. Ikumbukwe mwaka 2017/2018 Bunge lilipitisha kiasi cha shilingi bilioni nne kama fedha za maendeleo lakini kwa taarifa za Waziri kwenye kitabu cha hotuba anasema hadi Aprili, 2018 Wizara haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya maendeleo licha ya Wizara kukusanya zaidi ya shilingi bilioni nane kwenye tozo ya chapa za ng'ombe tu.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini tunapoteza muda na fedha za Watanzania walipa kodi maskini kukaa vikao vya bajeti ambavyo hata asilimia moja ya utekelezaji inakosekana? Hii ni aibu kubwa sana kwenye mhimili huu muhimu sana katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naomba kuongelea umuhimu wa kuufungua mnada wa mpakani wa Magena uliopo katika Halmashauri ya Mji wa Tarime. Naomba sasa kuikumbusha kwa mara ya nne Serikali juu ya umuhimu wa kuufungua Mnada wa Magena ambao ulifungwa bila sababu za msingi mwaka 1997 kwa kile kilichodaiwa kuwa ni wizi wa mifugo. Sababu hii ilitolewa tarehe 9/4/2018 wakati Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi akijibu swali langu nilipotaka kujua ni lini Serikali itaufungua mnada wa mpakani wa Magena. Kwa masikitiko Serikali ilirudia majibu ya ukaririsho kuwa mnada ulifungwa mwaka

1997 kwa ajili ya wizi wa mifugo. Ukweli ni kwamba kuna nia ovu na wananchi wa Tarime na nia hiyo imetawaliwa zaidi na utashi wa kisiasa badala ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2011 nimekuwa nikiiomba Serikali kuufungua Mnada wa Magena nikitambua fika mnada ule upo kimkakati na ufunguaji wake ungeweza kutoa fursa nydingi sana kwa wananchi wa Tarime na kupelekea kukua kwa uchumi kwani sekta mbalimbali zingenufaika (*multiplier effect*). Majibu ya Serikali ya tarehe 9/4/2018 yalijaa fedheha kwa wananchi wangu wa Tarime kwani mnada kupelekwa Kirumi bado ng'ombe wanaonunuliwa Kirumi hupitishwa Tarime kwenda Kenya kwenye Mnada wa Maabara na kupelekea upotevu wa fedha za Tanzania kwani wanaopeleka ng'ombe Kenya hufanya manunuzi ya mahitaji huko huko na kutoa fursa za ajira Kenya.

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize zaidi hapa Tarime wanaposema tangu mwaka 1997 hadi 2018 yaani miaka 21 baadae bado wimbo ni sababu ya wizi wa ng'ombe? Serikali inasahau kuwa Tarime bado kuna Mnada wa Mtana na Randa mbona hao ng'ombe hawaabiwi? Serikali inasahau kuwa tuna Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya na kuwa Mnada wa Kirumi kwanza siyo wa mpakani, lakini pia upo Mkoa wa Kipolisi wa Mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii hii haijui kwamba mwaka 2016 baada ya kuuliza swali Bungeni aliye kuwa Waziri wa Kilimo, Uvubi na Mifugo, Mheshimiwa Mwigulu aliweza kufika Tarime na watendaji wa Wizara ambapo tulikaa kikao na Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya pamoja na Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime na maazimio ya kikao ilikuwa ni kuufungua Mnada wa Magena baada ya kujiridhisha na mazingira ya sasa na hivyo kupangwa siku za Mnada wa Kirumi uwe mara mbili kwa wiki na ule wa Magena nao mara mbili kwa wiki ila siku tofauti. Baada ya hapo tuliweza kutembelea eneo la mnada na kujiona miundombinu iliyopo kuwa inakidhi kuanza mnada mara moja. Mheshimiwa Waziri

pamoja na DC Luoga waliongea na wananchi na kuwahakikishia ufunguzi wa mnada huo.

Mheshimiwa Spika, nimeandika haya kuweka kumbukumbu sawa maana nilishtushwa na majibu ya mwaka 2018 wakirejea maamuzi ya mwaka 1997 ilhali kuna maamuzi ya mwaka 2016 yanayosubiri utekelezaji tu. Naomba Serikali ione ni kiasi gani tunapoteza fursa kwa kutoufungua mnada ule kwani Mnada wa Kirumi kamwe hauwezi kuwa mbadala wa Mnada wa Magena badala yake tutaendelea kuifaidisha Kenya.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba ng'ombe zinazotoka Wilaya ya Serengeti haziendi Kirumi zinaenda moja kwa moja Kenya kupitia Tarime. Ng'ombe zinazotoka Rorya kwa asilimia kubwa zinaenda Kenya moja kwa moja kupitia Tarime. Ng'ombe zinazotoka Kirumi zinapita Tarime kwenda Kenya.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali hii ya CCM ifungue mnada huu wa kimkakati wa Magena ili uweze kuwa *stop center* ya minada hiyo mingine na uweze kuliingizia Taifa fedha ambazo sasa zinapotea kwa kupeleka ng'ombe kwenye mnada wa mpakani wa Kenya ilhali Tanzania tuna mnada wa mpakani lakini tumeufunga kwa sababu za kisasia. Tunataka kuona watu wa Kenya wanakuja kufuata mifugo Tanzania na kuweza kuacha fedha za kigeni kwetu na siyo sisi kuapelekea mifugo.

Mheshimiwa Spika, labda Serikali haijui Kenya wanategemea sana ng'ombe (mifugo) wa Tanzania na hivyo huu mnada ukifunguliwa utakuza uchumi wa wananchi wangu wa Tarime, Halmashauri tutapata mapato na Serikali Kuu pia itapata mapato na zaidi kasi ya ukuaji wa Mji wa Tarime itaongezeka na fursa za uwekezaji nazo zitaongezeka na hatimaye maendeleo. Zaidi ule usumbu wanaoupata wafanyabiashara wa Tanzania wakati wanavusha mifugo kwenda Kenya utakuwa umepunguzwa. Naomba Wizara inipe majibu ni lini na kwa uharaka mnada ule utafunguliwa.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na kazi nzuri inayofanyika katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu Ranchi za Taifa. Kumekuwa na malalamiko makubwa ya siku nyingi kuhusu wananchi wanaoishi karibu na Ranchi za Taifa maeneo yaliyogawanya katika *blocks* (vitalu) kukosa malisho. Wananchi wanaoishi Misenyi katika Kata ya Kakunyu, Kijiji cha Bubale na vijiji vingine katika kata hiyo maeneo yao yalitwaliwa, watu wakagawiwa *blocks* na wananchi wazawa/wakazi wakakosa mahali pa kulima na kufugia. Wamesema, wamepiga kelele, wamepaza sauti lakini sauti zao hazisikiki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema wale walioshindwa kuendeleza vitalu walivyopewa watanyang'anya wapewe wawekezaji wengine wenye ng'ombe wengi. Nauliza swali, viyi sasa hawa wananchi wakulima/wafugaji ambao maeneo yao yalitwaliwa na hawana maeneo? Kwa kuwa kwenye vijiji hivi watu wameongezeka (*population*), naomba yatengwe maeneo zaidi na haya yarudishwe kwa wananchi wa kawaida ambao ni wakulima/wafugaji.

Mheshimiwa Spika, pili, hawa wafugaji wadogo wadogo wanahitaji kuendelezwa. Waliambiwa wajunge kwenye vikundi vikundi watapewa maeneo ya kufugia. Napendekeza tusipendelee wawekezaji peke yao, itafutwe namna ya kuwaendeleza wafugaji wadogo wadogo pia kwa kuwapa maeneo ya kufugia, kuwapa elimu juu ya uboreshaji wa malisho na mifugo. Bajeti hii haioneshi ni kwa namna gani inapanga kumuendeleza mfugaji mnyonge.

Mheshimiwa Spika, sababu ya uvuvi uliopitiliza (*over fishing*), samaki wamepungua sana kwenye Ziwa Victoria. Ili kulisipunguzia mzigo Ziwa Victoria, kuongeza samaki na kuwaletea mapato wananchi na hivyo kukuza uchumi ni vizuri wananchi wakaendelea kuhamasishana ili wafuge samaki.

Mkoa wa Kagera watu wengi wameitika/wamehamasika, wamechimba mabwawa na kufuga samaki, tatizo hao samaki hawanenepi hata baada ya miezi nane au kumi bado wanakuwa na uzito mdogo sana. Tatizo ni kuwa wakulima hawajui mbegu bora iko wapi, hakuna Maafisa Ugani wa kuwashauri wafugaji wa samaki na pia chakula sahihi ni shida. Je, ni lini Serikali itatenga pesa za kutosha na kuendeleza ufugaji wa samaki wa mabwawa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya pili katika Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo, hata hivyo idadi hiyo haijaweza kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa kutokana na changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya mifugo. Wafugaji wa Taifa hili wamekuwa wanahangaika sana kwa kukosa malisho na huduma muhimu na hivyo kusababisha migongano ya wafugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Ardhi na Maliasili zinaelekeza Mawaziri watenge maeneo ya mifugo na kuyatangaza kwenye gazeti na kuyalinda. Sasa Serikali ieleteze hapa ni maeneo gani yametengwa kwa ajili ya mifugo na malisho ya mifugo, yako mikoa na wilaya zipi?

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa wanakamatiwa mifugo yao kwenye hifadhi za misitu, inapigwa mnada hata pale Mahakama inapotoa hukumu kwamba irudishwe kwa wenyewe. Waziri wa Mifugo anashughulikiae suala hili ambalo limewafilisi wafugaji wengi na wamebaki maskini?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani kuhakikisha nyakati za mvua vyakula vyataga mifugo

vinaandaliwa na kutunzwa kwa ajili ya matumizi ya nyakati za ukame, Kilenge's Silage na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, kuna mpango gani wa Serikali kutengeneza na kuendesha kampeni za unywaji maziwa mashulenii na katika jamii nzima? Sote tunafahamu umuhimu wa maziwa na kwa ng'ombe tulionao Tanzania inawezekana kabisa kila shule kupata maziwa kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi vya kuchakata mazao ya mifugo vimekufa hali inayopelekeea wafugaji kukosa masoko ya uhakika kwa mifugo yao. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha viwanda vyote vya ngozi, nyama na kadhalika vinafanya kazi? Naomba Waziri aje na majibu ya nini mkakati wa kufufua viwanda hivyo.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mungu kwa kunipa wasaa wa kuchangia kwa maandishi. Pia nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Mpina na Naibu Waziri Mheshimiwa Ulega.

Mheshimiwa Spika, Kibiti tuna ng'ombe wengi sana, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu siku wafanye mazingira ya wafugaji yaye rafiki kwa kuwajengea malambo, majosho, machinjio ya kisasa, vituo vya minada na vituo vya kukusanya maziwa. Kwa kufanya hivyo itatatua mgogoro baina ya wakulima na wafugaji kwani wananchi watafaidi kwa Halmashauri kukusanya ushuru na kuongeza kipato chake cha ndani hivyo kukamilisha miradi yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kibiti ni Jimbo ambalo lipo pembezoni mwa Bahari ya Hindi ambapo kata tano, vitongoji 42, vijiji 17 vipo maeneo ya Delta na hivyo shughuli kubwa ya kujipatia kipato ni shughuli za uvuvi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, uvuvi wa kamba mti, naomba yafuatayo yafanyike; kuongeza muda wa uvuvi (msimu);

kubadilisha muda wa msimu, kwa sisi Wana Kibiti kamba mti wanapatikana kuanzia mwezi wa nane hadi wa 12; kupunguza wingi wa kodi; muda wa kuleta meli isiwe chini ya miaka 10, iwe zaidi ya miaka 20 na kuwasaidia wazawa kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji samaki, naomba Wizara ije na mpango mkakati wa kuanzisha uchimbaji wa mabwawa ya ufugaji wa samaki. Kwa kufanya hivyo, kutaongeza kipato, lishe bora, ajira kwa vijana na mapato ya Halmashauri.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hotuba hii. Pili, nampongeza Waziri pamoja na watendaji wote kwa kuwasilisha hotuba hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia kuhusu wavuvi wadogo. Wavuvi wadogo ni sehemu kubwa ya wananchi wa Tanzania. Kundu hili linahitaji kuangaliwa kwa hisia ya pekee.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwatengenezea mazingira mazuri kwa kuwatafutia zana za kisasa na kuwapatia elimu juu ya uvuvi ili waweze kufanikiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

(i) Uchomaji nyavu haramu; hatupingi *operation* za kuchoma nyavu lakini hoja ni kwa nini wavuvi ndiyo watu wa mwisho kuadhibiwa, nyavu hizi haramu zinaingiaje nchini? Nyavu zinapitaje na kuingia nchini? Endapo Serikali imeweza kudhibiti mahindi kuuzwa nje ya nchi inashindwa nini kudhibiti uingizwaji wa nyavu haramu nchini?

(ii) Kiwanda cha nyavu haramu Arusha, tuliona Waziri alifika katika kiwanda na kubaini utengenezaji wa nyavu hizi

haramu. Je, ni hatua zipi Serikali imechukua dhidi ya kiwanda hicho? Kama wavuvi wakikamatwa na nyavu zinachomwa, je, kiwanda kilichozitengeneza kinachukuliwa hatua gani?

(iii) Migogoro ya wakulima na wafugaji Mkoa wa Morogoro bado ipo. Kwa nini Serikali isitafute suluhisho la kudumu? Kwa nini Ranchi ya Mkata, Kilosa ambayo imegeuka kuwa pori lisigawiwe kwa wakulima na wafugaji ili kukidhi upungufu wa ardhi na malisho kwa wakulima na wafugaji Wilayani Kilosa?

(iv) Usafirishaji wa ng'ombe toka Shinyanga hadi Dar es Salaam wanyama wanakuwa njiani. Kwa nini Serikali isijenge kiwanda cha kisasa au machinjio ya kisasa wanapotokea ng'ombe na nyama ikasafirishwa magari yenye *air conditioner* na ikapelekwa Dar es Salaam badala ya illivo sasa? Kuendelea kusafirisha mifugo siku nyingi njiani ni kuwatesa mifugo na ni kinyume na haki za wanyama. Kama Dodoma kuititia machinjio yake wamesafirisha mbuzi toka Dodoma hadi Dar es Salaam na wamesafirishwa kwa ndege kwenda Uarabuni ndani ya saa 24, kwa nini Shinyanga, Kanda ya Ziwa washindwe kusafirisha nyama badala ya mifugo?

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kuishauri Serikali kuangalia upya juu ya suala zima la upigaji chapa mifugo ambao unaharibu uzuri wa ngozi hivyo ngozi zetu kukosa soko katika soko la dunia.

Pili, napenda kushauri Serikali kujenga majosho ambayo miaka ya 1970 ilijenga majosho hayo na kusaidia wafugaji kuoshea ng'ombe au mifugo kwa kulipia kidogo hivyo kunusuru mifugo yao na magonjwa. Nashauri jambo hili lifanyike ili kusaidia wafugaji.

Tatu, nizungumzie suala zima la usalama wa nyama tunayotumia pamoja na machinjio yetu. Machinjio mengi

nchini ni machafu, miundombinu yake ni mibovu na hatarishi kwa afya ya jamii. Nimetembelea machinjio ya Dodoma ni ya kisasa na safi. Je, kwa nini Serikali isizlagize Halmashauri zote nchini kujenga machinjio ya kisasa?

Nne, uchomaji nyavu za wavuvi si jambo la hekima bali kinachotakiwa ni kuzuia uingizaji au utengenezaji wa nyavu zisizofaa kufika kwa watumiaji.

Tano, *operation* ya uvuvi haramu iwe na weledi na si ya kuonea watu kwani tunajenga uhasama na jamii. Mfano, mwananchi ajue ni kiasi gani cha samaki anaruhusiwa kuwa nacho ili asiweze kushikwa siyo kama ilivyo sasa.

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Aidha, napenda kumpongeza Spika kwa uongozi wake mahiri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania. Bahari ni fursa kubwa kwa waliojaliwa kuwa nayo kama sisi hapa Tanzania. Mwenyezi Mungu katujalia mwambao mkubwa wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, eneo hili kama Serikali ingeweza kulitumia vyema, nchi yetu ingeweza kujiongeza na kutoka katika hatua tulionayo sasa.

Mheshimiwa Spika, bahari ni shamba lilitosheheni mazao mengi, yaani samaki na vitu vingine kama gesi na mafuta. Bahari ni shamba ambalo halihitaji madawa, mbolea na wala halihitaji pembejeo ya aina yoyote. Lipo tayari kwa ajili ya kuvunwa tu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iondokane na usingizi mzito ilionao ili iweze kuitumia rasilimali ya bahari ambayo imesheheni neema kubwa na ya maana kabisa.

Mheshimiwa Spika, nchi zote zenyе bahari kama yetu wananaufaika na neema hii kwa kuweka mikakati madhubuti

ya kutumia teknolojia ya kisasa na vyombo vya uvuvi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu wenye mikakati thabitii ya uvuvi katika bahari kuu wanakuja kuvua katika maeneo yetu na wanatuvulia samaki wetu kwa wingi na kupeleka neema hii katika nchi zao. Siyo vyema kwamba neema ipo kwetu na kuwaachia wengine kuwavua samaki wetu na kuwahamishia kwao na baadae kuwasafirisha kuja nchini kwetu tukawa ni wateja wao kwa rasilimali itokayo ndani ya bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa kwa Serikali kuifanya bahari kuwa ni chanzo kingine cha mapato ya nchi kwa kuwavua samaki waliomo ili wainufaishe nchi kimapato. Sasa Serikali ije na mpango mkakati wa uwekezaji kama unavyofanywa katika sekta nyingine, kwa mfano, sekta ya madini na utalii.

Mheshimiwa Spika, samaki ni chakula maarufu sana duniani kote. Nchi zote zinahitaji samaki. Ni biashara yenye tija na inayoweza kuipeleka mbele nchi yetu kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameongelea mambo mengi kuhusu uvuvi kiujumla wake. Pamoja na mambo hayo, ni imani yetu kwamba Serikali imesikia ushauri huu na sasa Serikali itaichukulia sekta ya uvuvi kuwa ni chanzo kingine cha mapato, pia ni sekta inayotoa ajira nyingi kwa wavuvi, wachuuzi na wananchi wengine. Tuitumie bahari ipasavyo ili ituletee maendeleo. Ahsante.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Spika, kwanza ni masikitiko makubwa sana kuendelea kuona kwa miaka miwili mfululizo sasa pesa za maendeleo katika sekta ya mifugo – Fungu 99 na sekta ya uvuvi – Fungu 64 hazijapelekwa mpaka sasa. Naiomba sana Serikali kama kweli ina nia thabitii ya kuwasaidia wafugaji wetu na wavuvi wa nchi yetu, basi ipeleke pesa za maendeleo kwenye sekta hizi muhimu ili tuweze kuwakomboa Watanzania wenzetu wanaoteseka sana ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Ranchi ya Mkata kwa muda mrefu sana imekuwa kama kichaka cha wahalifu na kushindwa kusaidia wafugaji wetu kufuga, kulima, malisho na kukodishia wafugaji na kusababisha wafugaji wengi wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Kilosa kukosa njia mbadala ya kupata njia bora ya kufuga mifugo yao. Tunaomba Serikali iangalie sana ranchi hii.

Mheshimiwa Spika, bado kuna migogoro mingi ya wakulima na wafugaji kwenye Wilaya ya Kilosa na hii inatokana na ufinyu wa ardhi bora na wingi wa mifugo. Wafugaji wana mifugo mingi sana hata wanakosa maeneo ya malisho na maji ya kutosha (malambo) na kusababisha kuingiliana sana na mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro isiyokwisha ya wafugaji na wakulima. Tunaiomba sana Serikali ipunguze maeneo ya ranchi na maeneo tengefu na kuyagawa kwa wafugaji ili waweze kupata maeneo ya kufugia, malisho, malambo na majosho.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mipaka ya vijiji vya ufugaji na maeneo tengefu na hifadhi. Kuna migogoro mikubwa sana kati ya maeneo (vijiji) vya wafugaji kama Mufilisi na Mkaa Endelevu na vijiji vingine kama Kiduhi na mipaka ya Hifadhi ya Mikumi na vijiji vingine vya wafugaji kama Parakwiyo, Mbande na Twatwatwa viliyopo Wilayani Kilosa na ambavyo vimkuwa na migogoro ya mipaka na hifadhi na baadhi ya vijiji vya wakulima. Tunaomba sana Serikali itupie jicho jambo hili na kumaliza migogoro hii ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilosa ina upungufu mkubwa sana wa majosho, malambo na malisho ya mifugo. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali iweze kuwasaidia wafugaji wetu hao pamoja na madawa ya mifugo yao ambayo mingi inakufa kwa magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiwaomba sana wafugaji wapunguze mifugo yao kwenye Wilaya ya Kilosa lakini hatujawaandalia masoko ya mazao yao ya mifugo. Tunaiomba sana Serikali kujenga viwanda vya mazao ya

mifugo kama viwanda vya kusindika nyama, maziwa na viwanda vya ngozi katika Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Kilosa ili kuweka mazingira wezeshi na rahisi kwa wafugaji wetu kuweza kufuga mifugo michache na yenye tija kwa Taifa letu. Ahsante.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 100 wa hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Kipengele (c) kimeongelea juu ya ukaguzi wa ufanisi wa kazi katika Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (*MPRU*). Mheshimiwa Waziri anaelezea hatua za kuvunja Bodi ya Wadhamini na kumsimamisha kazi Meneja wa Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu kwa vigezo vya matokeo ya ukaguzi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*Performance Audit/CAG*).

Je, imekuwaje Waziri akimbillie kufanya maamuzi kama haya? Mbona Mawaziri wengine katika sekta zao hawakufanya maamuzi haya? *Performance Audit* zimefanyika kwa taasisi mbalimbali za Serikali na malengo yake yalikuwa ni kuboresha. Je, Mheshimiwa Waziri aliwapa nafasi ya kujibu yaliyojitekeza? Ripoti ya *CAG* haioneshi maeneo ya ukaguzi wala vigezo viliviyotumika katika kufanya hiyo *performance audit*. Pia ripoti hiyo haielezi chochote kuhusiana na udhaifu uliotajwa.

Mheshimiwa Spika, katika miaka miwili mfululizo *MPRU* haikutengewa kiasi chochote cha fedha kutoka Serikalini. Iweje Wizara itegemee *MPRU* kufanya utofauti chanya?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 113 na 114 wa kitabu cha hotuba imeonesha utekelezaji wa majukumu ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu chini ya *MPRU*. Hotuba imebainisha utekelezaji wa kazi zake (*MPRU*) pamoja na malengo yake ya kuendeleza mipango kazi yake kwa mwaka 2018/2019; je, ni kwa nini Wizara haikubainisha kushindikana kwa *MPRU* kutekeleza majukumu yake kwa ulinganifu wake na matokeo ya ukaguzi wa *CAG*?

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa MPRU/hukusanya maduhuli ya takribani slingi bilioni moja kwa mwaka na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 mwezi Machi, 2018 yaliiflikia shilingi bilioni 1.1. Je, uamuzi huu wa Mheshimiwa Waziri wa kuvunja bodi na kumwondoa Mkurugenzi kunatuhakikishiaje maboresho ya mapato?

Je, maamuzi yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri ni sehemu ya mapendekezo ya CAG? Kama siyo, yanasaidaje katika utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na maslahi mapana ya Kitengo?

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali katika jitihada zake za kuhakikisha wafugaji na wavuvi wananzaika na kazi zao wanazofanya katika kujitafutia kipato, kudhibiti uvuvi haramu, kuhifadhi mazingira na kudhibiti rasilimali za bahari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iweke mazingira wezeshi kwa wawekezaji katika sekta ya maziwa kwa kuangalia tozo na kodi mbalimbali zilizopo katika sekta hiyo ya maziwa. Serikali iwekeze fedha za kutosha katika uzalishaji wa viumbe kwenye maji ili kuongeza mazao hayo, kuongeza ajira na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, elimu ya ufugaji wa samaki na viumbe wengine waishio kwenye maji ipewe msukumo mkubwa kwa vijana katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nawatakia Mawaziri utekelezaji mwema wa majukumu yao ya kazi. Ahsante sana na naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nzuri zilizochukuliwa katika kutatua changamoto zilizoko katika sekta ya uvuvi na mifugo, kuna changamoto nyingi ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka. Naomba nichangie changamoto chache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi itaendelea iwapo itapata msukumo kwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa kama kuwekeza kwa wataalam ambao wataendana na teknolojia ya uvuvi wa kisasa, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uvuvi na uhifadhi wa samaki, elimu, semina za mara kwa mara kwa wavuvi wadogo wadogo. Viongozi wa Serikali watumie lugha ya kuelimisha wavuvi kuliko kutumia nguvu zaidi, hali wakijua uelewa wa watu uko tofauti. Ndiyo maana Baba wa Taifa alitumia kampeni ya kuelimisha na kuhamasisha watu katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iweke mazingira ya kujenga mabwawa ya kufugia samaki kwa kila Halmashauri ili wananchi waweze kupata lishe na pia kufanya biashara na kuongeza ajira kwa vijana. Kwa kufanya hivyo kunaweza kupunguza malalamiko ya uvuvi. Pia Kanda ya Ziwa itumike kujenga mabwawa ya ufugaji wa samaki kando kando ya Ziwa Victoria, kwa kiwango kikubwa bila kusahau kuwaelimisha wavuvi wadogo wadogo. Uvuvi wa bahari kuu ndiyo mkombozi wa kuingiza fedha za kigeni. Vilevile nguvu iongezwe kupata makampuni makubwa ya kuvua samaki katika bahari ya kina kirefu (*Deep Sea Fishing*).

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo ndiyo tegemeo la wanadamu karibu wote kwa maana ya kwamba kabla ya mtoto kuzaliwa, mama mjamzito hushauriwa kunywa maziwa, mtoto akizaliwa hunywa maziwa, mgonjwa hunywa maziwa, mzee chakula chake ni maziwa na sisi maziwa ndiyo chakula chetu cha kila siku. Serikali iangalie uwezekano wa kuwekeza katika sekta hii, kwa kuwa inawagusa wananchi wengi walio maskini sana, pia uelewa wao ni mdogo ingawa wana mifugo mingi. Ubora wa mifugo na unaifuu wa kodi ambazo ni kikwazo kwa mazao ya mifugo kama nyama, maziwa, ngozi, jibini, mifupa, mbolea na kadhalika. Kupiga chapa ng'ombe kuangaliwe kwa kuweka alama eneo la masikioni kuliko kuweka pajani au tumboni. Hali hiyo huharibu ubora wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Serikali ifanye uwekezaji mkubwa katika sekta ya mifugo na uvuvi ili

kufanya mageuzi na mapinduzi katika sekta hizi bila kusahau sekta ya kilimo pia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri. Changamoto zinazozungumzwa na Wabunge mkizifanya kazi zikaungana na yale mazuri mnayofanya, hakika tutapiga hatua katika sekta hii kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara izingatie na kusimamia matumizi bora ya ardhi katika kutatua migogoro ya wakulima, wafugaji na wawekezaji kwenye Ranchi za Kitengule, Kikurula na Mwisa. Nashauri yafuatayo yafanyike:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ikae na wawekezaji wa Kitengule na *Kikurula Ranch* akiwemo *Super Doll* na kuhakikisha mpango kazi wa matumizi ya ranchi yanaheshimiwa. Maelfu ya hekta zimetolewa Kitengule ila matumizi bora ya ardhi (ranchi) hayazingatiwi.

Mheshimiwa Spika, *interest* yangu Mbunge na Wana Karagwe ni kuona wawekezaji kwenye Ranchi za Kitengule na Kikurula wanasaidia kutengeneza ajira kupitia matumizi bora ya ardhi (uwekezaji), wanachangia kipato cha Taifa (kodi na *CSR*) kwa kata zinazozunguka ranchi.

Mheshimiwa Spika, vikundi 25 vya Karagwe vya *SACCOS* za wafugaji, naomba sana vipate vitalu Mwisa II kuondoa migogoro ya ardhi kati yao na wakulima na wawekezaji niliowataja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufugaji cha Kikurula kimesahaulika, naomba Serikali ikisaidie ili kipate kipaumbele kwenye bajeti ya maendeleo na kiwe *center of excellency* kwa Kanda ya Ziwa. Ahsante sana.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, katika Soko la Samaki la Kimataifa la Dar es Salaam zaidi ya asilimia 75 ya samaki wanaouzwa pale ni samaki kutoka nje ya nchi. Jambo hili ni baya na linahitaji kuangaliwa upya ili tuweze kuwalinda wavuvi wa ndani. Kibaya zaidi wamiliki wa viwanda vyta samaki ndio waagizaji wakubwa wa samaki kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ukamataji nyavu za kienyeji maarufu kama makokoro linawaonea wavuvi wa samaki wadogo yaani dagaa kwa kuwa dagaa hawawezi kuvuliwa na nyavu nyingine tofauti na nyavu za macho madogo. Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia wavuvi wa dagaa nyavu maalum za kuvulia dagaa, maana bei yake ni kubwa na wavuvi wetu hawawezi kumudu.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu uchapaji chapa wa ng'ombe. Uchapaji chapa ng'ombe unaharibu ngozi ya ng'ombe, hivyo itasababisha hasara ya ngozi ya ng'ombe. Naishauri Serikali waweke nembo kwenye masikio ya ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, uchomaji nyavu moto unasababisha hasara kubwa kwa wavuvi. Naishauri Serikali badala ya kuchoma nyavu hizo, zingepelekwa *VETA* kwa ajili ya kuunganisha ili wapate nyavu inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kamata kamata ya watu wanaoshikwa na samaki. Hii kamata kamata ya wanawake wanaokuwa na samaki hata wachache siyo haki. Naiomba Serikali waache kuwanyanyasa wanawake hao na badala yake waone ni namna gani watawadhibiti wavuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, pia bado kuna tatizo kubwa la mifugo kuzunguka zunguka mijini. Naiomba Serikali iondoe mifugo mijini na iwatafutie wafugaji maeneo ya vijijini ambako kuna nyasi za kutosha. Pia naomba Serikali itoe elimu

kwa wafugaji, wafuge kwa kutumia utaratibu wa *zero grazing*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu bajeti ya maendeleo. Inasikitisha kuona kwamba pamoja na Wizara kutengewa bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 lakini kwa bahati mbaya fedha hiyo haikwenda kwa ajili ya maendeleo. Naiomba Serikali ihakikishe inafuatilia fedha yote tunayoidhinisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mada iliyopo hewani. Naomba kuchangia namna wavuvi wanavyotozwa na kudhalilishwa na Wizara ya Uvuvi nchini.

Kwanza kuchomwa kwa nyavu zao. Kumekuwa na utaratibu mbaya sana wanaofanyiwa wavuvi wetu, wanaokamatwa na nyavu za aina fulani kwa kuchomewa moto, dau lake ni moto na kila kitu moto. Hivi kweli ni haki wananchi kufanyiwa hayo katika nchi yao? Kwani hapa Tanzania hakuna Mahakama?

Mheshimiwa Spika, lingine ni leseni ya wavuvi. Kumekuwa na manyanyaso makubwa hapa kwamba ni watu wa aina ipi katika chombo cha uvuvi wanaopaswa kuwa na leseni. Ni chombo, nahodha, mabaharia au vipi? Matatizo haya huletwa hasa na JWTZ na kusababisha madhara makubwa, vipigo na mara nyingine JWTZ huwanyang'anya wavuvi samaki wao baharani eti kwa kuwa hawana leseni ilivyo sahihi. Wakati mwingine wavuvi kutoka Zanzibar hulazimishwa kukata leseni ya kutoka Zanzibar na wakifika Bara haitakiwi wakati mwingine. Usahihi ni upi?

Mheshimiwa Spika, katika mitungi ya gesi hapa napo pana matatizo. Kwa kipindi kirefu wavuvi wamekuwa wakinyang'anya mitungi yao. Kimsingi hakuna sababu.

Wao wamenunua mitungi kwa ajili ya kuvulia na leo wananyang'anywa. Kama wametenda kosa, sheria ichukue nafasi yake, siyo kuwaonea.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mifugo, hivi ni kweli vifaranga vile vilivyotiwa moto ilikuwa ni sahihi? Naomba Mheshimiwa Waziri atapokuja kutoa maelezo, anipatie majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utekelezaji mzuri wa llani. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya wananchi wa Jimbo la Bagamoyo ni wakulima na wanaendesha maisha yao kwa kutegemea kilimo. Shida kubwa wanayopata wakulima wa Bagamoyo ni wafugaji wavamizi. Wafugaji wavamizi wamevamia karibu katika Kata zote za Jimbo la Bagamoyo, wanachunga ng'ombe mpaka katika mashamba ya wakulima bila kujali. Vyombo vyta ulinzi na usalama Wilayani vimeshindwa kudhibiti uvamizi huo na wananchi wanapata shida sana.

Naiomba Serikali yangu tukufu iweke utaratibu wa kudhibiti wafugaji wavamizi. Naishauri Serikali iwaboreshee miundombinu ya ufugaji wafugaji hao katika maeneo wanakotoka.

Mheshimiwa Spika, ufugaji samaki ni eneo ambalo lina uwezo wa kuboresha lishe na ajira kwa Watanzania. Namuomba Mheshimiwa Waziri aweke mkazo na bajeti kubwa ya kutoa elimu ya kufuga samaki nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea unyanyasaji unaofanywa na Wizara hii katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ziwa Rukwa yapo maeneo ya hifadhi ambayo hayajawekewa alama ya mipaka au maboya. Hivyo, wavuvi wanapoingia katika hifadhi hizo ndani ya maji bila kujua, hupigwa sana na kunyang'anywa vifaa na zana za uvuvi. Hivyo Serikali iweke alama katika Ziwa Rukwa ndani ya maji kuonesha mipaka ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali iwe na mpango mzuri wa kuzalisha vifaranga vyatamaki kuwagawia wananchi waweze kufuga katika mabwawa.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka nifafanuliwe katika hoja hizi. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutarudi saa 10.00 jioni hii, tuwahi ili ratiba zetu ziende vizuri saa 12.00 jioni tumalize. Serikali mnayo saa moja, halafu tutakuwa na yale mambo ya mafungu kwa saa moja.

Sasa ile saa moja mtagawana wenyewe kuona namna gani Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri mwenyewe mkaona mnafanyaaje. *Otherwise* kwa Waheshimiwa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Rweikiza, Katibu wenu anasema palepale saa 9.00 alasiri kikao. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, basi nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(Saa 7.09 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2018/2018 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Tuendelee wenzetu watatukuta tukiendelea, mabadiliko ya muda kuanza saa 10.00 jioni yana athari zake na pia ni mwezi wa mfungo huu lakini watatukuta. Ila sijajua upande wa Serikali mmegawanaje ile saa moja.

Waziri wa Katiba na Sheria hatazungumza?

WAZIRI FULANI: Hapa hakutumia kipaza sauti)

SPIKA: Kwa dakika tano? Sawa ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kabudi, karibu, dakika tano.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nami nianze kwanza kwa kuwapongeza sana Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa kuelewa kwamba sekta ya mifugo na uvuvi zinagusa sana mambo ya sheria. Katika utekelezaji wa sheria, tufahamu kwamba sheria inaweza kuwa nzuri lakini utekelezaji wake ukawa na kasoro hapa na pale. Kasoro zinazojitokeza katika utekelezaji wa sheria zisitufanye tuone kwamba ile sheria haifai kabisa.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa na wewe unafahamu kabisa kwa sababu unatoka kwenye eneo hilo ni kuweka uwiano kati ya uhifadhi na matumizi ya rasilimali ili wananchi wetu waweze kuneemeka. Kwa hiyo, pamoja na mambo yote tunayoyazungumza, napenda Waheshimiwa Wabunge tuzingatie kabisa kwamba sheria hizi zote zimetungwa kwa nia njema ili kwa upande mmoja tuhifadhi wanyamapori, misitu na samaki kwa faida yetu sisi na vizazi

vijavyo. Hata hivyo, najua kwamba katika utekelezaji kumekuwa na matatizo ya hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kueleza jambo fupi tu kuhusu baadhi ya mifugo iliyokamatwa na kutaifishwa katika mbuga zetu za hifadhi. Nalisema hilo kwa sababu linaangukia pia katika Ofisi ya Mashtaka na chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, nipende kueleza Bunge lako kuwa baada ya kupata malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi kupitia kwa Waziri wa Mifugo, jana Mkurugenzi wa Mashtaka amepitia mashtaka mbalimbali ambayo yamefikishwa mbele yake ili kuona ni yapi anaweza kuyachukulia hatua. Kwa kupitia mamlaka yake aliyonayo kwa sheria na katiba, ameamua kuachia ng'ombe 553 za wafugaji katika eneo la Swagaswaga ambao baadaye wataelezwa utaratibu. Kwa hiyo, Mkurugenzi wa Mashtaka ameamua kwamba katika kesi hizo nne katika eneo la Swagaswaga ambalo linahusu ng'ombe 553 hatakata rufaa na amri imetolewa ng'ombe hao waachiwe kuanzia leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zipo jumla ya kesi tano zina rufaa katika Mahakama ya Rufaa ambapo Mkurugenzi wa Mashtaka amekata rufaa kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu. Kesi hizi kwa sababu ziko Mahakamani tunaomba ziendelee lakini ambacho tutajitahidi kuiomba Mahakama ziharakishwe kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, pia ziko kesi nyingine ambazo wenyewe wafugaji wamekata rufaa. Tungewaomba wafugaji wenyewe waliokaza rufaa katika kesi hizo ni vyema wakashauriwa kufuta rufaa zao ili pia kuharakishwa kuachiwa kwa mifugo yao, kwa sababu kama kesi ziko kwenye Mahakama ya Rufaa zitaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kuna jumla ya kesi 23 kati ya 27 ambapo watuhumiwa walilipa faini bila kupelekwa Mahakamani na wakarejeshewa mifugo yao. Pamoja na

kulipa faini ambayo ni kati ya shilingi 10,000 na shilingi 300,000 lakini bado kuna malalamiko kuwa wamelipishwa faini kubwa kinyume cha sheria. Tungependa wale wote ambao wana malalamiko ya kweli wayawasilishe ili pia yaweze kufanyiwa kazi ili pale panapolazimika haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, la jumla na mengine tutayazungumzia siku ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka baada ya kuwa ametengeneza maelekezo mahsus i kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka kwa ajili ya kesi zinazohusu wanyamapori na kuzinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa anajipanga kutengeneza mwongozo mwingine kwa ajili ya Maafisa wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili ziweze kuweka utaratibu wa kushughulikia kesi zinazohusu mifugo, uvuvi na atashirikiana na Mahakama ili kuona jinsi gani kesi zinazohusu mifugo zitaendeshwa mapema.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili tutaleta Muswada wa kuanzisha Mahakama Zinazotembea (*Mobile Court*). Ni imani yetu kwamba Mahakama hizo zikiundwa kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika *operation* hizi zitakapofanywa basi hiyo mahakama inayotembea itakuwa hapo ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi, umetupatia habari muhimu sana na nzuri sana na kama ulivyosema kuanzia Jumatatu tutakuwa na Maliasili na Utalii itakuwa vizuri tena jambo hili likasisitizwa kwa sababu kwa kweli wafugaji wamepata taabu sana na wameendelea kupata taabu sana. Yapo mambo mengi yasiyokuwa ya kiutu katika upande huo.

Mimi kama mfugaji mmojawapo na nimezaliwa katika watu hao yaani nashindwa kupata picha mtu ng'ombe wake 100 wamekamatwa halafu wanauzwa wote

ye ye akishuhudia yaani hakuna *massacre* kama hiyo kwa upande wa hifadhi za wanyamapori. Kwa hiyo, utatusaidia tena Jumanne ukirudia ujumbe huu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 15 tafadhali, karibu sana Mheshimiwa Ulega. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo leo nikiwa na afya njema. Nianze mchango wangu kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Napenda kutumia nafasi hii kumuahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitafanya kazi yangu kwa uadilifu na uaminifu mkubwa sana ili kuhakikisha kwamba Tanzania sekta hizi za mifugo na uvuvi zinachangia kikamilifu katika kuinua pato la mfugaji na mvuvi na kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kipato cha katii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda nichukue fursa hii nimshukuru tena Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wao mahiri na makini kabisa ambao unaipeleka nchi yetu katika uelekeo wake ule ule wa amani, utulivu na maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisera kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru sana wewe mwenyewe, Naibu Spika, Wenyevitit wote wa Bunge, Wabunge wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao kwa ujumla wanaonipa katika utendaji wangu wa kazi za ndani na nje ya Bunge letu tukufu. Nawaahidi ushirikiano na nasema ahsanteni sana kwa ushirikiano mnaonipa kila mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia vilevile nichukue fursa hii niwashukuru watendaji wetu katika Wizara, Katibu Mkuu Dkt. Mary Mashingo anayeshughulika na mifugo, vilevile Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba anayeshughulika na uvuvi na Wakuu wa Idara zote na taasisi zote zilizoko katika wizara yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu katika Jimbo la Mkuranga na nataka niwahakikishie kwamba mimi kijana wao niko makini na timamu kabisa kuendelea kutumikia kazi hii ya Ubunge wa Jimbo la Mkuranga bila ya kuchoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naomba uniruhusu pia nimshukuru mke wangu na familia yangu kwa namna ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano wa hali na mali wakati wote wa kutumikia kazi hizi za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba sasa uniruhusu niweze kujibu hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia mjadala wa bajeti yetu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, sisi katika Wizara tumeyachukua mawazo, maoni na maelekezo yao mbalimbali waliyotupatia. Nataka niwahakikishie kwamba vitu vyote hivi walivyotushauri tutavifanyia kazi ili kuweza kupata uendelevu wa sekta zetu hizi za mifugo na uvuvi kwa manufaa mapana sana ya nchi yetu ya Tanzania. Mimi nitazungumza kwa uchache lakini baadae Mheshimiwa Waziri wangu atakuja kueleza kwa

upana zaidi ili kuweza kujibu hoja zote bila mashaka yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni namna ambavyo sisi kama Serikali tulivyojipanga kuhusiana na sekta hii inayochipukia ya ufugaji wa samaki. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge sisi tunaelewa namna ambavyo Wabunge wengi wamekuwa wakivutiwa na suala hili la ufugaji wa samaki kwa maana ya *aquaculture*. Mpango mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba Watanzania walio wengi wanaingia katika ufugaji wa samaki kwa sababu ufugaji wa samaki umekuwa ni wenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, namna gani Wizara tumejjipanga? Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sheria na kanuni zetu wakati fulani unaweza ukaziona kwamba, mathalani samaki ambao wanafugwa katika mabwawa yetu hawaruhusiwi kuchakatwa na hata kuuzwa nje. Hivi ni vitu ambavyo vimesababisha wakati mwagine sekta zetu zisisonge mbele kwa sababu zinakuwa si sekta shindani, watu hawavutiki kwenda kuwekeza pesa zao katika *aquaculture*.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie baada ya mazungumzo ya muda mrefu chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Waziri Luhaga Joelson Mpina, tumekubaliana kufanya mapinduzi katika eneo hili la *aquaculture*. Moja, hatuoni sababu ya kwa nini samaki wanaozalishwa katika mabwawa yetu wasiuzwe kibiashara. Kwa hiyo, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili tunakwenda kulifanya marekebisho. Tuchakate samaki wetu wanaotoka katika mabwawa (*ponds*) lakini turuhusu pia vilevile hata wauzwe ili tuweze kuvutia uwekezaji zaidi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi tumeona juu ya kodi na tozo mbalimbali ambazo zinafanya sekta hii isiweze kuvutia hasa katika eneo la uingizaji wa vifaa mbalimbali. Tumekuwa tukiendelea na mashauriano na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunaamini kwamba

watalifanya *consideration* ambayo itakwenda kuwasaidia Watanzania wavutike katika kuwekeza kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumejiwekeza zaidi katika kwenda kuviimarisha vituo vyetu, tunavyo vituo nchi nzima vinavyofanya kazi hii ya *aquaculture*. Vituo vyote hivi tumejielekeza katika kwenda kuviimarisha ili kuzalisha vifaranga vyta kutosha, tuvigawe kwa wananchi lakini vilevile kuhakikisha tunapata chakula bora kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Maana tatizo kubwa lilitopo katika eneo hili ni upatikanaji wa chakula kizuri na upatikanaji wa vifaranga. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba vyote hivi tunaenda kuvitatua.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni eneo la nyavu, je, hizi nyavu mbona zimekuwa na mjadala mkubwa sana, ni nini tatizo? Pia vilevile imezungumzwa ya kwamba sisi tumetoa *monopoly* ya kiwanda kimoja tu katika nchi ambacho ndiyo kinaingiza nyavu kwa wavuvi, lakini Waheshimiwa Wabunge wakafika hatua ya kusema tumezuia uingizaji wa nyavu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako tukufu hili, Wizara yetu haijazuia hata kidogo uingizaji wa nyavu nchini isipokuwa lazima tukubaliane kazi tulioifanya ya kuondoa zile nyavu ambazo zinasemwa na sheria kwamba ni nyavu haramu ni kubwa mno. Ukitazama anayeathirika ni yule mvuvi wa chini kule, tulipokwenda kuzichoma na kuziteketeza kwa mujibu wa sheria, waathirika wakubwa ni wale wavuvi wetu wa kule chini. Mara zote Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiuliza kwa nini Serikali inajielekeza zaidi kwenda kushughulika na wavuvi wale wa kule chini hawashughuliki na wazalishaji na wasambazaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maoni hayo ya Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana sisi hatukukubali kwanza moja kwa moja kufungua mipaka yetu kuziingiza nyavu zile. Tulisema ni lazima turatibu zoezi hili ili tusiende

kurudia makosa yale yale kila siku ya kwenda kumchomea mvuvi wetu, mvuvi mnyonge kwa sababu sisi tunaamini sekta hii ya mifugo na uvuvi haiwezi kuwepo bila ya kuwepo kwa hawa wavuvi wetu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishieni baada ya kukubaliana na kufanya tathmini hii tutakuwa tuko tayari hata kufungua.

Mheshimiwa Spika, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba nyavu hizi nyingi zinazalishwa katika nchi jirani mojawapo ambayo haina hata ziwa lenyewe. Sisi hapa hiki kiwanda kinachosemwa cha hapo Arusha tumekipa kweli leseni baada ya kutuomba. Mimi mwenyewe kama Naibu Waziri nimekipitia kiwanda hiki, kina marobota ya nyavu za kuvulia dagaa mengi sana hayana mnunuzi. Tumelewa *concern* ya Wabunge ya kwamba inawezekana wale mabwana nyavu zao hazina ubora. Tumekubaliana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara wanaohusika na masuala ya ubora tuweze kwenda kuhakikisha kwamba nyavu zile zinakwenda kuzalishwa zenye ubora zaidi.

Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtuamini ya kwamba jambo hili tunalizingatia ili kusudi sekta yetu ya uvuvi na wavuvi wetu wasiweze kuweza kwenda kuharibikiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna *contradictions* za sheria ambazo zimejadiliwa hapa na baadhi ya wavuvi wenzangu kwamba sasa inakuwaje juu ya hizi nyavu za dagaa lakini wakati huo huo zinakwenda na zinakamatwa tena. Unafahamu wavuvi nao vilevile ni binadamu na ni wajanja, kule Kanda ya Ziwa kuna uvuvi maarufu unaitwa gizagiza. Zilezile nyavu za dagaa kwa mujibu wa sheria na utaratibu wetu zile huenda kuvua kwa kutumia karabai, lakini watu wamezigeuza, hawatumii tena karabai wamefungia zile karabai zao, usiku wanakwenda kuvua bila ya zile karabai. Wanapokwenda kuvua bila ya zile karabai ndiyo wanaita gizagiza.

Sasa wakati ule wanapokuwa hawatumii karabai wanampata sangara mchanga, wanapata sato na mazao mengine ya uvuvi, ukitumia karabai haupati matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda, naomba niende katika upigaji chapa. Waheshimiwa Wabunge wengi sana wameeleza juu ya upigaji chapa na tena babu yangu Mzee Ndassa pale ameenda na kuniambia mimi kwamba tena wewe Ulega mwenyewe hata hii shughuli ya ufugaji hujawahi kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge mawazo na ushauri wenu wote mlioutoa katika kulinda sekta ya ngozi kwenye eneo hili la upigaji chapa tumeyachukua na sasa timu yetu inafanya tathmini. Kwa sababu hili eneo ni endelevu kwa maana ya kwamba upigaji chapa si kitu cha kusema kwamba kinaisha leo au kesho, ni kitu ambacho kipo kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kile ambacho ninyi mmekiomba ni kuhakikisha kwamba tunaboresha, tumeyachukua yale mawazo kwamba tusichome tena ng'ombe badala yake tuwavalishe hereni ama tutafute mbinu nyingine zozote ambazo zitakwenda kuifanya ngozi yetu na mifugo yetu iendelee kuwa na thamani. Mimi nataka niwahakikishieni kwamba jambo mlilotushauri ni jema na tumelichukua na tunakwenda kuifanya kazi mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa pia vilevile hoja na jirani yangu Mheshimiwa Dau iliyohusu *MPRU* kwa maana ya hifadhi ya bahari. Nataka nimhakikishie kwamba kama nilivyokuwa nikijibu kila mara kwamba hifadhi ya bahari ipo kwa mujibu wa sheria lakini yeye *concern* yake ni juu ya mapato na amezungumzia kwamba kwa nini tusichukue *MPRU* kwa maana ya Hifadhi wachukue asilimia 50 na Halmashauri wachukue asilimia 50. Kwa sasa hivi asilimia 30 zinakwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa maana ya 10 zinakwenda katika Halmashauri yenye na 20 inakwenda katika vijiji ambavyo vimezungukwa na ile hifadhi ya bahari. Ushauri wake wote aliotupatia wa kwamba tunataka twende katika usawa tunauchukua. Haya ni mambo ambayo tuna uwezo wa kuyazungumza, tukakaa kwa pamoja, tukashauriana na kuona ni namna gani bora zaidi ya kuweza kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumzia ufugaji wa kuku kwamba Wizara yetu inao mradi mkubwa sana wa kuhamasisha ufugaji wa kuku. Kwa hivi sasa tumeshazifikia halmashauri 20 katika nchi nzima. Tunagawa bure kabisa mbegu ambazo ni za Kitanzania zenye kuhimili matatizo na ugonjwa kama vile ugonjwa wa mdondo na mengineo.

Kwa kusema ukweli tutahakikisha kwamba tunafikia Halmasharuri zote nchini. Mradi huu umefadhliliwa na wenzetu wa Bill & Melinda Gates ambapo tunahakikisha mpaka kufika mwaka 2019, Halmashauri zetu nyangi ziwe zimepata mradi huu wa ufugaji wa kuku. Nia na madhumuni yetu ni kuhakikisha tunainua kipato cha wafugaji wetu lakini pia tuwe na uhakika wa chakula vilevile.

Mheshimiwa Spika, yapo magonjwa ya mifugo vilevile yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Nataka niwahakikishie kwamba sisi katika Wizara tumeweka mkakati madhubuti kabisa wa kupambana na magonjwa ya mifugo. Tumeweka magonjwa ya kipaumbele, yapo magonjwa kama kumi ambayo tumeona kwamba haya tuyafanye kuwa magonjwa ya kipaumbele katika ng'ombe kwa mfano ugonjwa wa kuangusha mimba na magonjwa ya miguu na midomo na katika kuku magonjwa kama vile ya mdondo, yote tumeyapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi maabara yetu ya pale *Temeke Veterinary* tuna chanjo takribani nne. Tunaamini kabla ya mwaka huu haujaisha tutakuwa tumeipata chanjo ya ugonjwa unaowasumbua ng'ombe wetu wengi sana, chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu. Mpaka mwisho wa mwaka huu tunahakikisha kwamba tumeipata chanjo ile. Baada ya hapo ni lazima niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba kama tunataka kweli kabisa sekta yetu ya mifugo isonge mbele ni lazima upigaji wa chanjo yaani uchanjaji wa mifugo yetu uwe wa lazima ili kuweza kuifanya sekta hii iweze kukua vizuri na hatimaye tuweze kushindana katika masoko ya kimataifa, tuuze nyama yetu na watu waikubali nyama yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tutakapofika katika hatua za namna hii nanyi muendelee kutuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba tena nichukue fursa hii kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia moa moja kabisa. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge yale yote ambayo leo mmetuambia katika Bunge hili na kututaka tuweze kurekebisha ili hali iweze kuwa nzuri zaidi katika sekta zetu hizi za mifugo na uvuvi, tumeyachukua na tunakwenda kuyafanya kazi. Ninaamini kwamba baada ya muda mfupi mtakuja hapa kutushangilia kwa namna ambavyo tumefanya vyema katika kazi mliyotutuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Tunakushuru sana kwa mawazo uliyoyatoa na Waheshimiwa Wabunge wamekusikia. Sasa nimuite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, unazo dakika 40, karibu sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja za Wabunge zipo nyingi, zipo ambazo nitafanikiwa kuzieleza hapa na zipo nyngine ambazo utaturuhusu tuzilete kwa maandishi ili Wabunge wetu waweze kupata hoja mbalimbali walizozuliza na ziweze kusaidia katika kusukuma hatua hii ya shughuli nzima ya sekta yetu ambayo ni ya mifugo na uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianza moja kwa moja na eneo ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge zaidi ya nane ambao wapo hapa ilikuwa ni eneo la malisho ya mifugo ambalo wameliongea kwa hisia kubwa. Wewe

mwenyewe najua ni mfugaji pia umeliongea kwa hisia kubwa sana. Pia imezungumzwa kuna migogoro mingi ya wakulima na wafugaji ambayo nayo imo mle, kuna migogoro kati ya wakulima na watumiaji wengine wa ardhi, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi pia kuunda Tume ya watalaam ya kufuutilia suala la migogoro hii kati ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kuwa katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta 10,378.53 kwa ajili ya maeneo ya ufugaji kwenye vijiji 13 katika Wilaya za Makete, Kilolo, Tanganyika, Mpanda na Kalambo. Hadi sasa hekta milioni 2.545 katika vijiji 741 zimetengwa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kuangalia hili suala la malisho ya wafugaji imefanya mambo yafuatayo; moja, katika ranchi zote za taifa (ranchi mama) hekta 2,000 zimetengwa kwa ajili ya wafugaji hasa wakati wa ukame na zitasimamiwa na *NARCO* yenyele lakini unapofika muda wa ukame, wafugaji waliopo kwenye maeneo hayo watakuwa wanlishia mifugo yao, haya ni mageuzi makubwa hayakuwepo. Jumla ya hekta 7,000 tayari zimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Pia hata hapo Kongwa tumetenga hizo hizo hekta 2,000 kwa ajili ya wananchi waweze kupata maeneo ya malisho. Kwa hiyo, katika Wilaya mbalimbali hizi za Kongwa, Longido, Siha, Arumeru na Karagwe kote kule tumetenga hekari hizo. Kwa hiyo, *NARCO* pamoja na *TALIRI*/yote tunatoa hekta hizo kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Spika, lingine tuliloamua ni kwamba katika maeneo ya ranchi zetu ambazo kuna watu wamewekeza, wale wawekezaji wote wababaishaji ambao na Waheshimiwa Wabunge mmewazungumza hapa kwa hisia kubwa, tumefanya tathmini wengine hawajawekeza kabisa na wengine hawalipi kodi ya Serikali, wote wale tunawaondoa. Taratibu zimeshakamilika kilichobaki ni kwamba kufikia tarehe 1 Julai, tutakuwa tumeshamaliza kuwaondoa wawekezaji wote wababaishaji na tutabaki na

maeneo yetu ambayo tutaweza pia kuwapa baadhi ya wafugaji kwa ajili ya kulishia mifugo yao kwa utaratibu ambao utakuwa umewekwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukaweka utaratibu mwininge kwamba kutakuwepo na ardhi ambayo haitakodiwa na mwekezaji wa kudumu. Itakuwa *standby* kwa ajili ya *ku-accommodate* kama kunatokea changamoto katika eneo hilo la malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, tukaenda mbali zaidi kwamba wenzetu Wizara ya Maliasili na Utalii walishakuja hapa kutokana na timu hiyo iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo Wabunge wengine wanauliza kwamba matokeo yake yapo wapi, lakini matokeo tayari tulishayaleta Bungeni. Hizi hekta nilizozitaja za watu ambao tunawaondolea ni zaidi ya hekta 65,000. Vilevile Maliasili na Utalii wamekubali kuyaondoa maeneo tengefu ambayo hayana sifa na wanakamilisha tu, wametuambia hapa watakamilisha hivi karibuni ili maeneo hayo yaweze kutolewa kwa wafugaji. Zaidi ya hekta 96,000 nazo zitatolewa ili kwenda kumaliza migogoro ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa ambalo limefanyika hapa leo, nadhani watu wote wamesikia maamuzi ya Serikali dhidi ya malalamiko ya wafugaji ambao mifugo yao ilikuwa imeshikiliwa na hifadhi. Waziri wa Katiba na Sheria hapa ametoa matokeo ambayo ni zaidi ya ng'ombe 500 kesho zitaondoka. Hii inatokana na kikao ambacho nilikutana na wafugaji juzi kabla ya kuwasilisha bajeti yangu hapa. Tukazungumza wakanipa malalamiko yao nikachukua hatua ya kumuomba Waziri Mkuu baadhi ya Wizara tukutane. Tukakutana Wizara yangu, Wizara ya Katiba na Sheria, Mwanasheia Mkuu wa Serikali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani tukazungumza tukakubaliana na hatua zinaendelea kuchukuliwa kwa ajili ya kupunguza haya malalamiko ya wafugaji hasa wanapokuwa wamekamatwa kwa makosa mbalimbali katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo nilichokifanya ilikuwa kuwakumbusha pia wenzangu wa Wizara zingine umuhimu wa kuzingatia sheria unapokuwa umekamata mifugo ili kupunguza malalamiko ya mifugo kukamatwa na kufa na kukosa mahitaji muhimu kama ya maji na malisho. Nikaandika Waraka kwa wenzangu wote na unafanya kazi, naamini kabisa kwamba malalamiko ya namna hiyo sasa yameanza kupungua. Nataka niwahakikishie wafugaji wa nchi hii wapo kwenye mikono salama na tutahakikisha kwamba haki zao zinalindwa kwa nguvu zote ili waweze kuzalisha kwa maslahi ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ilikuwa ni kuitaka Wizara kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwekezaji mkubwa katika viwanda vyta nyama, maziwa na kadhalika. Nataka niwahakikishie kwa muda huu mfupi ambao nilmekuwepo mimi na Naibu wangu kwenye ofisi ile tumefanya mambo makubwa. Tumefanya tathmini ya mikataba yote na mikataba mingi tumevunja ambayo haina tija kwa Taifa na mingine ambayo haijakamilika tupo kwenye hatua za kuikamilisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kiwanda cha Shinyanga kilichukuliwa na kikauzwa kinyemela na hati haikupatikana. Tumesimamia mpaka ile hati imepatikana kwa muda mfupi na sasa Kiwanda cha Shinyanga tathmini imeshakamilika na niwahakikishie kwamba mwezi huu wa sita tunatangaza *tender* ya kumpata mwekezaji mahiri kwa ajili ya kiwanda hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeenda Kiwanda cha Mbeya kiko vizuri kina ranchi safi. Kiwanda hiki na chenyewe tumehakikisha kwamba kinafanyiwa tathmini sasa ili mwezi huu wa sita na chenyewe kitangazwe ili tuweze kupata mwekezaji mahiri. Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza ambacho Wabunge hapa wamekizungumza sana na chenyewe tayari Msajili wa Hazina anaenda kufanya tathmini ya kujuu thamani yake ili na chenyewe tuweze kikitangaza ili tuweze kupata mwekezaji mahiri katika kiwanda hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mnawenza kuona kasi ya Wizara katika kuhakikisha kwamba viwanda vinajengwa Tanzania na vinaimarika kwa ajili ya ku-support hili soko la mifugo kwa sababu mifugo yetu tusipohakikisha viwanda hivi vinaanzishwa basi faida yake itakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, viwanda hivyo vinaanzishwa na kile cha Utigi, lakini tuna kiwanda kingine kinajengwa Longido cha mtu binafsi, tuna kiwanda kingine kinajengwa Chato, Geita cha mtu binafsi. Kwa hiyo, mtaona kwa muda mfupi mageuzi makubwa ya mifugo yanakuja.

Mheshimiwa Spika, mmezunguzia juu ya uwekezaji katika Ranchi za Taifa (*NARCO*) na kuna wachangiaji zaidi ya 12. Kuna migogoro ya mipaka imezungumzwa huko na kuna mikataba imevunjwa ambayo haina. Ni kweli kabisa, mkisoma kwenye ripoti yangu mtaona mikataba ambayo tumeamua kuivunja ambayo halna tija. Moja, ni mkataba wa *TMC*, kiwanda chetu cha nyama hapo ambapo toka tukibinafsische mpaka leo Serikali hajapata gawio, leo miaka kumi. Tumefanya tathmini katika kiwanda hicho, tukaona madhaifu yalipo na tukakuta kwamba miaka kumi hiyo hawajaweza kufanya malipo ya gawio lolote la kwetu.

Kwa hiyo, tunakamilisha hatua na mkataba huo tutauvunja. Tulipotishia tu kuvunja mkataba wakaja kwetu wakituambia kwamba tayari wana karibu shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kutoa gawio. Kwa hiyo, mnawenza kuona mambo ambayo yalikuwa yanafanyika, ni mambo ambayo yalikuwa yanahitaji tathmini nyingi ili uweze kufikia maamuzi. Ndiyo maana mtaona kwenye ripoti hii kuna tathmini na operesheni, mambo hayapo sawa ukiona hali imekaa namna ile.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diodorus Kamala, kaka yangu na kwa kweli nilikuwa mbeba mikoba hata alipokuwa Waziri. Yeye amezungumza suala la mgogoro wa mpaka alionao kati ya wananchi wake na *NARCO*. Mambo ya mipaka ni ngumu sana kiongozi kuyaamulia mezani, inahitaji nipate muda niende huko nikaone huo mgogoro kati ya *NARCO* na wananchi wale ukoje, tutatatua hakuna

ambalo litatushinda kwa sababu sheria ipo na nyaraka zipo, tutazipitia tutaona nani yupo sawa na kuna kasoro wapi. Nilishamuahidi Mheshimiwa Diodorus Kamala kwamba nitakwenda huko kwa ajili ya kushughulikia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la *Operation Nzagamba*. *Operation Nzagamba* imekuja baada ya kuona rasilimali zetu zinotoroshwa. Waheshimiwa Wabunge nataka niwaambie, tupo hapa tumekula kiapo kwa ajili ya Taifa hili na kulinda rasilimali hizi za Taifa. Hakuna mtu ye yote mwenye nia yoyote mbaya na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania hawa wafugaji na wavuvi, mimi kama Waziri mwenye dhamana ya mifugo ningependa wapate mafanikio makubwa sana na lazima wapate mafanikio makubwa. Rasilimali hizi zinaibiwa, kila mtu anabeba anavyoweza. Kwa mwaka mmoja ng'ombe 1,600,000 wamebebwa, kondoo na mbuzi zaidi ya 1,500,000 wametoroshwa kwenda kuuzwa nje ya nchi bila kulipa chocrote. Wanapoenda kuuzwa nje ya nchi sisi hatupati kitu chocrote. Ngozi, nyambi, ajira na mapato ya Serikali yanaenda nje, tutaendeshaje? Yaani tuchunge sisi halafu wafaidike watu wengine? Hatukatai rasilimali zetu kwenda nchi jirani hata kidogo na isichukuliwe kwamba kuna Waziri au mtu ye yote anakataa, tunachokataa ni lazima Taifa hili linufaikie kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, gharama ya mtu akitaka kuuza ng'ombe nje ya nchi analipia shilingi 20,000 kwa mujibu wa sheria kwa ng'ombe mmoja na kwa mbuzi analipia shilingi 5,000. Haiwezekani ng'ombe wetu wakaenda bila kuzilipa hizo tozo na mimi Waziri nipo hapo kwenye Wizara, haiwezekani. Lazima tuweke utaratibu ambao utalifanya Taifa hili linufaikie. Tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni 1.1 kwa mwezi kwa maana ya sekta ya mifugo, leo niwaambieni kutoka shilingi bilioni 1.1 hizi operesheni ambazo mmezihoji tunakusanya shilingi bilioni 3.5 kwa kudhibiti fedha ambazo zinaibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini wamekuja Mawaziri hapa wa Afya mmewapigia makofi kwa sababu wanajenga vituo vya afya lakini si ndiyo hela zenyewe lazima tusimamie vyanzo vyetu ili tuweze kulijenga Taifa letu. Sasa wewe una mifugo, unatangaza una mifugo milioni 30; mbuzi milioni 18 na kondoo milioni 50, uchunge wewe asubuhi mpaka jioni halafu wakanufaike watu wengine hata kodi kidogo usitoze, halafu ukitoza kidogo iwe lawama tena? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakubali yapo mambo ambayo tunaweza kushauriana kwa namna ya kuyaweka yawe vizuri zaidi, lakini nataka niwaambie tunaibiwa mno na ndiyo maana nikawapa na hiyo tathmini ya shilingi bilioni 263 zinotorosha. Mifugo iliyopo kwenye Taifa hili, Wizara ya Mifugo kwa kodi tunayokusanya haiwezi hata kulipa mishahara ya Wizara labda niwaambieni sasa ndiyo muone wingi wa utoshaji ullvyo. Hata Wizara ya Mifugo yenye mapato yanayopatikana hayawezi kulipa mishahara, hatuvezi kukubali ikawa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya *operation* hapa, watu wanaingiza maziwa na nyama ambazo hazijalipiwa. Wazalishaji wa nchi hii wanakula hasara kubwa, wenye viwanda vya nyama na maziwa wanapata hasara. Sisi ndiyo Wabunge na ninyi ndiyo muda wote mmetulalamikia kushindwa kusimamia *unregulated importation*. Sasa unataka Waziri afanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitegemea na naomba mnipe nguvu zaidi ya kuhakikisha kwamba tunazilinda hizi rasilimali. Katika miezi sita nillyokaa kwenye Wizara hii makusanyo ambayo tumekusanya pamoja na kodi mwaka jana mliondoa nyingi sana Waheshimiwa Wabunge katika Wizara hii lakini tumekusanya mpaka sasa hivi tuna shilingi bilioni 37; zaidi ya shilingi bilioni kumi za mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu walisema Wizara hii wanatoza watu kodi kwa ajili ya kubaki na hela, hakuna fedha yoyote inayobaki Wizarani. Fedha hizi zote zipo Hazina na ndizo hizo zinazoenda kwenye miradi yenu ya maji,

zahanati na kila kitu. Mimi Mpina na Wizara yangu tunapata mshahara tu uliowekwa, ndiyo tunachopata lakini hakuna maslahi mengine yoyote yale katika kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Taifa hili ni la kwetu, mmetuapisha kwa katiba na kwa sheria tunazisimamia sheria ili Taifa linufaikie. Mtaona makusanyo haya, tulikuwa tunakusanya kama shilingi bilioni 32 tu Wizara yote yaani sekta yote ya mifugo na uvuvi unayojua. Nawaambieni tupo hapa leo mwaka unaokuja wa fedha katika Wizara hii tutavunja rekodi ya kukusanya karibu shilingi bilioni 100. Yote haya ni ili Watanzania wapate fedha wanufaikie na rasilimali zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wapiga kura wangu wa Kisesa wako hapa wanansikiliza, mimi siyo mnafiki na mpaka naingia kaburini sitakuwa mnafiki. Sekta hili tutaisimamia kwa weledi mkubwa kuhakikisha kwamba Taifa hili linaendelea maana tumechezewa mno. Kama tunachezewa halafu hatujui tunachezewaje tutaingia kwenye mgogoro mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sekta ya uvuvi. Tumefanya maamuzi, Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkituomba muda wote mnataka Shirika la *TAFICO* lifufuliwe, nimefanya maamuzi Shirika la *TAFICO*sasa linafuliwa tarehe 1 Julai na watendaji watakuwa ofisini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mmezungumzia kuhusu ujenzi wa bandari, ujenzi wa bandari tayari na tumeshapata mpaka na mtu wa kufanya huo upembuzi yakinifu. Miezi nane anakamilisha, Tanzania tunaanza kujenga bandari ya uvuvi. Mungu awape nini kama siyo Mawaziri wenye kuthubutu kama mimi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya maamuzi, wafanyabiashara wetu wengi wanalamika juu ya *importation* ya samaki wengi sana. Tuna maziwa haya lakini samaki wanaoingizwa hapa mpaka sato ambao tunaweza

tukazalisha sisi, vibua ambao wako wengi tu, kwenda kuvua katika katika Ziwa Victoria, watu wanaingiza. Kuna watu wangependa sisi hapa tusivue hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hali ya uvuvi haramu ilivyo na nitawapa *documents* ninazo hapa, nataka niwape taarifa. Kuna Wabunge wengine hapa waliongea mpaka wakalia lakini nadhani kama kweli ni wazalendo, hizo taarifa nitakazozitoa hapa zitawaliza machozi kwa ajili ya Taifa lao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaibiwa kila sehemu, kwenye uvuvi hapa nimeendesha hiyo *Operation Sangara* inaitwa *Operation Sangara* 2018. *Operation Sangara* 2018 ninavyoendesha mimi na Wizara yangu, kwanza, utaratibu wa muundo wake, tumeunda *operation* ambayo sio ya wavuvi tu, tulijua hilli na mimi najua *operation* hizi, kila mtu aliyefanya *operation*, Waziri yejote aliyefanya operesheni alipata tatizo katika Bunge hili na nilijua toka mwanzo kwamba haya yatajitokeza. Ndiyo nikasema tunapounda *operation* hii, nikasema Wavuvi, Mazingira, Polisi, Usalama wa Taifa wote wawemo ili tunapokwenda, tunakwenda kama *task force* kwa ajili ya kwenda kung'oa huu mzizi wa uvuvi haramu ulioshamiri ambapo Taifa linakosa mapato yake. Watanzania wanakula vifaranga, hii nchi siyo ya kula vifaranga, yenye maziwa na bahari kubwa. Halafu Watanzania wanakula vifaranga na wanakula samaki wa kutoka nje na wana furaha kubwa kufanya hivyo wakati samaki wao wanavuliwa kwa shuka, wanavuliwa kwa nyavi zisizoruhusiwa. Kwa hiyo, tukawa tunafanya hivyo.

Vilevile kulikuwa na timu ambayo inaratibu zoezi hili ambayo nayo ilishirikisha Wizara hizo ninazosisema. Tulifanya tathmini za mara kwa mara kuangalia hizi *operation* zinavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme na Wabunge wanisaidie. Nimeingia kwenye Kamati yangu, ikanieleza kuhusu uvuvi haramu, wakanipongeza kwa kazi nzuri na wakasema niendelee. Nilipokuja kwenye Bunge lako nililieleza

kwamba kama kuna changamoto yoyote kuhusu uvuvi haramu, naomba basi hiyo *document* mimi niishughulikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wapo Wabunge ambaao walikuja ofisini kwangu na malalamiko ya wananchi wao. Mengine yalikuwa ya kutaka tu Waziri aone huruma dhidi yao na nilifanya hivyo na wako wengi. Mimi niliomba nipewe hizo nyaraka lakini mpaka leo ninavyozungumza hakuna nyaraka hata moja niliyoletewa na Mbunge hata mmoja ambayo Wizara yangu ilishindwa kushughulikia. Ndugu zangu uvuvi haramu unaliangusha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe matokeo, tumefanya *operation* mara tatu, katika *operation* ya awali watuhumiwa walikuwa 1,200, tulipokwenda kipindi cha mpito wakafika 610 na tumekwenda kipindi cha pili wakawa 1,474; kwa hiyo wanaongezeka. Zana haramu, kokoro, tulivoanza zilikuwa 2,661 tulizoziondoa majini, tulipokwenda kipindi cha mpito ikawa 335 na baadae awamu ya pili zikawa 8,007.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyavu haramu awamu ya kwanza ilikuwa 410,213, ya pili 63,757, ya tatu 81,461. Jumla ya nyavu haramu tulizozitoa Ziwa Victoria ni *pieces* 555,431 ukizidisha mara mita 80 unakuta karibia kilometra 40,000. Kilometra 40,000 ni sawa na kwenda Afrika Kusini karibu mara tano, unaenda unarudi, unaenda unarudi, ndiyo nyavu zilizokuwepo Ziwa Victoria.

Sasa kama una nyavu hizo katika ziwa lako, utafanya nini? Nyavu hizi zote tumeziondoa na sasa kama mnnavyoyaona matokeo ni makubwa, samaki wameongezeka katika ziwa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumekamata samaki wakitoroshwa kwenda nje ambaao Taifa lisengenufaika kwa chochote zaidi ya kilo 181,217. Maana yake ni magari 18 ya tani 10 zilikuwa zinatoroshwa tu kwenda Congo, Malawi, Kenya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mabondo ambayo yana thamani kubwa, zaidi ya kilo 5,147. Kuhusu pikipiki zinazokamatwa zikibeba samaki wachanga zaidi ya pikipiki 269 zimekamatwa wakibeba samaki wachanga na kwenda kufanya biashara usiku. Magari zaidi ya 564 yakiwa yamebeba samaki wachanga na wasioruhusiwa kwa mujibu wa sheria yalikamatwa.

Mheshimiwa Spika, sasa Ziwa Victoria kama mlivopata kwenye taarifa katika rasilimali ya tani milioni 2.7 ambazo Taifa hili ndiyo *stock* yetu ya samaki, tani milioni 2.1 zinatoka Ziwa Victoria. Kwa hiyo, *usipo-manage* uvuvi haramu kwenye Ziwa Victoria, maana yake sekta au Taifa haliwezi kunufaika kabisa na uchumi wa nchi yake.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mambo yafuatayo; hii taasisi yetu ya *TAFAWALIKUJA* ofisini na walikuwa na mambo mawili makubwa waliyoyawasilisha. Moja, ilikuwa ni suala la nyavu za kuunganisha, ndilo lililokuwa tatizo lao kubwa. Walipokuja kwangu nikawaambia nitalifanyia kazi na nikawaagiza *TAFIRI* kufanya utafiti huo ili tuweze kuja na majawabu ya nini tufanye katika uvuvi huu wa nyavu za kuunganisha.

Mheshimiwa Spika, lakini hata tulipoenda kwenye kikao chetu cha *Lake Victoria Fisheries Organization*, ndiyo matokeo haya yanatarajiwa yapatikane ili sisi wote kwa pamoja tuweze kuunga lile zoezi la kwamba kama *East Africa* tutaamua kuvua kwa nyavu za aina gani. Kwa sheria zilizopo zinakataza kufanya uvuvi kwa nyavu zilizoungwa, ndiyo sheria zilizopo na sio Mpina.

Mheshimiwa Spika, vilevile wavuvi hao walivyokuja kwangu baada ya kuachana nao na kuwasihii kwamba waache uvuvi haramu, jioni tu wote walikamatwa, sehemu kubwa wanahusika na uvuvi haramu. Mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakipigiiwa simu na wananchi wakiwa kule walikuwa wakiniwasilishia mimi malalamiko. Wanaponiwasilishia malalamiko anaambiwa amekamatwa tu akiwa hana koleo la plastiki, amepigwa

faini shilingi milioni tano. Ukienda kufuatilia, ukweli siyo huo na Mbunge mwenyewe mhusika anathibitisha kweli nilidanganywa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa nataka niweke hivi, cha kwanza lazima mfahamu, kukamatwa tu kwenyewe ni changamoto, ama umeonewa au umekamatwa kwa haki. Kwa hiyo, taarifa zinaweza zikaletwa zikawa sivyo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na huyu Mbunge wa Ukerewe Jimboni kwake, tulikuwa na Waziri Mkuu, tumefanya ziara katika eneo la Ukerewe, mabango yote ya Waziri Mkuu yalionesha wanaomba maji na vitu vingine, lilitoka bango moja tu la kulalamikia kuhusu nyavu. Waziri Mkuu ameweza kufanya ziara kule na mimi akaniita. Hakuna mahali ambapo Wizara ililalamikiwa kwa malalamiko ambayo yanazungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi muda wote niwapo hapa nimekuwa nikiwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba kama kuna tatizo, Mbunge umepewa muda wa kuongea na Mheshimiwa Spika, umepewa dakika 10 zote za kuongea, mpaka unamaliza kuzungumza unasema tu *operation* hii imejaa uonevu mkubwa, watu wetu wameonewa sana, watu wetu wamedhulumiwa sana lakini kwa nini mimi sijawahi kuambiwa ni wapi, licha ya kuliomba Bunge hili mara kwa mara lituambie ni wapi ambapo wananchi wameonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Musoma nimekwenda mara nyingi mimi, amezungumza kaka yangu hapa, Mheshimiwa Mathayo kuhusu yale magari ya wafanyabiashara. Amekaguliwa akakutwa na maboksi matatu ya samaki wasioruhusiwa, unataka watendaji wafanye nini? Una samaki maboksi matatu katika gari lako na wanafanya *sampling*, wakishayapata yale lazima wakukague, wafanye nini sasa, njia mbadala wafanyaje? Unajua kabisa wewe huruhusiwi kununua wala kuuza samaki wasioruhusiwa, alitaka Mheshimiwa Mbunge wafanye nini?

Mheshimiwa Spika, lile gari lingine liliokuwa limekamatwa akanipigia mimi simu, mimi na ye ye tunapigia simu tu. Yakakutwa maboksi 27 ambayo yana samaki wasioruhusiwa. Sasa ukisharuhusu sheria ya namna hiyo huyu mwenye pikipiki asikamatwe hata akiwa na samaki wasioruhusiwa, huyu mtu wa *class* hii asiruhusiwe, mtaisimamiae sheria na hawa watendaji wangu wasasimamiae sheria?

Kwa hiyo, mimi niseme Wizara yangu tuko *committed*, tuko tayari kuchukua maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge, watushauri katika maeneo yote ambayo wao wanaona kwamba hapa kuna kasoro na sisi tunayafanya kazi. Aliwahi kuja Mheshimiwa Ngeleja ofisini kwangu saa tano usiku akakuta Wizara nzima tuko ofisini. Tunakesha kufanya tathmini hizi lakini kwa shabaha moja tu kuhakikisha kwamba rasillimali za Taifa letu tunazikomboa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kwamba hawana nia mbaya na *operation* lakini tunalalamikia kasoro. Sasa mimi kwenye Kamati niliomba kasoro, nikaja hapa Bungeni mwezi Februari nikaomba kasoro na bahati nzuri kuna Wabunge wengine wanasema kabisa tuna ushahidi, huo ushahidi kwa nini hautolewi au kuna tatizo gani? Kwa nini mtu aseme tu nina ushahidi lakini usitolewe? Naweka mezani kwamba sijawahi kuletewa tatizo lolote na Mheshimiwa Mbunge nikashindwa kulitatua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niwaeleze jinsi mambo yanavyokuwa na niwape mfano mmoja wa Kisiwa cha Lubilli, Bukoba ambapo tulikuta wamevuliwa samaki wachanga kilo 65,000, wameanikwa mpaka hakuna hata pa kukanyaga na yule mtu ni Mkongo ambaye ndiyo anavua. Wanakuja Wacongo na Waganda wanalipa fedha hapa, wana-facilitate uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, ukienda Uganda, Mheshimiwa Yoweri Museveni ameamua kupeleka jeshi kabisa ziwani kwa ajili ya kupambana na uvuvi haramu. Sisi tunatumia *multi-*

agency ye ye anatumia jeshi. Uganda sasa hivi wamepiga hatua kubwa sana katika rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kueleza kwamba tuliwapa rekodi ya kupungua kwa samaki kutoka tani 50,000 mpaka tani 25,000/26,000 kwa maana ya karibia nusu ya rasilimali zetu zote zilizoko katika Ziwa Victoria zimepungua.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala ambalo limeletwa hapa la uwekezaji wa viwanda katika Ukanda wa Pwani. Tunaomba tuwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Ukanda wa Pwani mipango tulijonayo sasa uwekezaji utafanyika tu na ndiyo maana nimeamua kwamba *TAFICO* iwepo pale ili sasa iweze ku-coordinate uwekezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge hapa, kaka yangu sana, Mheshimiwa Alhaji Bulembo, amelalamikia juu ya kumualika mwekezaji mmoja kuja hapa Bungeni na akasema kwamba yule mwekezaji ana tuhuma. Ninachowea kukisema huyu mwekezaji kwa sasa hapa kwetu katika sekta ya uvuvi, Mafia ana shamba lake ambalo sasa hivi anavuna kwa mwaka tani 300 hadi 400 na ameajiri Watanzania 1,700. Mimi hapa Mpina kumualika kuja Bungeni kama ana tuhuma haimuondoshi kwenye tuhuma zake na wala Mpina hawezi kuingia kwenye mtego huo ambao unazungumzwa, mtego upi sasa? Mimi nimemualika tu kama mwekezaji aje hapa, kama ana matatizo vyombo vyaya dola si vipo, vitachukua nafasi. Kwa nini nalo hili liletwe liwe kama lawama kwa Waziri kualika mtu kuja hapa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hebu tupendane, tulijenge Taifa letu kikamilifu. Tulishachelewa mno, ni lazima tuungane sasa kulijenga kwa nguvu zote ili tuweze kufikia mahali ambapo kutaleta matumaini makubwa kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza dhidi ya nyavya na amefafanua vizuri kwamba tatizo la nyavya tumefanya hivyo baada ya kufanya *operation*,

umekamata kila mtu ana nyavu haramu, isingeweze kana muda huohuo tena ukasema kwamba unaweza kuruhusu watu kuingiza nyavu. Sheria inamtaka yule anayetaka kuingiza nyavu ahakikishe kwamba anapata kibali kwanza ndio anaagiza nyavu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi katika kipindi hiki tulichokuwa tunafanya tathmini na tumemaliza kufanya tathmini, tumeona, kama ni nyavu tutaruhusu za kutoka nje tunataka turuhusu kiasi gani? Si ndio Bunge hilihili mnalotaka tuvilinde viwanda vya ndani? Tumetathmini tumeona viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha karibia asilimia 50 ya nyavu zinazohitajika lakini tumeona bado hawana uwezo wa kumaliza kabisa *gap*. Kwa hiyo, sasa hivi tutaruhusu kiasi fulani cha nyavu kuingia ili kuweza kuziba *gap* ambalo watu wetu wanalilalamikia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na hoja nyingine mbili ambazo na zenyewe zimekuwa zikijirudia sana na zimezungumzwa katika maeneo mbalimbali. Wizara iwasaidie wavuvi kupata samaki wengi baharini, hilo Waheshimiwa Wabunge tunalfanya vizuri sana na miradi mingi sana tunapata kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wetu.

Sasa hivi *NMB* wamekuja na mpango mzuri sana wa kuwatafuta wavuvi wote na kuwaingiza kwenye usajili na kuwafungulia akaunti ili tuanze kuwafahamu wavuvi wetu wako wapi na wanafanya nini. Hili tumelisimamia vizuri sana pale Wizarani na sasa hivi karibu akaunti 20,000 za wavuvi zimefunguliwa nchini na *NMB* katika maeneo mbalimbali. Tutakwenda kuwafikia wavuvi wote ambao wako takribani 200,000 ili waweze kuingia kwenye mfumo rasmi wa uzalishaji waweze kukopesheka. Kwa sababu watakapokuwa na mikakati hii wavuvi wetu wataweza kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, lakini limezungumzwa sana suala la *BMUs* kwamba zitumike katika kusimamia mambo haya. Katika *operation* inayoendelea, watendaji na viongozi wengi wa *BMUs* tumewakamata kwa uvuvi haramu. Kwa hiyo, lazima utathmini kidogo uone mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kaka yangu, Mheshimiwa Kanyasu, ye ye kila siku akisimama anazungumzia suala la furu, nembe na gogogo; anazungumzia suala la nyavu ambazo ni *double*. Nimesema haya mambo jamani ukizungumzia mifugo na samaki, unazungumza sayansi. Waziri au Naibu Waziri hatuwezi kujifungia tu tukasema leo tunaruhusu *single*, utafiti unakamilika na *TAFI/R*/tumempa fedha alikuwa na upungufu wa shilingi milioni kumi tu kufanya na kuimaliza kazi hiyo ya utafiti. Tutakuja na majibu, Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hata hawa tulio wapa kazi ya utafiti hawajamaliza swali linaulizwa kila siku lile lile. Suala la nembe na gogogo sheria zilizopo zinakataza kuwava wale kwa maana ya nyavu zitakazotumika zitakuwa ni haramu Ziwa Victoria. Tayari tumesha mua-sign *TAFI/R*/kufanya hiyo kazi na fedha tumempa; mambo haya yatakamilika tupeni nafasi tunauwezo wa kuleta mageuzi makubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninajua, kwamba leo makofi yanaweza kuwa machache sana kwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, lakini nitakapokuja mwakani tarehe kama ya leo Bunge lako lote hili watageuka kuwa washangiliaji kutokana na mageuzi ambayo tunaenda kuyafanya. Tumejipanga, hatutashindwa, tupeni imani hiyo ili tuendelee kuwatumikia.

Mheshimiwa Spika, najua ilishagonga ya kwanza, lakini nimalizie tena kwa kuwashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kunipa imani kubwa ya kuisimamami sekta hii, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Baraza zima la Mawaziri. Pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kisera ambao wanaendelea kunivumilia katika hii kazi ngumu ninayoendelea nao ya kuwatumikia Watanzania. (*Makof*)

Mhehimiwa Spika, na mwisho Waheshimiwa Wabunge niwaombe, niliwasikia Waheshimiwa Wabunge wakisema kwamba hii bajeti itakuwa ni bajeti ngumu sana kupidishwa na Bunge hili. Mimi naomba iwe bajeti rahisi sana kupidishwa na Bunge kwa pongezi ya kazi kubwa tulizozifanya

kwa mageuzi kama hayo. Mmeona vitu vilivyokamatwa, hawa watu kama wangekuwa sehemu kubwa yao si waaminifu haya mambo tusingeyafanya. Kukusanya bilioni 7.5 katika muda huu za kuuza samaki wanaotoroshwa na faini ambazo zilizokuwa zikipigwa, shilingi bilioni 7.5 si kazi ndogo, wangekuwa wala rushwa hapa tusingefikia kukusanya hayo makokoro yote 555,000 kama wangekuwa watu si waaminifu tusingefikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ningewaomba kwanza tuwatie moyo Wizara ya Mifugo na Uvvi ambao wanasihamiwa kikamilifu ili waendelee kufanya kazi hiyo nzuri ya kulinda rasilimali na ili waweze kulinda Ziwa Victoria na maeneo mengine na maziwa yote na baharini kote. Tumefanya operesheni kule mmeona fani zaidi shilingi bilioni 20, tumekamata ile meli ipo mahakamani tunarajia tutashinda kesi hiyo, tunataifisha hiyo meli. Watu wamegeuza shamba la bibi hapa, wanavuna wao zaidi ya bilioni mia nne na hamsini, sisi tunakusanya kodi shilingi bilioni 3.2; jamani mmekubali haya yaendelee kutokea?

Mheshimiwa Spika, huko kwenye *operation Mati* nimezungumza suala la yule mwananchi ambaye alikufa. Jambo hili liko kwenye vyombo vya dola kuona mambo yalienda vipi na ndiyo maana Waziri wa Mambo ya Ndani hapa alishatoa majibu ya jambo hilo, linachunguzwa, watendaji hawa wa Serikali wana sheria zinazowaongoza, kama kuna kosa lilitanyika mhusika atachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaomba tena Waheshimiwa Wabunge waunge mkono bajeti hii ili waiwezeshe Serikali kutekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninawaomba tena; mimi Mpina na Wizara yangu ni vibarua tu, tuleteeni mapungufu ya maeneo mbalimba hapa hata leo, hata sasa hivi tutaenda kwenye maeneo hayo, kwenye vijiji hivyo kukutana na wananchi hao ili tuweze kumaliza mzizi wa fitina na kuondoa kasoro hizo ambazo wananchi wametendewa isivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Sware umesismama.

HOJA YA KUUNDA KAMATI TEULE

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa ridhaa yako. Naomba nisimame na Kanuni ya 120 nikikusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule ya Bunge lako ili kwenda kusimamia au kuangalia hill suala la *Operation Sangara* ambayo Wizara ilikuwa imetekeleza.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi humu ndani leo wameliongelea suala hili, hata kwenye *gallery* yako kuna makundi ya vyama vya uvuvi kutoka Ziwa Victoria wameleta barua pamoja na kuleta malalamiko yao/kilio chao Bungeni kuhusu madhara yaliyotokea baada ya kufanywa hii *Operation Sangara*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimechangia mwazoni na wachangiaji wengine waliopita tuliongelea kwamba hatukatai kulinda rasilimali zetu za uvuvi, tunalisimamia vizuri na nikatoa mfano mikakati Serikali ambayo imefanya ya kutengeza hata vikundi vya *BMUs* na hata kusajili hivi vikundi vingine vya uvuvi, ni lazima kutunza rasilimali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni kuwa *operation* hii imeleta madhara gani? *Operation* hii imetekelezwaje? Hiyo ndio hoja ilivoletwa hapa. Sidhani, waliokuja hapa ni wavuvi wadogo na wavuvi wadogo *majority* yao ni wa kipato cha chini. Kwa hiyo, sidhani kama mvuvi huyu amesafiri kutoka Dar es Salaam, mvuvi huyu amesafiri kutoka Ziwa Victoria

mpaka Dodoma kuja kuleta kilio chao na wamekaa hapa karibu wiki wakijaribu ku-move hii *issue*. Mfano tu rahisi na mwepesi *apart from* barua waliyoileta hawa wavuvi nilikutana na Mheshimiwa Waziri husika na nikamwambia akaniambia najua unachotaka kukifanya, nikamwambia ninachotaka kukifanya kiko wazi na ni kwa ajili ya wananchi walitutuma sisi kama Wabunge kuwasimamia. Nikamwambia hakuna siri kwa sababu kila kitu kiko wazi, mikutano tumefanya, majadiliano tumefanya barua yao wameleta na nikamuonesha kundi lenyewe la wavuvi wale pale nenda kaongee nao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba hapa anawasiliana nao. Hata hivyo nilimuomba personally kaongee nao kama unafikiria hiki tunachokifanya si sahihi, lakini Mheshimiwa hakwenda kuongea na wale wavuvi. (*Makof*)

Sasa naona inafaa na itakuwa ni jambo jema kwa sababu sisi hapa ni wawakilishi wa hao wanyonge, hao ndio walitutuma hata tumekuja hapa humu ndani, basi naomba wasikilizwe na Bunge lako tuweze ku-*justify*ni kweli kuna shida na shida ni nini kama Bunge ili tuweze kuishauri na kuisimamia Serikali vile inavyotakiwa. Naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hawa wavuvi wanaosemekana wana matatizo hebu simameni hapo.

(*Hapa wavuvi waliokuwa wamekaa katika Jukwaa ndani ya Bunge walismama*)

SPIKA: Haya, nashukuru. Nimeona hoja imetolewa na imeungwa mkono ila naomba mkae, nimewaona.

Hata hivyo nadhani Kanuni ile ya 120 ukiangalia kanuni ndogo ya (2)(a) utaona Mheshimiwa Sware inasema; baada ya hoja iliyokuja ikijadiliwa kuamuliwa ndipo ultakiwa uteremke sasa na hoja yako. Sasa hapa hatujaamua bado.

Kwa hiyo, inabidi tuendelee na mishughuliko kwanza na wewe uendelee kujipanga vizuri zaidi, una la kusema? Isome tu hiyo hoja vizuri, au isome watusikie wote hiyo 120.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa nafasi. Kanuni hii ya 120 inasema kwamba:-

120.- (1) Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalumu kwa hoja mahususi itakayotolewa kwa na kuafikiwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya fasiri ya (1) ya kanuni hii, baada ya kujadili hoja yoyote Bunge linaweza kuandaa Kamati Teule kwa madhumuni ya kushughulikia jambo lolote lilitokana na hoja hiyo kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa na kuamuliwa Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja hii chini ya kanuni hii anaweza kusimama mahali pake...

SPIKA: Sasa hapo hapo tu, baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa, ndiyo nasema, bado hatujafika mahali pa kuiamua bado ili sasa ikuruhusu uendelee na hayo mengine, lakini tumekusikia.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Maendeleo ya
Mifugo**

Kif. 1001 - *Administration General.....4, 471,936,196/=*

MWENYEKITI: Tunaenda kwa utaratibu ule tuliojiwekea wa maswali ya kisera kwa majina ambayo nimekwishaletewa tayari, tunaanza na Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mimi nilikuwa naomba nipate ufanuzi wa kina na wa kutosha kwenye tasnia nzima hii ya mifugo, pia pamoja na bidhaa zote ambazo zinahusiana na suala hili la mifugo kwa upande tozo, ada, na kodi mbalimbali. Ni changamoto kubwa ya siku zote na tusipopata majibu ya kuridhisha nitaomba pia Wabunge wenzangu tuweze kusaidiana kujenga hoja ya kuishauri Serikali ili tasnia hii iweze kuchangia vizuri sana katika pato la Taifa na kukuza sekta hii yote ya Mifugo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo nyingi sana katika tasnia hii, na haya ambayo mengine mnayasema ambayo ni ya Wizara ni madogo sana, lakini ukienda kwenye Halmashauri kuna tozo huko ya uchinjaji wa nyama, tozo mbalimbali wanatozwa wafugaji, kama wanafuga ng'ombe, wanafuga kuku, wale wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukijumulisha hizi tozo, ada na kodi mbalimba katika tasnia hii, na ukilighanisha na uwekezaji unaofanywa, fedha ambazo zinapelekwa na maendeleo kwenye uvuvi, kwenye mifugo, kwenye sekta nzima ni ndogo mno ukilinganisha na faida tunayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hii faida nyingine inayopatikana kwa watu ni kula nyama kwa wingi kula samaki kwa wingi sana lakini hii ni sekta isiyokuwa rasmi. Ukiangalia uwekezaji huo ni mkubwa na leo kupitia *regulations* (kanuni) mbalimbali kumeibuka mfumo wa kila mmoja, huku tukipitisha bajeti ikiwa ndogo wanaenda kwenye kanuni na kupandisha tozo mbalimbali. Wizara inapandisha tozo na wanaweka kwenye kanuni, kitu ambacho hata leseni au tozo hiyo iliyotozwa Halmashauri hawatambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo sasa suala la rushwa linaanza, kwa sababu leseni ambayo amekata huko mkoani au wilayani mwenye mifugo kupeleka mifugo yake kwenye mnada akikamatwa njiani anasema kama una ile ya Wizara haitambuliki. Sasa mwenye makosa pale ni nani, ni huyu aliyotoa huku chini ambaye ametoa na hiyo mifugaji ililipiwa tozo halali kabisa au ni huyu ambaye amejiamulia tu huku juu bila kutoa elimu kwa watu wa Serikali hao hao? Kwa sababu Serikali ni moja, kutoka ngazi ya taifa kuja huku halmashauri hakuna *coordination*. Viwanda vingi wanalamika, ukiangalia maziwa, wasindikaji mbalimbali, kila mmoja analalamika kutokana na tozo, ada na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itakaa kwa pamoja kuangalia hii tasnia nzima ya mifugo kuanzia kufuga, kuzitunza, kuvua, lakini pia kusindika hadi kuja sokoni na kuangalia kwa nini bidhaa hizi za nje zinanufaika badala ya bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa nchini? Na...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jitu umeshasema sana lakini sasa hebu *narrow-in* unachotaka ufanuzi hasa ni kitu gani?

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo hizi ni lini sasa watacaa pamoja kama Serikali na kuzipunguza au kuziondoa na kutambua kwamba...

MWENYEKITI: Ahsante sana umeelewaka.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

MWENYEKITI: Kwa hiyo issue ni ku-*streamline* tozo mbalimbali kati ya Wizara na kwenye Halmashauri zetu. Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhalii.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Jitu kwa swali lake zuri sana aliloliletu hapa na yeye tumekuwa naye, nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda

na Biashara, tulikuwa tukilalamika wote juu ya tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye maziwa na nyama. Serikali imelishalfanyia kazi jambo hili, Waziri wa Viwanda alilazimika kuunda tume ya wataalam kwa ajili ya kuzipitia tozo zote za taasisi zote na Wizara zote ili kuweza kutafuta namna ambayo inaweza kupunguza malalamiko lakini pia inaweza ikawasaidia wawekezaji wetu wa hapa nchini kuweza kuwekeza, lakini na kuweza kushindana na watu wengine au na nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imefanyika vizuri sana, mapendekezo yameshaletwa na sasahivi mapendekezo tayari yapo Serikali na niseme tu kwa niaba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba leo hii saa mbili usiku, tukitoka hapa kuna Baraza la Mawaziri kwenda kujadili tozo hizo na mimi nimesema hayo kwa sababu najua siyo siri kwa sababu ni jambo ambalo tulishayaliahidi siku nyingi kama Serikali. Kwa hiyo tunaenda kujadili ile taarifa ambayo imeshaletwa na watendaji wetu ili tuone na yote yamo ukiongelea Wizara yangu na Wizara zingine.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Jitu Serikali imeshalichukua kwa kiwango kikubwa sana suala hili, na halina matatizo tena kwa sababu tunajua baada ya kikao hicho mambo mengi yaliyokuwa yanalamikia yatakwisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Jitu bado unasimama?

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, mimi nashukuru kwa majibu hayo, tutasubiri ndani ya siku chache tu najua kabisa yale yote tunayotarajia kama hayatakuja tutaelewa siku hiyo ambapo si mbali, siku haziko mbali, ila wakajipange vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu, ni hakika, maana yake tozo Halmashauri hawajipangii tu lazima TAMISEMI waidhinishe. Kwa hiyo, ni jambo tu la kukaa ndani ya Serikali kuwekana vizuri ili tozo zinaposhuka kule chini ziwe na *coordination* ya moja kwa moja. Maana ziko Halmashauri

wanajiwekea tu wao na hasa zile Halmashauri ambazo hawapendi mifugo ndiyo taabu kweli, zipo nazo hizo, si mnawasikia hata Wabunge wake wakichangia wanasesma mang'ombe unajua tu huyu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

MHE CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri, na bahati nzuri sana amenitaja kwenye maoni yangu mara kuhusu ukamataji unaendelea wenyewe uhusiano na makosa ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotofautiana na Mheshimiwa Waziri ni kwamba anakamata bila sheria lakini unapouliza swali anajibu kisasa. Amezungumzia muundo wa tume ya kwanza ambayo anasema ilikuwa inahusisha vyombo vyote vya ulinzi na usala na muundo wa tume ya pili, ukisikiliza dosari ambazo zimekuwepo kwenye muundo wa tume yake ya kwanza ya *operation* na yeye *information* alizokua anazipata maana yake ni kwamba anataka tunapopata malalamiko ya mama ntilie kakamatwa yuko sokoni anauza samaki tumbebe kama ushahidi. Tunapopata taarifa kwamba kule waendesa baiskeli, waendesa pikipiki wanaombwa rushwa tuwabebe kama ushaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo ule unaouzungumza hauwezi ukampa taarifa sahihi ambazo yeye anazitaka kwa sababu ameunda yeye. Katika maoni yangu nilimwambia hata ungeweka Jaji kwenye ile tume ukamwingiza kwenye tume yako, halafu akawa sehemu ya watu wanaozunguka na mtumbwi wanatafuta watuhumiwa akiwa na Afisa Usalama na Polisi malalamiko haya yataendelea kuwepo kwa sababu yeye ni sehemu ya watu unaowalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilitaka kutoa ushauri na majibu yake yasiponiridhisha ninakusudia kushika shilingi. Ni kwa nini muundo wake huu auwekee maelekezo, kwanza atuambie, inavyoonekana wale watu wameachiwa

free kwenda kufanya wanachokifikiria ndiyo maana wametoka kwenye Mtumbwi, wakaenda kwenye nyavu, wakaenda kwenye Mabondo, wakaenda kwenye nyumba, wakaenda kwenye barabara, wakaenda kwenye magari; yaani wanakwenda *randomly* inaonekana muongozo haupo sawa.

Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ametengeneza vizuri maelekezo yake; kwa sasa asiendelee na *operation* yake ya awamu ya tatu kwa sababu madhara yake ni makubwa. Atakapotengeneza vizuri *operation* yake sasa na maelekezo yake ya kueleweka na kuweka vizuri mwongozo ndipo aendelee na *operation* yake ya awamu ya tatu.

MWENYEKITI: Narudi tena kwako Mheshimiwa Kanyasu, *specifically* unataka afafanue jambo gani? Tumekuelewa maelezo yako kwa ujumla wake lakini kile ambacho sasa afafanue.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *specifically* kwanza nilitaka *operation* yake ambayo ameipanga sasa kuanza awamu ya tatu, kwa kuwa tayari *operation* mbili za nyuma zina dosari nyingi kwa kukosa maelekezo sahihi isimame mpaka atakapokuwa ametoa maelekezo ya kutosha ambayo yatatusaidia kuondoa malalamiko haya yanayoendelea.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhali.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijieleza vizuri sana pale wakati naongea. Mheshimiwa Kanyasu ni mwenzangu wakati akiwa Mwenyekiti wa Vijana Mkao wa Mwanza mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Vijana Wilaya ya Meatu, kwa hiyo ninamfahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ameniuliza juu ya mwongozo au muundo wa timu yangu hii inayoundwa kwa ajili ya *operation* na muundo wake nimeshaueleza na labda

niongezee jambo moja tu, hawa watendaji wote wanapokwenda kwenye *operation* kule, vyombo vya dola vyote vinaarifiwa, kuanzia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Mkuu wa Wilaya wa eneo hilo, Mkuu wa Mkoa wa eneo hilo. Ndiyo maana hata juzi wakati nahitimisha *Operation Sangara Two* tulikuwa wote, mikoa yote inayozungukwa na Ziwa Victoria; Geita, Mwanza, Simiyu, Mara na Kagera, mikoa yote mitano na tulikuwa na Wakuu wa Mikoa, tukawa na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi pamoja na vyombo vingine vyote vya dola, na tuna-*discuss* kwa kina kwa taarifa moja baada ya nyingine iliyowasilishwa kutoka eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukatoa maelekezo mahususi kwamba watendaji hawa Serikali wanapokuwa kwenye *operation* hizo hawaondoki kwenye mamlaka ya usimamizi wa Serikali ambayo ni Mkuu wa Wilaya wa eneo hilo na Wakuu wangu wa Wilaya wanalo hilo jukumu la kusimamia kuhakikishwa kwamba shughuli za Serikali zimefanyika katika eneo hilo. Kwa hiyo malalamiko yoyote, shida yoyote inawasilishwa katika *level* hiyo ya Serikali ambayo ipo na hajiaundwa na Waziri, ni mfumo wa Serikali ambao upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisimamisha leo *operation* itakuwa ni kufungua lango, nyavu zile, wavuvi haramu wale warejee tena majini. Mimi ninachoweza kukiomba, nimeshaona malalamiko haya ambayo wameyasema Wabunge na wameyasema wengi; kwanza wa ukanda wenyewe ule wa Ziwa Victoria. Nitaomba sana hata baada ya kupitisha bajeti yangu hii hebu tukutane waniambie hasa maeneo yapi ambayo yanalamikiwa ili tuweze kufanya masahihisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na kero hizi ndogo za watu kukatazwa kupanda na samaki kwenye mabasi. Wabunge waliniambia kwa kuniita Mpina rekebisha hili, nikalirekebisha, sasa hivi haizuiliwi kupanda na samaki ambao wanaruhiwi kwenye vyombo vya usafiri, kitu ambacho hakiruhusiwi ni samaki waliovuliwa kwa njia haramu, ni

samaki waioruhusiwa. Mimi ningemuomba kaka yangu Kanyasu kama kuna chagamoto tu za kurekebisha katika *operation* tuondoe tukarudi huko tena kwenye tatizo kubwa ambalo linalilisababishia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukisimamisha *operation* tutasimamisha kwa faida ya nani? Wakuu wetu wa Wilaya si wako kule? Kama mtu anaonewa hatua zitachukuliwa, kama kuna uonevu wa aina yoyote.

Kwa hiyo, mimi namuomba na nilikuwa naendelea kulishawishi Bunge lako lote kwamba sisi kama kuna changamoto ambazo zinahitaji marekebisho, ambazo hazipelekei kuvunja sheria sisi hatuna tatizo, tutafanya hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaombwa Wabunge tujadili suala hili, nina sababu mbili; moja, leo hii kwenye Kiswi cha Bisula na Lyakanyasi wamekwenda watu wa *operation* wanataka mitumbwi iwe na bendera, wavuvi wawe na sare, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri hayaeleweki. Kwa hiyo naombwa Wabunge mniunge mkono tujadili suala hili ili tuweze kupata suluhu ya wavuvi katika Ziwa Victoria. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Katibu wangu anawaorodhesha msijemkasema Spika ananibagua mimi, Katibu ndiyo anawaorodhesha huko.

Sasa hata Wabunge wanaotoka Kongwa nao wanasimama, mnawajua samaki jamani? Haya mashikolo mageni haya. Waheshimiwa Mawaziri nimewaona.

Haya tuenze na Mheshimiwa Papian, jirani wa Kongwa kama unawajua samaki. Mheshimiwa Papian. (*Kicheko*)

MHE. EMMANUEL J. PAPIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi haramu linaloendelea na kulalamikiwa kwa maana ya Waziri kulalamikiwa hili suala si kweli. Suala hili kwa mambo yanayojitokeza sasa hivi ni suala la kawaida, Serikali imefikia wakati wa kufanya haya na yalitakiwa yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

MWENYEKITI: Ni dakika mbili.

MHE. EMMANUEL J. PAPIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunafukuza ng'ombe wa nchi za nje Bunge hili liliridhia na likapiga makofi. Tulikuwa tunaokoa nchi kwa sababu tulikuwa tunatafuta uhalali wa wafugaji wetu na maeneo ya malisho kwa ajili ya watu wetu.

Kwa suala la samaki tunadhani kwa sasa ilikuwa ni lazima haya yafanyike ili tuokoe samaki, mazalia ya samaki waweze kupatikana. Nchi jirani za nje zote; nimetoka Uganda juzi; samaki wanaovuliwa ni samaki wakubwa wa kiwango cha kutosha, hatuwezi kukubali kuvumilia suala la uvuvi wa samaki ambao ni wadogo ili sisi tuendelee kukosa mapato kwa ajili ya nchi yetu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, nakushukuru sana.

Katika orodha yangu hapa sijaona hata mmoja katika Wabunge wa Ziwa Victoria ambalo ndilo linalolalamikiwa. Mheshimiwa Profesa na Mheshimiwa Mabula angalau. Mheshimiwa Profesa dakika mbili, halafu Mabula.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Suala la hali ya wavuvi katika Ziwa Victoria ni tete na mimi naomba kabisa Mheshimiwa Waziri atusaidie kuondokana na *operation aingie* kwenye programu, kwa sababu wavuvi wanakaa roho juu, wanafanyiwa vitendo vya ajabu na Mheshimiwa Waziri anajua mimi mwenyewe nilimuandikia barua nikiwa kwenye

visiwa kuona hali ambayo ilikuwa hairidhishi kabisa kabisa. Kwa hiyo haiwezekani sisi kabisa sisi kama wawakilishi wa wananchi kukaa hapa na ku-*pretendkwamba* mambo yako sawa sawa. Kwa kweli watu wananyanyaswa na wanakomolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena, kwamba Mheshimiwa Waziri tusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mitego ambayo inatoka Arusha, sasa hivi mingine kiwango chake ni haffifu, kwa hiyo unatakiwa kukamata samaki wanaingia mule sangara wapasua ile mitego wanaondoka. Kwa hiyo unakuta kwamba wavuvi ni sekta ambayo tumewatesa sana. Kwa hiyo mimi nafikiria kwamba hapa tunalotafuta ni kwamba Waziri kweli kazi yake ni ngumu lakini *he needs a program* si kwenye vitu vya zimamto na *operation* moja baada ya nyingine. Kwa hiyo mimi nafikiria kwamba hapa tuingie kwenye programu tuondokane na zimamoto, asaidie wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukusanya fedha ni muhimu lakini haiwezi kuwa *at any cost* tumekusanya fedha, ni lazima pia fedha itokane na maendeleo ya wananchi tunaowawakilisha, wananchi ambao Serikali hii ni Serikali ya yao, na Mheshimiwa Rais anapambana usiku na mchana. Sasa huwezi kusema kwamba kukusanya fedha siyo kigezo tu, siyo *parnacea*, siyo mwarobaini, lazima ujue kwamba zile fedha zimekusanya katika mazingira gani. Kwa hiyo mimi ndiyo msimamo wangu kwamba Waziri... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa. Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi pia niungane na Mheshimiwa Kanyasu kwa maana hii kama nimemwelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetangaza *operation* namba tatu itakayoanza muda si mrefu. Hoja ya

Mheshimiwa Kanyasu kabla ya *operation* namba tatu haijaanza ambayo kwa mujibu wa Waziri itakuwa na Mahakimu na watu wengine, tunachokiomba, kabla *operation* hiyo haijaendelea, kwa sababu *operation* iliyopita imeonekana kuwa na madhara mengi makubwa kwa wavuvi, basi Mheshimiwa Waziri aipange vizuri na taarifa zisambae kabla haijaanza iwe Wizara au Waziri amejiridhisha kwamba *operation* itakayokwenda kufanyika haitakuwa na madhara kama haya ambayo tunayapigia kelele sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri huo ndio ulikuwa msingi ambao Mheshimiwa Waziri anaweza akatafakari na akaona ni kweli kwamba *operation* namba tatu inakwenda kuanza lakininaanza kwa mfumo gani kuepuka madhara mengi yaliyojitezea kwa *operation* zilizopita. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Meshimiwa Mussa Mbarouk dakika mbili atafuata Mheshimiwa Sokombi (CHADEMA) kwa dakika mbili.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nafikiri wakati nikichangia nilisema hapa mchana kwamba hizi *operation* mimi sioni tija yake kwa sababu *operation* mara nyingi zina matatizo; na nikatoa mfano wa *Operation Tokomeza* jinsi ilivyoichafua nchi, jinsi ilivyoitia doa Serikali. Sasa Waswahili wanasesma 'kosa si kufanya kosa, kosa ni kurudia kosa, sasa mbona tunakwenda kule kule kwenye *operation*? Halafu kwa nini Waziri anakuwa ni mbishi kiasi fulani? Kwa sababu ajue yeye ataondoka, hiyo misingi anayoiweka yeye ni vyema akaweka misingi mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimtakte tu kwamba asimamishe hizo *operation*, naungana na Mheshimiwa Kanyasu. Vilevile niwaambie wavuvi; njia fupi ya kukatisha hizi *operation*, wakitishia tu kurudisha kadi za CCM kesho asubuhi *operation* zitakufa. Ahsante. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Hilo la mwisho tumefuta kwenye *Hansard* kabisa. Mheshimiwa Sokombi. (*Kicheko*)

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi namuunga mkono Mheshimiwa Kanyasu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli wavuvi hasa hasa Ziwa Victoria wananyanyasika sana. Hebu niambie Mheshimiwa Waziri wewe ni binadamu, wale watu jinsi wanavyonyanyasika kusema ukweli inatia uchungu na inatia huruma kama binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa viongozi hasa hasa huyu Waziri wanatumia nguvu za dola, wanatumia polisi, wanakwenda mpaka ziwani kule kwenye makokoro, wanafika wanapiga mabomu ya machozi, wananchi wanakimbia, wanapokimbia, wanakanyaga watoto, watoto wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni unyanyasajji wa hali ya juu kwa wavuvi. Ninaomba tafadhali sana Mheshimia Waziri, na hii hoja ilyoko mbele yake tunaomba isitishwe, aangalie makunyanzi yaliyoko nyuma halafu tuangalie mbele tunakwendaje hii *operation* kwa kweli isitishwe. Ahsante

MWENYEKITI: Mheshimiwa Januari Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba waliyoyasema Wabunge kuhusu namna *operation* ilivyoendeshwa sisi Serikali tumeyasikia na tumeyachukua na tutakaa pamoja ndani ya Serikali kwa sababu *operation* hii inahusu taasisi kadhaa zilizo chini ya Wizara kadhaa zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. (Makof)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa atatuita katika Kamati Ndogo ya Baraza la Mawaziri, tutapitia, tutafanya tathmini kuhusu awamu zilizoanza kwa madhumuni ya kuchukua hatua za kudhibiti vitendo ambavyo havikuwa vizuri. Si tu katika ngazi ya Wizara lakini pia katika ngazi ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na

Wilaya katika maeneo ambako *operation* imefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabla hatujaanza *operation* ya awamu inayofuatia basi tutakuwa tumerekebisha yale yanayolalamikiwa na Wabunge. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri Kairuki.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuku. Nipende kuunga mkono maelezo ya hoja ya Mheshimiwa Mpina na nikiongezea maelezo mazuri ya Mheshimiwa Januari ambayo ameelezea azama ya Serikali.

Mheshimiwa Mpina ameeleza bayana *operation* hii namna ilivyokuwa ikifanyakazi, hapa kuna *issue* mbili, kwanza kuna suala la utekelezaji wa sheria, lakini pili kuna suala zima la namna ya usimamizi wa utekelezaji huu wa sheria.

Mheshimiwa Waziri amekuwa tayari kwamba atakaa na Waheshimiwa Wabunge, waeleze dosari mbalimbali ambazo wamezishuhudia katika maeneo ambako *operation* hii imetekelze; lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuitia maelezo ambayo Mheshimiwa Januari ameji-*commit* hapa, kama Serikali tutaweza kukaa natutayafanyia kazi. Tumpe fursa Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali, tuyapitie masuala haya, tusikilize dosari na mapendekezo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini pili, namna ambavyo mtaeleza uzoefu uliojitokeza katika *operation* hizi na naamini hii itaweza kujenga tathmini nzuri katika kuelekea katika *operation* ya tatu. Nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimefurahi sana kwa michango ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge na nakubaliana kwamba kwanza tulipomaliza *Operation Sangara* awamu ya pili hatukuondoka wote, kwa maana

ya kuziba ile mianya ambayo inaweza kutokea kule ziwani watu wakaondoka. Hata hivyo kwa *operation* awamu ya tatu bado hajjaanza isipokuwa sasa hivi kuna kupindi cha mpito tu cha ulinzi ili kuhakikisha kwamba watu wasiingie tena na zile nyavu haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hapa nilikuwa nataka kuzungumza kwamba mimi kama nilivyosema niko tayari, hata kesho nikae na Wabunge wote na nikishamaliza kukaa na Wabunge, niende kwenye kikao ambacho Mheshimiwa Makamba pale amependekeza cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukakae tukiwa na taarifa za Waheshimiwa Wabunge za malalamiko za maeneo yote ili twende tukajadili kwa kina na kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maelezo ndiyo hayo, kwa hiyo, niko tayari...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Kanyasu sasa nakurudishia. (*Makofii*)

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru wote ambao wameunga mkono hoja yangu na kimsingi unajua tunatofautiana sana uelewa.

Mheshimiwa Papian yeye alilingia chaka kabisa, hatupingi sisi habari ya *operation* kwa maana ya ukamataji wa uvuvi haramu, tunachopinga ni matukio yaliyoambatana na zoezi, sasa wengi hawaelewi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimshukuru sana Mheshimiwa Makamba kwa sababu ulichozungumza *actually* kila mtu alitarajia kwamba kasoro ambazo zimejitokeza si za Wabunge, ni kasoro za wananchi, kwa hiyo majibu ya Serikali ni hayo. Mimi Mheshimiwa Waziri kama alivyosema, kwamba tulikuwa naye Umoja na Vijana na Naibu wake tulikuwa naye Umoja wa Vijana, hivyo sina sababu ya kuendelea kushikilia shilingi na naomba nimrudishie shilingi yake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Kanyasu kwa kururahisishia jambo hili tunakushukuru sana.

Sasa ni ushauri wa jumla tu Mheshimiwa Waziri, hizi *operation* hizi ni lazima kufungua masikio yote mawili. Wako watu wako Serikalini wanakuletea ripoti, lakini pia kuna *feedback* hii tuliyopata kutoka kwa Wabunge. Kwa hiyo, lazima kufungua masikio yote mawili kwa sababu uzoefu umeonesha, kwa mfano, tungesema tuunde Tume ya Bunge ingeleta mambo ya ajabu sana hapa, kweli kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata tunavyokwenda kwenye vikao tusiende na hii *notion* ya ripoti za usalama, kwani *Operation Tokomeza* hawakuwepo Usalama? Hawakuwepo Polisi? Hawakuwepo hao wote unaowataja? Kwa nini kulikuwa na ukatili mkubwa kiasi kile? (*Makofî*)

Kwa hiyo, ni lazima kuangalia ili na hao nao wasije wakakutia kwenye chaka. Lazima kwenda kupima kidogo *ku-balance*, tusiende tu kwamba tuko *right*, tuko *right*, ndio ushauri wa jumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, na kama sitaridhika nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu chake cha hotuba mwanzo mwisho sijaona mkakati wowote wa kuwasaidia wavuvi wadogo zaidi ya *operation*. Nimeona kwenye kitabu chake sana sana alichotenga katika mwaka unaokuja ni semina kwa mahakimu, viongozi wa dini, madiwani, wapelelezi, waendesha mashitaka, maafisa uvuvi lakini si kwa wavuvi wenywewe wadogo, hii kazi si ya kimaskini kama vile wanavyoifirkira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenda *deep sea* unahitaji vyombo na zana bora za kisasa. Wavu mmoja tu wa kwenda

kuvua hao jodari, papa si chini ya shilingi 300,000 na *minimum* unahitaji nyavu si chini ya kumi hizo ndizo ndogo kabisa. Sasa ili uweze kwenda huko unahitaji mtaji mkubwa sana na ukiangalia katika hii bajeti hakuna bajeti ya ruzuku yoyote kwa wavuvi zaidi ya ruzuku za *operation*, kufungua bandari, na bandari hizi ni wavuvi wa kutoka nje na sio wavuvi wadogo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba anieleze ana mkakati gani wa kuwawezesha wavuvi wadogo? Vinginevyo natoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, wanaulizia programu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, naomba tu kwanza nimirshukuru tu Mheshimiwa Hawa Ghasia na nimpongeze kwa sababu mara zote hapa Bungeni yeche amekuwa akisisitiza sana katika kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wavuvi wa Mtwara na maeneo mengine ya ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, Wizara yetu inayo programu ambayo ni endelevu. Programu ile ni ya kuwasaidia wavuvi; na hivi sasa tumekuwa tukiitazama. Mwanzo tulikubaliana kwamba tutatumia mfumo wa kuwapatia mashine zile kwa ajili ya kupachika katika mitumbwi yao katika vyombo vyao kuweza kuingia baharini. Mashine zile tumekubaliana hatutoi kwa mtu mmoja mmoja, tunatoa kwa vikundi ambapo kikundi kinadhaminiwa na Halmashauri yenyewe, kinatoa asilimia 60 na Serikali inatoa asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, tuliwaza sana, ilikuwa tungeweza kuwapa nyavu, ilikuwa tungeweza kuwapa vifaa vingine vyovyote. Hata hivyo tulidhani kwamba hizi mashine zinaweza kwenda kuwa na msaada zaidi. Asilimia 40 tayari inakuwa imeshalipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, tulichokiona ni kwamba bado vikundi vyetu vingi hata hiyo asilimia 60 yenyewe

inaonekana kwao ni mtihani, ikiwani ni pamoja na vikundi vya kwa mama yangu hapo Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba sisi katika Wizara kwa kuwa tunao mpango wa kuona namna ya kuwasaidia wavuvi jambo hili tumelichukua kama changamoto. Sasa hivi watalaan wetu wanaangalia na kudurusu mipango hii kila mara ili iweze kuendana na matakwa ya wavuvi wetu.

Pia habari njema kwa wavuvi wote wa Ukanda wa Pwani, nikiwemo mimi mwenyewe; ni kwamba tuna mradi mkubwa sana wa *SWIOFish* wa *World Bank* Tuna bilioni nane, zile zitasaidia mambo mbalimbali hata huduma za kijamii. Kwa hivyo naomba niwahakikishie Wabunge wote wa Ukanda wa Pwani akiwepo Mama Hawa Ghasia ya kwamba wakae mkao wa sawa sawa ili wavuvi wetu waweze kupata faida hiyo.

MWENYEKITI: Kwa majibu hayo Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi sijaridhika, kwa sababu hiyo mashine ni shilingi milioni nane wao wanatoa shilingi milioni mbili tu, hiyo shilingi milioni sita hao wavuvi wangu wadogo wanazitoa wapi? Halafu kwa miaka minne wana-*engine* 73. *Engine* 73 gawa kwa Wilaya 14 zilizoko mwambao wa bahari ni wastani wa *engine* 18 kila Wilaya nina vijiji zaidi ya 30, siwezi kugawa hata *engine* moja moja. Bado mpango uliopo hauridhishi naomba niungwe mkono kujadili mpango wa kuwawezesha wavuvi wadogo.

MWENYEKITI: Katibu andika wavuvi wa Pwani.

Wakati bado Katibu anaandika inanikumbusha enzi hizo nilivyokuwa Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na mazingira tuliwahi kutembelea Jimbo la Mheshimiwa Hawa Ghasia. Palikuwa na mradi wa kutoka Serikali ya Ufaransa na Mradi wa *MACEMP* wa kuwasidia wavuvi wadogo kwenye kijiji

kimojawapo kinaitwa Nalingu. Tulifukuzwa huko, walikuwa hawataki kabisa hiki anachokisema Mheshimiwa Mbunge leo. Tulika pale siku mbili na maelezo yetu yote yalikauka, enzi hizo Mwenyekiti wa Kamati alikuwa Mama Makinda na mimi Mjumbe wa Kamati hiyo, ilikuwa shughuli, patashika tunaulizwa ninyi hamna bahari kwenu? Palekeni kwenu huko. Hiyo ilikuwa *story* tu sasa tuanze na Mheshimiwa Dau na Mheshimiwa Kawambwa.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia hapa nilisema mapema tu kwamba Wizara lazima ijipange vizuri aiache huu utaratibu wa kufanya kazi kwa *operation*. Ni lazima waiachie mifumo ifanye kazi. Hamuwezi kufanya kazi kama *fire brigade*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilio na kutwa nzima jana na leo hapa mazungumzo yamekuwa ni habari ya nyavu. Leo katika zana za hizo za uvuvi ambazo vimeziwa kule Sirari, kuna nyavu zimeziwa kule na ugomvi ni nyavu. Leo Wizara inakuja na hoja kwamba watatoa mashine za bei nafuu.

Mimi nafikiri wangeanza kwanza kutupatia hizo nyavu na wala si mbali, waziruhusu zile nyavu ambazo wamezizua mpakani kule. Nyavu halali zije ziingie na watu tuko tayari, na wavuvi wetu wako tayari kununua nyavu. Hizo mashine zenu hizo za msaada tunazitaka, lakini ugomvi uko kwenye nyavu. Mtatupatia mashine ukishatupatia mashine halafu nyavu napata wapi? Nikiweka nyavu...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa umeelewka. Mheshimiwa Jenista nilikuona ulisimama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuelewa sana dada yangu

Mheshimiwa Hawa Ghasia. Jambo analolizungumza kimsingi ni suala zima la kuwawezesha wananchi na hasa kuwawezesha wavuvi kwenye sekta ya uvuvi, lakini waweze kujijenga na kufanikiwa katika kujenga uchumi wao.

Mheshimiwa Hawa Ghasia anajenga hoja ya msingi, kwamba pamoja na programu hiyo nzuri inayoendeshwa na Wizara. Lakini mtazamo ni kwamba ni lazima kupanua uwezeshaji huo ambao utawafikia wavuvi wengi na wengi wataweze kujijenga na kufanya shughuli hizo za uvuvi kama watasaidia sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba, kwanza nimuombe dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia aridhie huu mpango ulioanza kwenye Wizara, lakini kwa kuwa sisi Serikali tunafanya kazi kwa pamoja na tunazo njia nyingine za ziada za kuwawezesha wananchi wetu katika vikundi vyta miradi hiyo midogo midogo kama hiyo miradi ya uvuvi baharini; tunao uwezo pia wa kuangalia mifuko mingine ambayo inaweza ikaongeza nguvu katika programu kama hiyo na hivyo wavuvi hawa wadogo wadogo kwenye vikundi vyao wakawenza tu kufikiwa na kufanyiwa hizo kazi wanazozihitaji. Uzuri ni kwamba hatuwezi kuanza kwa wote, lakini tunawenza kujunganisha pamoja.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Hawa Ghasia aachie hiyo shilingi Serikali tutafanya kazi kwa pamoja kuangalia mahitaji hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ulega, halafu Mheshimiwa Hawa tufungie, kwa dakika moja.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kumuomba na kumsisitiza Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa heshima kubwa na taadhima na bahati nzuri Mheshimiwa Jenista Mhagama ameliweka vizuri zaidi. Sisi katika programu zetu tulizonazo tunayo Programu ya Wavuvi Skimu ambayo inaendeshwa na NSSF. Wanatoa mikopo, wanawapa na *benefits* zingine zote wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika wavuvi wa Mtwara hawajafikiwa na programu hii atuachie shilingi yetu, namhakikisha ya kwamba mimi mwenyewe nitahakikisha nazungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF na tutafanya kazi pamoja na Wizara yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo itahakikisha programu hiyo inafika na Mtwara, Lindi na kote Pwani ilimradi wavuvi wale waweze kujengewa uwezo na waweze kupata hizo mashine kama binadamu wengine.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa turudishie shilingi.

MHE.HAWA GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi lakini Mheshimiwa Jenista na Mheshimiwa Ulega ni lazima wafike kwenye Jimbo langu haya waliyoyasema wakafanye kwa vitendo.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Sasa Waheshimiwa wabunge kama mnavyojua huu mwezi mtukufu. Nina mamlaka ya kuongeza nusu saa lakini sitafanya hivyo kwa sababu busara ni kwamba lazima tumalize saa 12.00 jioni. Kwa hiyo Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti tuko fungu 99 Maendeleo ya Mifugo...

MWENYEKITI: Sasa nisomee ile Kanuni ya 104 tu, kwa muda uliobaki.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2) inasema; Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kumaliza muda chini ya fasili ya (1) na Kamati bado hajjamaliza kupitisha mafungu yote mwenyekiti atafunga mazungumzo yanayoendelea na papo hapo atawahoji wajumbe kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo.

MWENYEKITI: Haya tunaingia kwenye *guillotine*, Katibu sasa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 1001 - <i>Administration General</i>	4,471,936,196/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	1,323,940,112/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	1,288,128,386/=
Kif. 1004 - <i>Research, Training and Extension</i> ...	7,357,725,116/=
Kif. 1005 – <i>Info, Educ. and Com Unit</i>	390,763,186/=
Kif. 1007 – <i>Internal Audit Unit</i>	416,054,095/=
Kif. 1008 – <i>Procurement Management Unit</i>	556,121,186/=
Kif. 1009 – <i>Legal Services Unit</i>	283,468,000/=
Kif. 1010 – <i>Info Comm nd Technology</i>	538,991,072/=
Kif. 7001 – <i>Veterinary Services</i>	8,382,599,777/=
Kif. 7005 – <i>Veterinary Council of Tanzania</i>	426,077,386/=
Kif. 8001 – <i>Livestock Prod. and Marketing</i>	4,926,858,488/=
Kif. 9001 – <i>Fisheries Development Division</i>	0/=
Kif. 9002 – <i>Aquaculture Development Division</i>	0/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Maendeleo ya Uvuvi

Kif. 9001 – <i>Fisheries Dvt Division</i>	12,013,443,000/=
Kif. 9002 – <i>Aquaculture Development</i>	952,963,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Maendeleo ya Mifugo

Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	152,620,000/=
Kif. 1004 – <i>Research, Training and Extension</i>	452,990,000/=
Kif. 7001 – <i>Veterinary Services</i>	1,000,000,000/=
Kif. 8001 – <i>L/stock Prod. and Marketing</i>	3,394,390,000/=
Kif. 9001 – <i>Fisheries Development Division</i>	0/=
Kif. 9002 – <i>Aquaculture Development Division</i>	0/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Maendeleo ya Uvuvi

Kif. 9001 – *Fisheries Development Division* 5, 926,680,000/=
Kif. 9002 – *Aquaculture Dvt Division*.....1,200,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea. (*Makofi*)

T A A R I F A

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu kama kamati ya matumizi na kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kuyapitisha. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako. Naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ni wajibu wangu sasa Waheshimiwa Wabunge kuwahoji kufuatana na hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kutokea jana mpaka leo tunayo. Kwamba sasa mkubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. (*Makofi*)

*(Hoja llitolewa lamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha
2018/2019 -Wizara ya Mifugo yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Kwa niaba yenu Wabunge nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa mjadala huu ambao umeendelea wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu hakika mmepita kwenye tanuru la moto, naamini kabisa kwa michango iliyotokea hapa kwa siku hizi mbili imewaongezea kitu fulani cha kwenda kufanya kazi mnaporudi Wizarani. (*Makofi*)

Vile vile niwapongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi na watumishi wote. Kwa kweli kazi mnayoifanya tunaithamini, tunaiona na sisi Bunge tunawatachia kila la heri katika mwaka ujao wa fedha.

Tunawaomba sana Wizara ya Fedha, jamani, jamani, msalieni Mtume Wizara ya Fedha, kwamba kweli ndugu zetu wa mifugo na uvuvi hawa hamuwapi hela ya maendeleo kama Wabunge walivyosema kweli kabisa jamani, yaani mfuto kabisa. Hapana! Hapana! haiwezekani mwakani tusirudi tena na hadithi hiyo. (*Makofi*)

Tukirudi na hadithi hiyo itahama kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sasa itabidi Waziri wa Fedha akae kikaangoni hapa; atupe kigezo chake cha kugawa pesa mpaka mifugo na uvuvi haipati kitu halafu Waziri wa Kilimo ye ye ndiye anapata kidogo kabisa. Hebu mkaangalie taratibu zetu za kugawa hela huko. Kilimo, Mifugo na Uvuvi ndio maeneo ya wananchi hayo kwa hiyo kwa kweli mwaka huu tumewasurubu wenyewe, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Mifugo na kadhalika lakini mwakani kama hawakupata pesa kwa kiasi ambacho tumekiona safari hii kweli itabidi tulale mbele na Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Pia katika kuwatachia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, ukombozi wetu kama alivyosema, nadhani Mheshimiwa Kishamba *or somebody*, kwamba ukombozi wetu katika mambo ya uvuvi ni *aquaculture*. Kabisa, kabisa wala si hiyo

ya uvuvi wa baharini sijui ya uvuvi wa ziwani sijui ukoje ukoje. Hata huko ziwani wamesema baadhi ya wavuzi wa *Lake Nyasa* hapa, upande wa pili wa Malawi wanafuga samaki ziwani na wanavuna samaki wengi lakini kwa kuwafuga ziwani. Sasa na sisi inabidi tujifunze kufuga samaki, ziwani humo humo lakini unawafuga samaki, na ni wa kwako, unawavua unavyotaka na kadhalika.

Lakini ufgaji huo wa kisasa wa mabwawa maana yake ni kwamba hata Mkoa wa Dodoma, Singida, Shinyanga na Manyara mikoa ambayo ni mikame kwa kiasi fulani ina uwezo wa kufuga samaki na kuzalisha samaki kuliko Ziwa Victoria, yaani kuzalisha tani nyingi kwa kupitia utalaam huo.

Kwa hiyo tunadhani kitengo hicho mngekipa uimara zaidi, na katika fedha za maendeleo basi mngejaribu kuangalia, kama wallwyosema mfike mahali muanze kugawa vifaranga watu wengi wameanza kuitikia wito wa kuwa na mabwawa ya samaki, hasa mionganoni mwa wasomi, wengi sana wameanza kuitikia jambo hili. Tukienda upande huo naamini tunaweza tukawa na biashara kubwa sana ya samaki ambayo itatokea katika nchi yetu.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri, time ya kuahirisha imeshafika. Waheshimiwa Wabunge naomba sasa niahirishhe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi na baada ya hapo Waziri wa Maliasili na Utalii atakuwa kilingeni.

Kesho walenga shabaha saa 1:00 asubuhi. Haya jamani nawaageni. (*Kicheko*)

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 21 Mei, 2018 Saa Tatuhu Asubuhi)*